

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Tano – Tarehe 11 Septemba, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO  
(K.n.y WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):**

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba (*Intergovernmental Agreement – IGA*) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (*East Africa Crude Oil Pipeline – EACOP*) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania).

**MHE. DEO F. NGALAWA - MAKAMU MWENYEKITI WA  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI):**

Maoni ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba (*Intergovernmental Agreement – IGA*) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

na Serikali ya Jamhuri ya Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (*East Africa Crude Oil Pipeline – EACOP*) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania).

**MHE. DEVOTHA M. MINJA (K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI):**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Nishati na Madini kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba (*Intergovernmental Agreement – IGA*) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda kuhusu Mradi wa ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (*East Africa Crude Oil Pipeline – EACOP*) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania).

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Kuunganisha Mashirika ya Hifadhi ya Jamii**

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Mafao ya wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mashirika mengi ya Hifadhi ya Jamii yamekuwa na utata kuhusu fao la kujitoa. Je, Serikali inatoa tamko gani ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kuunganisha mifuko hiyo na kuondoa mkanganyiko kwa wanachama?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mkataba wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) Na. 102 wa mwaka 1952, fao la kujitoa sio mionganoni mwa mafao yaliyoainishwa katika mkataba huo. Kwa hapa Tanzania fao la kujitoa ni utaratibu wa wanachama kujitoa na kuchukua mafao yako katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inayotoa mafao ya pensheni kabla ya kufikisha umri wa kustaaifu. Utaratibu huu umezoleka mionganoni mwa wanachama wa mifuko hiyo na hata kuonekana ni mojawapo ya mafao ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto ya kipato inayowakabili wafanyakazi wale wanaopoteza ajira, Serikali itawasilisha Bungeni mapendekezo ya marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii yatakayoanzisha fao la upotevu wa ajira (*unemployment benefit*) kwa wafanyakazi watakaokuwa wanapoteza ajira kabla ya kufikisha umri wa kustaaifu kazi. Fao hili litakuwa linatolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inayotoa mafao ya pensheni.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya wingi wa mifuko inayoiakabili Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, mwaka 2015 Serikali ilifanya tathmini ya mifuko yote ya pensheni kwa lengo la kuangalia uwezekano na namna bora ya kuiunganisha. Matokeo ya tathmini hiyo yalionesha kuwa inawezekana kuunganisha mifuko hiyo na kubaki na michache kwa kuzingatia hali halisi ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matokeo ya tathmini hiyo, Serikali imeandaa mapendekezo ya kuunganisha mifuko mitano inayotoa mafao ya pensheni na

kubaki na michache iliyo imara. Mapendeleko hayo yameshajadiliwa na wadau wa kukubaliwa. Hatua inayoendelea hivi sasa ni kuwasilisha mapendeleko hayo katika vikao maalum vya Serikali ili Serikali itoe kibali. Matokeo ya kuunganisha mifuko hiyo ni pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji, kuboresha mafao na kuifanya mifuko kufanya kazi kwa ufanisi na kwa uendelevu katika kipindi cha muda mrefu ujao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yamejikita katika kuelezea uhalisia wa mifuko hii na changamoto zilizopo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, kwa vile inaonekana wazi kwamba watumishi wengi na hasa wanachama wa mifuko hii wanapokuwa wameachishwa kazi au wametorokwa na waajiri wao wanahangaika sana kuweza kujikimu katika maisha yao na hiyo sio hiari yao isipokuwa wameachishwa kazi au wametorokwa na **waajiri**. Sasa Serikali haioni kwamba kuna haja hawa watu ambao wanapata dhahama hii, wasaidiwe kuchukua mafao yao ili wajikimu katika maisha yao wakati wakitafuta kazi zingine za kuweza kujipatia kipato?

Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kabisa kwamba mifuko hii ina changamoto nyingi sana, ikiwa ni pamoja na gharama za uendeshaji ambayo inakula mifuko ya wanachama hawa, lakini pili kutokana na kwamba mifuko hii imekuwa mingi mno na utitiri ambao mafao yao hata hayana tija kwa wanachama wenyewe.

Je, ni lini sasa Serikali, kufuatia kauli ya Mheshimiwa Rais siku ya sherehe ya Mei Mosi Moshi katika Mkoa wa Kilimanjaro alipotaka Serikali ilete hoja hapa Bungeni, Muswada wa kuweza kuigawa mifuko hii kutoka utiriri huu

na kubakiwa na angalau mifuko miwili tu ambayo itakuwa na sekta ya umma au na sekta binafsi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raphael Chegeni umeanza na ni lini, hujamalizia sasa swalı lako ni lipi kwenye swalı lako la pili. Sekunde tano, usirudie maelezo, maelezo ameshayasikia, lakini swalı lako ni nini, yaani maana umeuliza ni lini halafu ukaanza maelezo bila kusema sasa swalı lako ni lini nini yaani? Malizia.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba ni lini Serikali itatii maagizo ya Mheshimiwa Rais kwa kuleta Muswada hapa Bungeni ili tuweze kurekebisha suala la mifuko hii? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalı lake la kwanza naomba tu nirudie majibu yangu ya msingi ya kwamba katika kuliangalia suala hili la fao la kujitoa kama liliyokuwa linaitwa, sisi kama Serikali na kupitia maazimio ya Bunge hili mwaka 2012 ambayo ilisema Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kushughulika na suala hili la fao la kujitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kama nilivyosema tayari tumekwishaanza maandalizi ya kuja na utaratibu mwingine mbadala ambao utamfanya mfanyakazi wa Kitanzania yule ambaye ataachishwa kazi na hajafikisha umri huo wa miaka 60 wa kuchukua mafao yake, tuone namna ya kuweza kuliweka sawa na kumsaidia asipate shida katika muda huu wote wakati bado anasubiria kupata ajira nyininge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kwa sababu jambo hili linakuja Bungeni, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge avute subira. Muda sio mrefu tutawasilisha mapendekezo yetu hayo na ninyi kama Wabunge mtapata nafasi za kuweza kuchangia na kutushauri vema sisi kama Serikali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lke la pili; ni lini tutatii maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kuunganisha mifuko hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba sisi baada ya tamko la Mheshimiwa Rais kazi hiyo imefanyika mara moja na katika majibu yangu ya msingi nimesema tayari tumeshakutana na wadau, tumezungumza namna bora ya kuunganisha mifuko hii na muda sio mrefu tutatoa pia taarifa sehemu ambayo tumefikia na tutawapa pia *the way forward* ya namna ambavyo mifuko hii itakuwa. Hivyo Mheshimiwa Mbunge vuta subira tu, hii yote iko katika mipango na agizo la Mheshimiwa Rais tumelitekeleza. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimewaona. Nitoe tu ushauri ili tuweze kwenda vizuri, maswali ya nyongeza yawe kwa kifupi maana muda wetu hautoshi, tunajua tuna saa moja na nusu.

Mheshimiwa Richard Mbogo swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Badala ya kuwa na fao la kupoteza ajira, kwa nini Serikali isilete sheria na kuibadilisha katika mafao ya mtu apewe angalau theluthi moja ya mafao yake baada ya kuwa amepoteza ajira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee tu maneno yangu ambayo nimeyasema pale awali katika jibu la msingi ya kwamba Serikali tutaleta mapendelekezo yetu na Bunge hili litakuwa na nafasi ya kuweza kutushauri vema. Mimi nafikiri katika hali hii ambayo tumefikia hivi sasa, Waheshimiwa Wabunge mtuvumilie na msubiri muone mapendelekezo ya Serikali na baada ya hapo mtatushauri tuone namna bora ya kuweza kulifanya jambo hili tuondoe matatizo kwa wafanyakazi wetu. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasuku Bilago, swali la nyongeza.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mfanyakazi aliyemaliza kazi kwa kustaaifu au kupoteza kazi aweze kulipwa mafao yake katika mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ni pamoja na kupata barua yake ya mwisho. Wafanyakazi waliopatikana na vyeti *fake* hawajapata mafao yao kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa sababu hawana barua za kumaliza huo ufanyakazi *fake*.

Je, Serikali iko tayari kuwapa barua zao ili wakahangaike kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpungeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na majibu fasaha na huo ndiyo utaratibu wa Serikali katika kushughulikia yale ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu la Mheshimiwa Bilago, swali hili la mafao ya watumishi ambao wameonekana kwamba ni watumishi wenye vyeti *fake* na ambao wamepatikana na masuala kadha wa kadha katika utumishi wao, limekuwa likijiwi na Serikali mara kadhaa ndani ya Bunge lako Tukufu na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine wote waendelee kuvuta subira, yale ambayo yamekuwa yakijibiwa na Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma hayo ndiyo ambayo yatakuja kutekelezwa baada ya Serikali kufikia maamuzi yale ambayo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma amekuwa akieleza humu ndani ya Bunge lako Tukufu kila siku.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa Mbunge wa Biharamulo Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 53

**Kero ya Kutopandishwa Madaraja kwa Walimu nchini**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Walimu Wilayani Biharamulo na kwingineko nchini wanalalamika kwamba jitihada zao kwenda masomoni kujiedeleza zinafuatiwa na kusitishwa kwa upandaji wa madaraja yao katika utumishi wa umma. Pale ambapo mwalimu kapanda daraja kunaenda sanjari na yeye kuwa masomoni.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kero hii na kukatishwa tamaa kwa walimu wetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapongeza walimu wote na wataalam mbalimbali wanaojiendeleza kwa lengo la kuongeza ufanisi wao wawapo kazini. Kwa utaratibu wa sasa kupanda daraja kunaendana na matokeo ya ufanisi kazini baada ya kupimwa jinsi mtumishi alivyotekeleza malengo yake. Kwa utaratibu uliopo, mwalimu aliyejiendeleza hadi ngazi ya stashahada au shahada anapaswa kubadilishiwa muundo baada ya kuwasilisha vyeti vyake kwa mwajiri wake. Hivyo, waajiri wote wanapaswa kuzingatia taratibu za utumishi kwa kutenga bajeti kwa watumishi walio katika maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oscar Mukasa, swali la nyongeza.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini naomba kufahamu kwamba kwa maelekezo hayo ambayo Serikali imeyatoa kwa waajiri kutekeleza upandishwaji wa madaraja hayo.

Je, Serikali iko tayari sasa kuratibu suala hilo ili kuhakikisha kwamba tunafanya uhakiki wa walimu wote wenye malalamiko haya ili yapatiwe utatuzi.

Swali la pili, kwa sababu pia yako malalamiko kutoka kwenye Halmashauri zetu kwamba Walimu wanapokwenda kujiendeleza unatokea upungufu wa Walimu kwenye shule wanazotoka.

Je, Serikali iko tayari kutumia vizuri fursa ya Chuo Kikuu Huria ili yenye kwa ngazi ya Serikali Kuu iratibu namna ya kuwasaidia Walimu wajiendeleze kwa kupitia Chuo Kikuu Huria bila kuathiri uwepo wao kwenye shule zao? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hoja ya Mheshimiwa Oscar ni kwamba kufanya tathmini ya kuratibu vizuri mchakato huu, naomba tulipokee hili kwa sababu lengo kubwa ni kwamba kama Serikali tuna haja ya watumishi mbalimbali ambao malalamiko yao yapo yaweze kufanyiwa kazi kwa sababu tunajua yakifanyiwa kazi vizuri ndiyo wataweza kufanya kazi vizuri wanapokuwa ofisini mwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mukasa nadhani hii ni hoja ya mapendekezo na sisi

tutaangalia jinsi gani tuweze kuratibu vizuri ili haki ya mfanyakazi iweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili katika eneo la pili ni kwamba jinsi gani tufanye kwamba tutoe maelekezo ya watumishi wote kada ya ualimu kutumia Chuo Kikuu Huria. Nadhani tuweke hili dirisha wazi kwa sababu kila mwalimu ana *preference* yake na kitu gani anachokihitaji, isipokuwa jambo la misngi ni lazima tuweke mipango mizuri lengo ni kwamba walimu watakapoenda kujiedeleza basi tusiwe na mapungufu makubwa katika maeneo yetu. Tunajua kwamba tatizo hili limekabili maeneo mbalimbali lakini hoja hii ni hoja ya msingi nadhani hili sasa katika mamlaka ya Serikali za Mitaa tutatoa maelekezo mahsusni ya kiutawala/kiofisi kwamba nini kifanyike kama walimu wangapi wanatakiwa wakiondoka wengine wabaki, ili watoto wasiathlirike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo katika mchakato wetu ambao tunaufanya hivi sasa lengo kubwa ni kuajiri walimu wapya tunajua kwamba tukiongeza idadi ya Walimu tutaweza kupunguza kwa kiwango kikubwa tatizo hili ambalo liko hivi sasa katika Halmashauri zetu. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nataka kuweka msisitizo tu kwamba msimamo wa Serikali kuhusu wanafunzi kujunga na vyuo vikuu ni kwamba mwanafunzi anachagua mwenyewe mahali ambapo anataka kusoma, kwa hiyo utaratibu huo unawahusu watarajiwa wote wa vyuo vikuu ikiwa ni pamoja na walimu. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuweka tu mazingira mazuri ili wanafunzi waweze kuendelea kuwa na fursa ya kwenda mahali wanapotaka lakini Serikali haiwezi ikampangia mtu kinyume na matakwa yake. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bobali swali la nyongeza.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tabia kwenye Halmashauri wanapokwenda masomoni baadhi ya watumishi kwenye Halmashauri, Halmashauri zinakuwa zinagharamia hususan wale walioko kwenye ngazi ya pale Halmashauri. Lakini si kwa kada za ualimu na kada zingine.

Je, nini kauli ya Serikali kwamba Halmashauri zinagharamia masomo kwa wale watumishi waliopo ndani ya Halmashauri pale pale au kwa watumishi wa Halmashauri nzima? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ni kwamba kuna utaratibu wa mapendelekezo ya watu kuonyesha *preference* yao kwamba watu wanataka kwenda kusoma, hili mara nyingi sana huwa inawekwa katika mchanganuo wa kibajeti katika kila Idara, kwamba kila Idara ina utaratibu na mipango yake kwamba mwaka huu kuna watu wangapi wataenda kusoma. Kwa hiyo, jambo hili sio wale wa Makao Makuu peke yake hapana, jambo hili maana yake ni kwa Halmashauri nzima, kama kuna Halmashauri ambayo inafanya kuwapa upendeleo maalum wale waliopo Makao Makuu peke yake, hilo ni kosa na halikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, utaratibu ni kwamba mpango wa bajeti wanapopanga bajeti wanapanga mwaka huu Idara fulani tutapeleka watu fulani kusoma katika *level* fulani ambayo inaingizwa katika bajeti, *then* unaweka hilo *open door policy* katika hiyo Idara, kila mtu aweze ku-*apply* kuangalia nani ata-*qualify* katika kipindi hicho kuweza kupata fursa ya masomo, kwa sababu mkate

huo ni mkate wa Halmashauri nzima siyo watu maalum katika Makao Makuu ya Halmashauri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Kikwete swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wengi walipata fursa ya kwenda kuijendeleza na waliweza kuijendeleza, pale wanapokuwa wanafanya hayo masomo yao katika ngazi ya shahada wanapokwenda kwenye ile *Block Teaching Practice* walimu hawa wanapangiwa kwenye shule za sekondari na wanapomaliza bado walimu hawa wanarejeshwa kwenye shule za msingi. Wanaporejeshwa kwenye shule za msingi, yale waliyosomea hayapo kwenye shule za msingi bali yapo kwenye shule za sekondari.

Serikali hapa ina utaratibu gani wa kubadilisha au wa kutengeneza mitaala kuhusiana na shule za msingi ili wakitoka kule warudi kule kule walikotoka? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mama yangu Salma Kikwete anazungumzia changamoto za jinsi gani tuweze kuboresha elimu yetu kwa watu walioko katika vyo wanapoenda kwenye katika zile *field practical* na wanapoenda kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni wazo kwa sababu bahati nzuri Mheshimiwa ni mwalimu anajua changamoto gani zipo na vipi tuziboreshe. Mimi naomba tulichukue hili kama wazo jema, kwamba nini tufanye hasa katika suala zima la mitaala kiujumla wake, hata hivyo, tuangalie ni jinsi gani wanafunzi wetu wanapokuwa katika masomo, kile kitu ambacho anaenda kufanya *field practical* na iwe *best practice* akienda kwenye kazi. Kwa hiyo, nasema huu ni ushauri mzuri, Serikali tumeuchukua, tunachukua mawazo mazuri, kwa sababu tuko katika mchakato wa kuboresha

elimu yetu iwe elimu shindani tunachukua mawazo haya kwa ajili ya kuyafanya kazi vizuri. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TAKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. nampongeza Mheshimiwa kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongezea tu kwamba lengo la kufanya mafunzo kwa vitendo ni kutoa fursa kwa wanafunzi kuweza kufanya kwa vitendo kile ambacho wanajifunza. Katika *teaching practice* jambo kubwa ambalo linaangaliwa ni ule mfumo wa ufundishaji yaani kwa kingereza tunaita *pedagogical skills*, jinsi ambavyo mwalimu anaweza akalihimili darasa, anaweza akafanya yale ambayo yanatakiwa kumudu darasa lake. Kwa hiyo, mwalimu ambaye anajifunza mafunzo ya sekondari *principal* za darasani kwenda kujifunza, hata akienda kufanya katika shule za msingi hakuna jambo lolote ambalo linaharibika. Ndio maana wapo walimu wa sekondari wanapangiwa kwenda kufundisha shule za msingi kwa sababu kinachoangaliwa ni ule uwezo wa mwalimu kufanya ule ufundishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na nini anachokifundisha, ukiangalia maudhui ya mtaala katika elimu ya msingi ni ya kiwango cha chini kuliko ya sekondari. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba mwalimu ambaye ana uwezo wa kufundisha sekondari atakuwa ni mwalimu mzuri sana katika kufundisha shule za msingi. (*Makofî*)

Na.54

**Ujenzi wa Barabara ya Rujewa - Mbarali**

**MHE. ORAN M. NJEZA (K. n. y MHE. HAROON M. PIRMOHAMED)** aliuliza:-

Mji Mdogo wa Rujewa ni kitovu cha shughuli za

biashara na Makao Makuu ya Wilaya ya Mbarali na kwa bahati mbaya barabara nyingi za mji huo hazipitiki kutokana na ubovu. Wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2015 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kujenga kilometra tano za barabara kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo kwa wananchi wa Mbarali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri Wilaya ya Mbarali iliidhinishiwa na kupokea shilingi milioni 793.02 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kilomita 20, kalavati kubwa 17 na matengenezo ya madaraja matano. Serikali itafanya kila liwezekanalo ili ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais iweze kutekelezwa ndani ya miaka mitano ya utekelezaji wa llani. Halmashauri imepanga kuweka kipaumbele na kutenga bajeti katika mwaka wa fedha 2018/2019 ili kuanza utekelezaji wa ahadi ya kujenga kilometra tano za barabara kwa kiwango cha lami kwa usimamizi wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (*TARURA*).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana vilevile nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kazi zilizokuwa zinaendelea zilizokuwa zinafanywa na Halmashauri na hizo

zimehamishiwa kwenye *TARURA* sasa hivi. Je, ni lini *TARURA* wataanza na kuendeleza hizo kazi?

Swali la pili, kama ilivyo katika Mji Mdogo wa Rujewa vilevile Mheshimiwa Rais aliahidi kumalizia ujenzi wa kituo cha mabasi cha Mbalizi katika Mji Mdogo wa Mbalizi.

Je, ni lini kazi hiyo ya kujenga kituo cha mabasi cha Mji Mdogo wa Mbalizi kitaanza? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumekuwa na kipindi cha mpito ambapo kazi za ujenzi wa barabara katika Halmashauri zilikuwa zikisimamiwa ndani ya Halmashauri zetu, lakini chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Sasa hivi tumeunda Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini ambao unaitwa *TARURA* sasa umeshaanza kuchukua majukumu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tunafahamu wazi kwamba kulikuwa na mikataba mingine na kazi mbalimbali zilikuwa zinaendelea na tulitoa maelekezo katika ofisi yetu kwamba zile kazi zote kutokana na mikataba iliyokuwa inaendelea ambazo ziliingiliwa na Halmashauri kazi zile zilipaswa kuendelea, isipokuwa taratibu za malipo ndio zilikuwa zinafanyiwa utaratibu maalum. Tulitoa maelekezo haya kwa Mameneja wa *TARURA* katika nchi nzima katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, wakati mwingine kulikuwa na uelewa tofauti katika baadhi ya maeneo, baadhi ya maeneo kazi zilikuwa zinaendelea vizuri lakini sehemu zingine kazi zilisimama, kazi kubwa iliyofanyika ni kuhamisha zile akaunti ziweze kufanya kazi vizuri ili utaratibu uendelee kufanyika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na *concern* yako Mheshimiwa Oran naomba niigize Halmashauri yako Meneja kama kuna changamoto ambayo ameipata katika ofisi yake tuwasiliane na ofisi na hasa na Mtendaji Mkuu wa *TARURA* ampe maelekezo ya kutosha nini kifanyike, ili kazi kule *site* isiendelee kukwama, ziendelee kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la ujenzi wa stendi hii ya Mbarali, naomba nilichukue hili halafu njue kwamba kuna kitu gani kilichokubaliwa na imefikia hatua gani? Changamoto iko wapi? Hili naomba niwahakikishie ofisi yangu itasimamia kwa sababu ahadi ya Mheshimiwa Rais lazima itekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilichukue jambo hili tutaenda kulifanyia kazi haraka iwezekanavyo, kuangalia nini tufanye ili kuhakikisha ile stendi inatengenezwa. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwalongo swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* imepokea kazi hizi za barabara katika Halmashauri zetu, sasa katika masuala haya ya barabara katika Halmashauri tulikuwa tunakarabati barabara hata katikati ya msimu, inaweza ikatokea mvua nyingi ikasomba barabara, Halmashauri ikatoa lori, wananchi wanashiriki kujenga ile barabara.

Je, katika kipindi hiki cha *TARURA*, wataendelea kufanya hiyo Kazi? Kwa sababu sasa *TARURA* haina malori, Halmashauri ina malori haina mafungu ya barabara, lakini *TARURA* wana mafungu hawana malori. Hapa huu utaratibu wa kurekebisha hizi barabara utakuwaje? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo wala kwanza halina mashaka, kwa sababu jukumu hili sasa liko chini ya *TARURA*. Lakini ufahamu siyo Halmashauri yako peke yake, kuna Halmashauri mbalimbali wengine wana greda. Nafahamu magreda haya au malori haya sio kwamba yatakuwa yanafanya kazi peke yake lakini inawezekana ni

kitega uchumi cha kwenu ninyi kama Halmashauri. Wakati *TARURA* inafanya kazi yake, wakati inatekeleza kupitia Meneja wa *TARURA* katika ngazi husika lazima kama utaratibu wa kukodi malori utafanya katika utaratibu ule usiokuwa na kikwazo. Kwa hiyo, kama mna malori yenu, mna magreda yenu ambayo nanyi ni sehemu ya kitega uchumi kwenu barabara zitakapokuwa zinajengwa katika maeneo yale kama mtakuwa na utaratibu wa kukodisha jukumu kubwa ni kwamba *TARURA* itemize wakibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mwalongo naomba usihofu kila kitu kitaenda vizuri, ni kipindi cha mpito tu kina mashaka kwa sababu ni jambo jipya lakini jambo hili litakuwa halina matatizo ya aina yoyote, tutafika muda mtaona kila kinaenda vizuri katika Halmashauri zetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pascal Haonga swalii la nyongeza.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la miundombinu ya barabara katika Mji Mdogo wa Rujewa linafanana kabisa na ubovu wa miundombinu ya barabara katika Mji Mdogo wa Mloo, Jimbo la Mbozi.

Je, nini ahadi ya Mheshimiwa Waziri kwa wananchi wa Mloo kuhusu miundombinu mibovu ya barabara ambayo ni tatizo la muda mrefu sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Haonga unapozungumza suala la Mloo nafahamu kwamba changamoto kubwa ya Wabunge wengi humu ni suala zima la miundombinu ya barabara katika Halmashauri zetu. Ndiyo maana nawashukuru sana katika Mpango ule wa bajeti mwaka huu mmeona tumetenga bajeti kubwa karibuni ya shilingi bilioni 263. Lengo kubwa ni kwamba barabara za vijijini zenye vikwazo na zile barabara nyingine tuweze kuzihudumia.

Kwa hiyo, naomba niseme kwamba katika eneo la kwako ulilozungumza na kwa sababu tumeshawaajiri watu tena tunawapa *performance contract* ya jinsi gani kila meneja katika Halmashauri anapoenda kule afanye kazi yake na tutaipima na meneja atakaposhindwa ku-deliver maana yake hatokuwa na hiyo nafasi atapewa mtu mwagine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ondoa hofu ni kwamba tutakuwa katika mkakati wa kutofanya kazi tena kimazoea katika utaratibu wa sasa, na kwa sababu jambo hili liliahidiwa katika llani ya Chama cha Mapinduzi lazima tuwe na *TARURA* tutaenda kutekeleza kwa nguvu zote, naomba ondoa hofu katika eneo la Mloo tutalifanya kazi haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mipata swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais alitembelea Namanyere na akatoa ahadi kwamba akipita tutapata kilometa tano za barabara ya lami. Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo amekuwa akilisema mara kwa mara lakini mpaka sasa halijatekelezwa.

Nataka kujua Serikali ina mpango gani kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na hata nilipotembelea Namanyere Mheshimiwa Keissy alizungumza katika mukutano nilipokuwa ninaongea na Watumishi kuhusu ahadi hiyo sambamba na ahadi ya maji ambapo bwawa lilikuwa linaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mipata kwa sababu nafahamu pale Namanyere ndiyo Makao yenu Makuu ya Mji kwa ahadi hii ya Serikali na sisi ametupa dhamana kuhudumu katika ofisi yake,

tutafanya kila liwezekanalo katika kipindi hiki cha miaka mitano, ahadi ya Mheshimiwa Rais kupitia *TARURA* tutaitokeleza, tutakapofika mwaka 2020 tusiwe na changamoto nyingine yoyote katika suala la hiyo kilometa tano Mheshimiwa Rais alizoziahidi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba sasa aulize swali lake.

Na. 55

**Kuhusu Ukoefu wa Ardhi ya Kilimo Kijiji cha Ngadinda Madaba**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA** aliuliza:-

Zaidi ya wananchi 181 wa kijiji cha Ngadinda Halmashauri ya Madaba wanalima ndani ya Wilaya ya Namtumbo kwa sababu ya kukosa eneo katika kijiji chao. Baraza la Madiwani lilihauri sehemu ya shamba la hekta 6,000 la Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi liliopo ndani ya kijiji hicho ambalo lilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ili litumike kwa shughuli za kilimo na sehemu ibaki kwa ajili ya mifugo. Hivi sasa wafugaji toka maeneo mbalimbali nchini wapo katika shamba hilo lakini wakulima hawajatengewa eneo.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kitendo hicho ni ubaguzi na kinaweza kuchochaea migogoro kati ya wafugaji na wakulima?

(b) Je, ni lini Serikali itasikiliza kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Ngadinda cha kutengewa eneo la kilimo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali a

Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Songea mwaka 2014 iliunda Tume ya kuchunguza matumizi ya shamba hilo ambalo lilikuwa linamilikiwa na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvubi na kubaini kuwa shamba hilo halitumiki vizuri kwa shughuli za ufugaji. Kwa msingi huo Tume ilipendekeza hekta 4000 wapewe wananchi wa Kijiji cha Ngadinda na eneo linalobaki la hekta 2000 libaki kwa shughuli za uwekezaji na ufugaji. Hata hivyo, baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Wilaya ya Songea kugawanywa na kupata Halmashauri mpya ya Wilaya ya Mababa uamuzi huo haukutekelezwa. Hivyo, Halmashauri ya Madaba inatakiwa kujadili suala hili katika vikao vya Halmashauri na kufanya uamuzi kuhusu matumizi ya shamba hilo kwa kuzingatia maslahi ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa katika sehemu (a) ya jibula msingi, Halmashauri ndiyo yenyen jukumu la kujadili na kukubaliana kuhusu matumizi ya shamba hilo lililokuwa linatumika kwa shughuli za ufugaji. Serikali itatoa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha maslahi ya wakulima na wafugaji yanazingatiwa kuhusu matumizi ya shamba hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafsi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile vikao halali vya Halmashauri ya Wilaya ya Songea vilishamaliza jukumu la kihalmashauri kuhusu matumizi ya eneo hili la ardhi; na kwa vile katika mazungumzo na ufuutiliaji Wizara ya Kilimo walishaelekeza kwamba sasa Mkoa ukabidhi sehemu ya eneo la shamba hilo kwa wananchi ili waweze kuendelea na shughuli za kilimo; na kwa vile msimu wa kilimo umekaribia sana na wananchi hawana sehemu ya kulima

mazao ya chakula, na kwa vile wafugaji tayari wameanza kufuga katika eneo hilo.

Je, Serikali ipo tayari sasa kutoa maelekezo kwa Serikali ya Mkoa kuhusu kutekeleza jukumu hili haraka iwezekanavyo?

Pili, iwapo zoezi hili litaendelea kucheleta kutekelezwa, je, Serikali ipo radhi sasa kuruhusu wananchi wa Ngadinda na kwa vile mipaka inafahamika, kuiagiza Serikali ya kijiji iweze kuanza kushirikiana na wananchi kuwatengea maeneo hayo waweze kuanza kuzalisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa hizo *initiative* zote walizozifanya mpaka wamefikia hapo. Mimi nafahamu kwamba kama hatua nyingi za msingi zimeshafanyika kikubwa zaidi ni sehemu yetu ya Mkoa. Nichukue fursa hii kuiagiza Ofisi ya Mkoa wa Ruvuma iangalie jinsi gani ya kufanya kama mijadala yote imeshakamilika iende haraka kurekebisha jambo hili ili wakulima na wafugaji tusiwe na mgogoro tena katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua wazi kwamba jambo hili likiwa na ukakasi wake mwisho wa siku tunakuja kuzalisha matatizo makubwa sana ya uvunjivu wa amani. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuiagiza timu ya Mkoa wetu wa Ruvuma iende ikalifanyie kazi jambo hilo haraka iwezekanavyo na ikiwezekana mpaka mwezi wa Kumi jambo hilo liwe limekamilika na ofisi yetu ya TAMISEMI tupate taarifa ya jinsi gani jambo hilo limekamilishwa kwa sababu vikao vyote halali kwa taarifa niliyoipata kutoka kwa Mbunge zimeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili kwamba kukiruhusu kijiji kwenda kuhakikisha kwamba wanaenda

kugawa hilo eneo, naomba tuvute subira kwanza, timu ya Mkoa ifanye kazi yake vizuri baadaye tukishapata taarifa tutajua nini kifanyike. Lengo kubwa kama unavyowapigania wananchi wako Serikali itaingilia kati kwa nguvu zote sisi tukishirikiana na Wizara ya Kilimo tutafanya kila liwezekanalо eneo lile liwe katika utaratibu mzuri, wananchi wa eneo lile wawzeze kupata ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ondoa hofu Mheshimiwa Mbunge tunalifanya kazi jambo hili. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wananchi wa Madaba wameonesha kuhamasika sana kulima tangawizi, hata mimi ninalima tangawizi Madaba. Je, Serikali haioni kwamba kiwanda cha Mamba Miamba ambacho kitakuwa tayari *by March next year*, kitahitaji tangawizi nydingi sana siyo kutoka Same tu pamoja na Madaba.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia wananchi wa Madaba ardhi ya uhakika ili walime tangawizi kwa wingi? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuchukue kilio cha mama vilevile kama kilio cha Mheshimiwa Joseph Mhagama. Serikali inaona umuhimu huo na tutafanya kila liwezekanalо kuhakikisha mambo pale yanakaa sawasawa wananchi walime tangawizi waje, kulisha katika kiwanda cha Mama Anne Kilango Malecela. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa fursa hii.

Tatizo la mgogoro wa shamba la Madaba linafanana sana na tatizo la shamba la Kigomani na Utumaini lillipo Wilayani Mafia.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuja Mafia kukaa na wadau wa Halmashauri pamoja na Viongozi wengine kutatua tatizo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge na lile deni letu tumeshatoa shilingi milioni 50 tumemaliza kituo cha afya, hongera sana Mheshimiwa Mbunge kwa ujenzi wa *theatre*. Hata hivyo, katika jambo hili mimi naomba nilichukue, lakini kabla mimi sijaja kule nimuagize Mkuu wa Wilaya ya Mafia kwanza aende akalishughulikie jambo hili na ikiwezekana tupate taarifa amelishughulikia vipi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakapopata hiyo taarifa jinsi gani limeshughulikiwa jambo hili na mgogoro huo haukuisha, na mimi nitaona jinsi gani ya kufanya, lakini kwamba nitatumia vyombo vyangu vya chini kule kwanza, Mkuu wa Wilaya ya Mafia aanze kuifanya kazi hiyo harka iwezekanavyo kumaliza hilo tatizo na ofisi yetu ipate taarifa ndani ya mwezi mmoja, jinsi gani mgogoro huo umeshughulikiwa kwa kadiri iwezekanavyo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, sasa aulize swalilake.

Na. 56

### **Kushuka kwa Thamani ya Shilingi ya Tanzania**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kumetokana na kuruhusu kutoza bidhaa mbalimbali na huduma kwa dola na kuathiri thamani ya fedha yetu.

Je, Serikali inachukua hatua gani za kuimarisha shilingi yetu na kupiga marufuku matumizi ya fedha za kigeni nchini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kushuka au kupanda kwa thamani ya shilingi hakutokani na kuruhusu bidhaa mbalimbali na huduma kutozwa kwa dola, bali hutokana na misingi ya shughuli mbalimbali za kiuchumi (*Micro Economic Fundamentals*) na hali halisi ya uchumi wa nchi tunazofanyanazo biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kushuka au kupanda kwa thamani ya shilingi kunaweza kusababishwa na mambo makuu yafuatayo:-

(i) Nakisi ya urari wa biashara; nakisi ya urari wa biashara ya nje ya nchi (*balance of payments*) husababisha sarafu kushuka thamani kama mauzo ya bidhaa nje ya nchi ni madogo ikilinganishwa na ununuzi wa bidhaa kutoka nje. hali hiyo, hufanya thamani ya shilingi kushuka kwa sababu mahitaji yetu ya fedha za kigeni ni makubwa kuliko mapato ya mauzo yetu nje ya nchi.

(ii) Mfumuko wa bei; pamoja na mambo mengine

mfumuko wa bei husababishwa na ongezeko kubwa la ujazo wa fedha kuliko uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali katika nchi. Aidha, thamani ya fedha hupungua iwapo mfumuko wa bei wa ndani ni mkubwa kuliko mfumuko wa bei katika nchi tunazofanyanazo biashara ni za nje ya nchi.

(iii) Tofauti ya misimu (*seasonal factors*); upatikanaji wa fedha za kigeni kutoptaka na biashara za msimu husababisha kusesereka au kutoserereka kwa shilingi ya Tanzania. Kwa mfano, mapato mengi ya fedha za kigeni kutikana na biashara ya nje huongezeka wakati wa nusu ya pili ya kila mwaka yaani kati ya Julai na Disemba, ikiwa ni kipindi cha mavuno na kilele cha utalii hivyo, thamani ya shilingi huimarika au kuwa na utulivu zaidi katika kipindi kati ya Julai na Disemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa pamoja na kuwepo kwa sheria ya kutotumia kabisa fedha za kigeni nchini Afrika ya Kusini, lakini sarafu ya nchi hiyo imapatwa na misukosuko mikubwa zaidi ya shilingi ya Tanzania. Hata thamani ya sarafu nydingine kubwa duniani kama vile Yen ya Japan, Renminbi ya China na Euro zimekuwa zikiyumba kwa kasi zaidi ya shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha thamani ya shilingi Benki Kuu inaendelea kudhibiti mfumuko wa bei, ili usitofautiane sana na wabia wetu wa biashara. Pia Benki Kuu imedhibiti biashara ya maoteo (*speculation*) katika soko la fedha za kigeni, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa miamala ya fedha za kigeni inayofanywa na benki kwa ajili ya shughuli za kiuchumi tu na sio biashara ya maoteo. Hali hii itasaidia upatikanaji wa fedha za kigeni katika soko la rejareja na hivyo kupunguza shinikizo la kuperomoka kwa thamani ya shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema ikaelewaka kuwa pamoja na hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Benki Kuu, ufumbuzi wa kudumu wa kutengemaa kwa thamani ya shilingi hutegemea zaidi kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma

na uhamisho wa mali nchi za nje. Hii itawezekana tu endapo tutaongeza uzalishaji na kuwa na ziada ya kuongeza mauzo yetu nje ya nchi na pia kupunguza uagizaji wa bidhaa na huduma zisizo za msingi kutoka nje.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, mpaka sasa hivi kuna baadhi ya makampuni ya watu binafsi na wafanyabiashara wanaendelea kutoza na kupanga bei kwa kutumia dola badala ya *Tanzanian shillings*.

Je, Serikali haioni hiyo inaidhalilisha shilingi yetu na kuonesha kwamba, hawana imani na shilingi ya Tanzania?

Swali la pili, kwa kuwa moja ya eneo ambalo linatumia fedha nydingi sana na kusababisha kutokuwepo kwa urari mzuri wa nchi ni uagizaji wa vyakula mbalimbali kutoka nje ya nchi wakati vyakula hivyo vinaweza kuzalishwa ndani ya nchi, maeneo kama mafuta ya kula, sukari na mazao mengine ambayo yanaweza kuzalishwa hapa nchini. Kwa mwaka tunatumia zaidi ya shilingi trillioni 2.8 kwa ajili ya kuagiza mazao yanayotokana na vyakula vinavyoweza kuzalishwa hapa na kutoa ajira kwa wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuzuia uagizaji wa baadhi ya vyakula kutoka nje ya nchi ili kuinua ualishaji wa ndani ya nchi na kuokoa shilingi? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa NaibU Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza kwamba katika watu ambaao wanaweka bei kwa kutumia dola wanaidhalilisha

shilingi yetu, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tulipitisha sheria katika Bunge lako Tukufu kwamba siyo kosa kuweza kuweka bei kwa *currencyambayo* siyo ya Tanzania, kosa ni ni kukataa pesa shilingi ya Tanzania pale ambapo mteja anataka kulipa na yule mwenye duka akakataa kupokea hilo ndio kosa, lakini siyo kosa katika kuweka bei hiyo kwa *currencyambayo* sio shilingi yetu ya Tanzania, kama Taifa tuliona inafaa na ndiyo maana tunaendelea kutekeleza sheria hii tuliopitisha mwaka 1992.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuzuia *ku-import* bidhaa ambazo zinazalishwa hapa nchini. Napenda kulijibu Bunge lako Tukufu kwamba, ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Tano inasisitiza kwamba uchumi wa viwanda ili tuweze kuzalisha bidhaa zetu za kutosheleza ndani ya nchi yetu. Tutakapokuwa tumeweza kuzalisha bidhaa hizi kwa kiwango ambacho kinatosheleza hatuna sababu ya kuendelea *ku-import* na tutaweza kurekebisha sheria zetu ili tuweze sasa kutumia bidhaa zetu, lakini kusema sasa tupige marufuku wakati bado kuna uhitaji wa bidhaa hizi, haitakuwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kuiunga mkono Serikali yetu katika kuiendea Tanzania ya Viwanda, tuna uhakika ndani ya miaka mitano mpaka kumi tutakuwa tumeweza kujitosheleza kwa bidhaa zetu ndani ya Tanzania. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kangi Lugola, swalii la nyongeza.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwa kinywa chake katika majibu yake ya msingi kwamba, kushuka au kupanda kwa thamani ya shilingi yetu hakuna uhusiano na utozaji wa bidhaa au huduma kwa dola.

Je, anataka kuwaaminisha wachumi wote Tanzania na duniani kote na Bunge hili kwamba hata miaka mitano

tukiamua kutumia dola tu bila kutumia shilingi na baadaye tukairejea baada ya miaka mitano tutakuta uchumi wetu haujaathirika na wala shilingi yetu haijaathirika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, si kuwaaminisha Wachumi, kama nilivyosema nimeeleza sababu ya kushuka kwa thamani ya *currency* yoyote ile hata kama sio shilingi ya Tanzania. Kuweka *quotation* kwa bei ambayo siyo shilingi ya Tanzania si sababu mahsususi, lakini naomba kumwambia Mheshimiwa Kangi Lugola kwamba ni asilimia 0.1 tu ya watu ambao wanaweka *quotation* kwa bei ambayo sio shilingi ya Tanzania ambao wako tayari kupokea fedha hii kwa kutumia *currency* ile waliyo-quote. Zaldi ya asilimia 99.9 ya Watanzania na wafanyabiashara wanaoweka *quotation* kwa pesa ambayo sio *T-Shillings* wako tayari kupokea bei yao na kuza bidhaa zao na kupokea shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kangi Lugola kama nilivyosema ziko *indicators*. Viko viashiria mbalimbali vinavyosababisha kushuka kwa uchumi na hatuna sababu ya kusema kwamba tuweze kuweka miaka mitano tufanye *quotation* na tusitumie shilingi yetu ya Tanzania. Nimesema kupitia Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006, Kifungu cha 26 ni shilingi ya Tanzania ndiyo *legal tender document* ambayo inaruhusiwa ndani ya Taifa letu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninauliza swali moja la nyongeza.

Kutokana na ripoti ya *BOT latest* ya mwezi Juni, inaonesha kwamba *export volume* yetu imeshuka kutoka dola milioni 4.5 mpaka dola milioni 3.8 wakati huo huo *prices*

za *commodities* kwenye soko la dunia imeendelea kushuka na *import volume* yetu ya *capital goods*imeendelea kushuka.

Je, Serikali ina mpango gani kutokana na *variables* hizi zote nilizozitaja kuhakikisha kwamba, miezi mitatu mpaka sita ijayo *stability* ya shilingi yetu inaendelea kuwa imara kwa sababu *indications* zote zinaonesha kwamba, shilingi yetu inaendelea kushuka kila siku kutokana na hali ya uchumi na uzalishaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo amesema ni kweli kwamba *export volume* yetu imeshuka, na mimi katika jibu langu la msingi nimesema katika miezi ambayo Taifa letu huwa linapanda katika *exportation* ni kuanzia Julai mpaka Disemba na ndio kipindi hiki. Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Bashe kwamba ndani ya kipindi hiki kwa sababu ndio tunazalisha na tunavuna *export* yetu itapanda muda siyo mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimesema kwenye jibu langu la msingi kwamba tuendelee kuiunga dhamira ya Serikali yetu, Tanzania ya Viwanda ndiyo itakayotuwезеша kuongeza *export volume* yetu na kuweza kupunguza *importation* ya bidhaa ambazo tutazalisha ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuendelee kumuunga Mheshimiwa Rais wetu katika dhamira yake hii na sisi kama wasaidizi wake tuko imara katika kumsaidia kuhakikisha kwamba, thamani ya shilingi yetu inaendelea kuimarika na *export volume* kulingana na viwanda ambavyo tayari sasa vimeanza kufanya kazi, itaongezeka muda siyo mrefu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nilitaka nimpe Taarifa tu Mheshimiwa Hussein Bashe kwamba, katika *record* za hivi karibuni nchi yetu ina *reserve* nyingi na ina *over five months of imports* kutokana na *credibility* ya *Government Policy*. Kwa maana hiyo, kushuka kwa *imports* wala hakujaathiri sana matarajio ya kuharibika kwa ustahimilivu wa mfumuko wa bei kutokana na kwamba, Serikali ina *reserve* nyingi za kutosha na kwa maana hiyo *export* zitakapokuwa zimeongezeka zitakutana na *reserve* za kutosha ambazo hazitaleta uharibifu wowote kwenye mbadilishano wa fedha pamoja na mfumuko wa bei. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo, Mbunge wa Same Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 57

#### **Kuongeza Ukwasi Kwenye Benki kwa Wananchi**

**MHE. MATHAYO D. MATHAYO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuongeza ukwasi katika benki na kwa wananchi wa kawaida ili washirikiane na Serikali katika kujenga uchumi wa mtu mmoja mmoja, kaya na taifa kwa ujumla?

#### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathayo David Mathayo, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo ya Serikali ya kuimarisha uchumi na kudumisha utulivu wa mfumuko wa bei, Benki Kuu hutekeleza Sera ya Fedha inayolenga kudhibiti ukwasi ili uendane na mahitaji halisi ya uchumi. Kati

ya Julai, 2016 na Julai, 2017 kiwango cha ukiasi katika mabenki kwa ujumla wake kiliongezeka kutoka asilimia 35.53 hadi asilimia 38.41 kwa mtiririko huo. Kiwango cha ukiasi wa asilimia 38.41 ni kizuri zaidi katika uchumi ikilinganishwa na kiwango cha chini cha asilimia 20 kinachotakiwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarika kwa ukiasi kwa mwaka 2017 kunatokana na hatua mbalimbali za kisera zinazochukuliwa na Benki Kuu. Miongoni mwa hatua hizo ni kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki, kununua fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni (*Interbank Foreign Exchange Market*) na kushusha riba inayotozwa kwa benki za biashara na Serikali wanapokopa Benki Kuu kutoka asilimia 16 hadi asilimia 12 mwezi Machi, 2017 na kutoka asilimia 12 hadi asilimia tisa mwezi Agosti, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine iliyochukuliwa na Benki Kuu ni pamoja na kushusha kiwango cha sehemu ya amana ambayo mabenki yanatakiwa kuhifadhi Benki Kuu kutoka asilimia 10 hadi asilimia Nane (8) kuanzia mwezi Aprili, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Benki Kuu, hali ya ukiasi katika sekta ya fedha, hususan benki ni nzuri na hakuna viharishi vyta kuleta madhara hasi katika uchumi wetu. Aidha, Benki Kuu itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha masoko ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kwamba, yanaendeshwa kwa ufanisi na ushindani na hivyo kusaidia kuongeza ukiasi miongoni mwa mabenki na taasisi nyingine za kifedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mathayo Mathayo swali la nyongeza.

**MHE. MATHAYO D. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.

Aidha, napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa kujibu maswali yake vizuri na kitaalam. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Benki Kuu imepunguza riba ya mabenki ya biashara yanapokopa kutoka kwenye Benki Kuu hadi kufikia asilimia tisa na kwa kuwa pia, imepunguza amana kutoka asilimia kumi hadi asilimia nane ya kiwango cha fedha ambazo mabenki haya ya biashara yanatakiwa yahifadhi Benki Kuu. Je, Benki Kuu imefuatilia na kuona kwamba, mabenki ya biashara yanatoza riba nzuri au yametoa pungozo zuri la riba kwa wananchi ambao wanakopa kwenye mabenki hayo?

Swali la pili, kwa kuwa katika nchi zinazoendelea asilimia 70 ya fedha zinakuwa mikononi mwa wananchi na asilimia 30 inakuwa kwenye mabenki pamoja na Serikali. Je, Benki Kuu imefanya utafiti na kuona, kwa sababu sasa hivi tukiangalia fedha katika mzunguko kwa wananchi wa kawaida zimepungua sana.

Je, Benki Kuu imefanya utafiti na kujua kwamba, fedha hizi ziko wapi ili waweze kutunga Sera ambazo zitarudisha fedha hizi kwenye mabenki ya biashara pamoja na wananchi ili maisha yaweze kuwa mazuri, lakini wananchi pia washiriki vizuri katika shughuli za kujenga nchi yao? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumeshusha kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi na kwa sasa tunafanya ufuatiliaji kuona kwamba, riba zinazotozwa na benki zetu za biashara pamoja na taasisi za kifedha zinashuka *ku-respond* katika jitihada hizi ambazo zimefanywa na Serikali kupitia Benki Kuu. Tutakapomaliza ufuatiliaji huu na sasa hivi tuko katika vikao mbalimbali na mabenki haya kuona ni jinsi gani sasa wanawea kurejesha riba chini ili wananchi wetu waweze kukopa, tutaleta taarifa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, napenda kumwambia Mheshimiwa Mathayo kuwa ni sahihi kwamba asilimia 30 tu ya pesa ndiyo iko benki, asilimia 70 iko kwa wananchi. Kinachoonekana kwa sasa ni kwamba Serikali tumeimarisha mfumo wetu wa ukusanyaji wa kodi. Yule mfanyakibashara aliyejewa akifanya biashara bila kulipa kodi akijidanganya ile ni faida yake, sivyo ilivyo kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono tuweze kukusanya kodi inavyostahiki na ili Watanzania sasa tuishi katika uchumi ambao Taifa letu na wananchi wanastahili kuishi. Kiuhalisia fedha bado iko ya kutosha katika mikono ya wananchi kama alivyokiri yeye Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali kwamba asilimia sabini ya pesa yetu iko kwa wananchi na uchumi wetu unaendelea vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, aah, sikuwaona mmesimama mwanzo naona sasa hivi mmesimama wote kwa kasi. Mheshimiwa Mwakajoka, swali la nyongeza.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kumekuwa na tafsiri ambayo siyo sahihi sana kwa vijana ambao wanunuwa Kwacha kwenye mpaka wa Tunduma na Zambia ambapo fedha hizo, Wazambia wanapokuwa wamekuja kununua bidhaa kwenye Mji wa Tunduma wanakuja na Kwacha na baadaye vijana wanunuwa zile Kwacha na Serikali imekuwa ikisema kwamba vijana wale hawalipi kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kununua zile Kwacha, wanakwenda Lusaka kununua dola na baada ya kununua zile dola wanakuja ku-*change* kwenye benki zetu za Tanzania. Hawa wafanyakibashara wa Kwacha wanakuwa tayari wamelipa kodi.

Je, Serikali haioni kwamba nao pia ni walipa kodi katika Taifa hili na badala yake wanaendelea kuwasumbua? Wataacha lini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naona upo tayari kujibu japokuwa swali siyo la nyongeza hilo, naona ni swali la msingi, tofauti kabisa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipaka ambayo kuna *black market* ya kutisha ndani ya Taifa letu ni mpaka alioutaja wa Tunduma na ndio maana wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri wa Fedha alikuwa mpakani kule na sasa tumeimarisha na tutahakikisha Mheshimiwa Mwakajoka tunakusanya kodi yote. Hawawezi kutoa Kwacha huku wakaenda kuibadilisha na wakarudi nchini bila kukusanya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeapa kulinda na kuweza kukusanya kodi yetu, tutakusanya kodi hii kwa kila mtu anayefanya biashara hili. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa uhusiano wa benki na mtu wa kawaida ambaye hafanyi biashara, ni kuweka hela yake ili apate faida na pia kwa usalama; na sasa hivi tunashuhudia kwamba hata mitandao ya simu mtu unaweza ukawekeza hela yako. Ni lini sasa benki hizi zitakaa chini na kuona kwamba kuna umuhimu wa kuongeza faida (*Interest rate*) kwa wale wanaoweka hela zao kwenye *savings account?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimekuwa nikisema tangu mwaka 1991 nchi yetu iliingia katika soko huru katika masuala ya kifedha nchini na *interests* zinazopangwa na mabenki yetu katika *savings account* huwa zinawekwa kulingana na uhalisia wa soko. Ina maana faida inapatikana kwa mabenki na kwa wananchi. Kwa kumbukumbu ambazo tunazo Wizara ya

Fedha na Mipango, *interest* hii imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe angalizo kwa mabenki yetu kuangalia kwamba wana *balance interest* wanayotoza waone *interest* wanayowapa wananchi kwa kuweka pesa hizi katika akaunti zao hasa *savings account*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika katika hili mabenki yetu yanafanya kazi vizuri kuhakikisha wao wanapata na wateja wao ambao ni wananchi wanapata vizuri kwa kuwa tupo katika soko huria na wanapambana kuweza kupata wateja kuweka pesa katika benki zao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 58

### **Uuzwaji wa Silaha Kiholela Nchini**

#### **MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Kumekuwa na uuzwaji wa silaha kiholela kama vile mapanga na visu katika barabara zetu ikiwemo Ubungo kwenye mataa hali ambayo inaleta hofu kwa raia wema.

Je, Serikali inalichukuliaje suala hilo ambalo ni hatari sana kwa usalama wa raia?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwepo na uuzaaji holela wa silaha za jadi katika maeneo mbalimbali ya barabara zetu ikiwemo katika makutano ya barabara ya Mandela na Morogoro eneo la Ubungo, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inatambua uwepo wa tatizo hilo na tayari hatua mbalimbali za kudhibiti hali hiyo zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya operesheni za mara kwa mara na kukamata wauzaji wa silaha za jadi barabarani kama vile mapanga, mikuki, upinde na mishale. Aidha, elimu inaendelea kutolewa kwa wafanyabiashara wa bidhaa za silaha hizo kutowapatia wauzaji wasio na eneo maalum la kufanya biashara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali linaanda utaratibu maalum wa uuzaaji wa bidhaa za aina hii na kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya biashara hii na kuwashauri wananchi waipige vita na kuepuka kujihusisha nayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Msabaha, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kumuuliza Naibu Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imekuwa kisiwa cha amani, lakini kuna genge la wahuni ambalo hatujui wanapata wapi silaha za kijeshi na kushambulia raia wasiokuwa na hatia.

Je, Serikali haioni sasa imefika wakati muafaka kufanya doria katika sehemu zote za mipaka na barabarani na hata katika vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha genge hili halina nguvu kwa sababu linachafua taswira ya Tanzania katika medali za kitaifa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa bado silaha hizi zinaendelea kuuzwa sehemu za starehe kama vile minadani na sehemu mbalimbali na kuhatarisha amani ya ambao wanafika katika kupata huduma katika sehemu hizo.

Je, Serikali ina mikakati gani ya ziada kuhakikisha suala hili kuuza silaha holela linakomeshwa na wale wanaokamatwa wachukuliwe sheria kali ili suala hili likome mara moja? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni bahati mbaya sana Mheshimiwa Mbunge hajalitaja jina la kundi ambalo amelizungumza, lakini kimsingi nataka nimueleze tu kwa ufupi kwamba hali ya matumizi ya silaha kufanya uhalifu nchini imepungua, ndio maana hata ukiangalia takwimu tokea Juni, 2016 mpaka Agosti, 2017, hakuna matukio makubwa ya mauaji ya kutumia silaha za jadi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utaona ni kazi kubwa ambayo Serikali imefanya kupitia Jeshi la Polisi kuweza kudhibiti wahalifu na magenge mbalimbali ambayo yamekuwa yaktumia silaha hizo za jadi kwa ajili ya kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba mafaniko hayo yamepatikana kwa sababu gani? Kuna mikakati mingi ambayo imefanyika ili kuweza kufikia malengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumeendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusiana na makundi ambayo yamekuwa yakijitokeza, kwa mfano, maeneo ya Kanda ya Ziwa kuna watu walikuwa wanaitwa wakata mapanga, ukija huku Mbeya na kadhalika, wapo watu ambao walikuwa wanafanya mauaji kwa vikongwe kwa imani za kishirikina. Kwa hiyo, Jeshi la Polisi kwa kupitia utaratibu wake wa ulinzi shirikishi tumekuwa tukifanya jitihada kubwa sana za kutoa

elimu kwa jamii ili kufahamu madhara ya matumizi ya silaha za jadi, hasa matumizi ya kujichukulia sheria mkononi kwa jamii, hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilingine, tumekuwa tukiendelea kufanya doria na ukaguzi barabarani kuweza kusimamisha magari na watu ambao wakipita na silaha hizo za jadi na kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria. Hii doria imekuwa ikiendelea na ndiyo maana mpaka sasa hivi tumeweza kufanikiwa kwa mujibu wa takwimu ambazo nimezieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeendelea kuhakikisha kwamba huduma zetu za Jeshi la Polisi zinashuka katika ngazi ya Tarafa na Kata. Tuna Ofisi za Ukaguzi katika ngazi ya Tarafa na Kata ili kusogeza huduma ya Polisi karibu na wananchi kuweza kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu ya aina kama hii ambayo Mheshimiwa Mbunge amezungumza. Kwa hiyo, nikiri tu kwamba kwa jumla kazi kubwa imefanyika na mafanikio yake mpaka sasa hivi ndiyo haya ambayo nimeyaeleza, ni makubwa ya kuridhisha kwa kiasi fulani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf, swali fupi.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Watanzania wengi ni wakulima, wafugaji na wavuvi. Kwa mantiki hiyo, kisu na panga ni kitendea kazi muhimu na adhimu kwa kukamilisha kazi zao. Kama ni *misuse*, hata tai inaweza kutoa maisha ya mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini tafsiri sahihi ya neno silaha? Naomba majibu.

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya silaha tunaitafsiri kufuatana na mazingira

inapotumika. Kama mtu amebeba fimbo na anachunga, tunaelewa kwamba mazingira ya anakochunga anastahili kuwa na fimbo hiyo. Leo hii kama mtu anaingia Bungeni na amebeba kisu, ile inageuka kuwa silaha ambayo iko katika matumizi ambapo haitakiwi kuwa na huyo mtu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo, kama mtu anaenda kuangalia mpira (*Ndondo Cup*), hata kama kwenye utamaduni wake anatakiwa kuwa na mkuki, hatutarajii aende nao kwenye uwanja wa michezo, tunatarajia aende nao anakochunga ambako anaweza akakutana labda na wanyama wakali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, hata uholela tunaounglelea kama ambavyo silaha zote zina utaratibu wa maeneo ambapo zinatakiwa kuuzwa, tunatarajia pia hata kwenye matumizi ziwe katika mazingira yanapotakiwa kutumika. Hatuwezi tukaruhusu Watanzania kila mmoja akawa anatembea na silaha popote anapojsikia kuwa nayo kwa sababu udhibiti wake utakuwa ni hatari kwa namna ya kuweza kuhakikisha wale wasiopenda au wasio na silaha wanaweza wakapata athari popote pale ambapo mwenye silaha anaweza akaamua kuitumia. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, swalilake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza.

Na. 59

### **Mamlaka ya Mji – Ngara**

**MHE. ALEX R. GASHAZA (K.n.y. MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA)** aliuliza:-

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kuna matatizo makubwa sana ya maji kiasi kwamba wananchi wa maeneo hayo wanaona kuwa kupata maji ya bomba ni kama ndoto isiyowezekana na wamekuwa wakilipishwa ghamama ya maji

hata kwa wateja ambao hawapati kabisa huduma ya maji kwa kipindi cha mwezi husika ikiambatana na shilingi 1,500 kila mwezi kwa ajili ya mita ya maji.

(a) Je, Serikali inakubaliana na tozo ya shilingi 1,500 ya lazima kwa malipo ya mita?

(b) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wanaotozwa bili za maji wakiwa hawajapata huduma ya maji?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uendeshaji wa mamlaka na utoaji bora wa huduma ya maji, tozo ya shilingi 1,500 ilipitishwa na *EWURA* mwaka 2011 kwa mchanganuo ufuataao:-

(i) Shilingi 500 *service charge*; na

(ii) Shilingi 1,000 *meter rent*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo hii iliendana na bei ya maji inayotumika hadi sasa. Kutokana na *tariffs* mpya za *EWURA* ambazo zimeondoa tozo hiyo kwa sasa Mamlaka ya Maji Mjini Ngara inaandaa andiko la mpango wa biashara (*business plan*) litakalowasilishwa *EWURA* kwa ajili ya mapitio ya bili hiyo na kupata bili mpya ya maji inayoendana na wakati uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na malalamiko yaliyopo kuhusu baadhi ya wananchi kupelekewa ankara wakati hawapati huduma ya maji, Wizara itafutilia kwa kina kujua kama ni kweli tatizo hilo lipo na endapo itabainika hatua stahiki zitachukuliwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alex Gashaza, swali la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Sambamba na hilo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na miradi ya vijiji kumi ambayo imechukua muda mrefu bila kukamilika. Kwa mfano, mradi wa Kijiji cha Mbuba, Munjegwe, Kanazi, Kabarenzi na Mkibogoye, je, ni lini miradi hii itakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwamba tumepata shilingi milioni 24 kwa ajili ya pampu ya K9, lakini kwa namna ya kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 20 alipokuwa Ngara alitupatia shilingi milioni 13 kwa ajili ya kununua pampu ya maji ili kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Ngara. Imeshafungwa na maboresho yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na ahadi yake ni pamoja na kuanzisha mradi ambao unaweza ukawa suluhisho kwa Vijiji vyote vya Wilaya ya Ngara na Wilaya ya jirani kwa kutumia mradi wa vyanzo vya maji, Mto Kagera, Mto Luvubu na Mlima Shunga na akaahidi kwamba ataagiza Waziri na watendaji kufika kwa ajili ya kuangalia namna ya kufanya usanifu wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Waziri na timu yake ya wataalam yupo tayari baada ya Bunge hili kuambatana nami kwenda Ngara ili kuona uwezekano wa kusanifu mradi huu ambao utakuwa ni suluhisho kwa vijiji vyote vya Wilaya ya Ngara na Wilaya jirani? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia huduma ya maji katika Wilaya yake ya Ngara na hasa Mji wa Ngara ambapo Mheshimiwa Rais alipatembelea na akaweza kutoa fedha za kutengneza pampu ili wananchi wa pale wawewe kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maswali yake ya nyongeza, Mheshimiwa Mbunge ameulizia baadhi ya Vijiji ambavyo anasema havijakamilika. Nitoe tu taarifa kwamba Serikali imetenga shilingi 1,500,000,000 katika bajeti yake ya mwaka 2017/2018 kwa maana ya kuendelea kukamilisha miradi hiyo inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kama nipo tayari kwenda naye Ngara, mimi nipo tayari na nimepanga baada ya Bunge hili nitakwenda Ngara kuangalia huduma ya maji katika Mkoa mzima wa Kagera. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Natambua kwamba tatizo la uhaba wa maji linawakumba sana wanawake wote Tanzania. Nilikuwa naomba Mheshimiwa atusaidie hasa kwenye Mkoa wetu wa Singida, hakuna mradi wowote mkubwa wa maji ambao umeanzishwa kwa ajili ya kuokoa tatizo la maji katika Mkoa wa Singida.

Je, ni lini sasa Serikali itaenda kuwakomboa wanawake wa Mkoa wa Singida kwa tatizo la maji? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli watu wanaopata adha kubwa katika suala la maji hasa vijijini ni akina mama na Serikali inatambua

jambo hilo na ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 tumetenga shilingi bilioni 237. Hizi zinakwenda kwenye Halmashauri zote katika kutekeleza miradi ambayo iko vijijini na hususan miradi hiyo ikikamilika itakuwa imeondoa hii adha ya akina mama wanaopata shida ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali kama tuna mpango wa kupeleka mradi mkubwa, katika bajeti ambayo imetengwa hiyo ya shilingi bilioni 237, kwanza tunataka tukamilishe miradi ambayo tayari Serikali ilishawekeza. Kwa hiyo, ikishakamilika miradi hii tutaangalia mahitaji sasa ya ziada na tutaona namna gani tuweze kutafuta mradi mkubwa wa kuweza kuwafikishia wananchi wa Mkoa wa Singida. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlowe, swali la nyongeza.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri amekuwa akiahidi kila siku juu ya bili kupanda kwa wananchi wetu. Hapa ninavyoongea nina bili ya maji ya shilingi 700,000 ambapo maji hayatoki lakini unaletewa bili.

Sasa naomba kujua, je, ni lini, tunaomba ututajie kabisa Mheshimiwa Waziri utatekeleza ahadi hii kwa wananchi wetu kwa sababu wanaumia sana? Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlowe, tusaidie, hiyo bili ni ya kipindi gani? Maana isije ikawa ni ya mwezi mmoja; ili Mheshimiwa Waziri ajue anachojibu. Hiyo bili ya shilingi 700,000 ni ya muda gani? Hiyo uliyoishika wewe hapo ni ya muda gani?

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Bili hii ni ya miezi mitatu, lakini maji hayatoki kabisa. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshatoa maelekezo kwenye mamlaka zote kwamba haiwezekani mtu akalipa bili ya maji ambayo hajatumia. Kwenye mamlaka zote tumeweka bodi za kusimamia uendeshaji wa mamlaka zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba sana ndugu zangu, kama kuna mtu ambaye kapelekewa bili ambapo hakupata maji, basi mahali pa kupeleka ni pale kwenye bodi, maana hili ni suala mahususi ili liweze kushughulikiwa. Hatuwezi kuwa na jibu la moja kwa moja kwa sababu siyo wote wanaopata bili ya maji ambayo hawajatumia.

Mheshimiwa Nailbu Spika, kama kuna *special case*, naomba uniletee. Pia Mheshimiwa Mbunge akiwa kwenye Jimbo lake apeleke kwenye mamlaka ile, hasa kwenye Bodi ya Wakurugenzi inayosimamia uendeshaji wa mamlaka hizi ili mtu alipie maji aliyotumia tu, kulingana na Sera yetu ya Maji ya mwaka 2002 na Sheria Namba 12 ya mwaka 2009, kwamba ni lazima wananchi tutachangia huduma ya maji. Sasa katika kuchangia ni pamoja na kulipa bili, lakini kama bili ina mzozo, basi tatalishughulikia jambo hili na kuweza kulimaliza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mradi wa Maji wa Haydom unafanana kabisa na jinsi ambavyo matatizo ya Ngara yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu wa Haydom umekaa miaka saba, mkandarasi amechukua pesa na muda wa kukabidhi mradi umeshafika. Mkurugenzi kafanya jitihada mpaka leo mradi haujaisha.

Je, Mheshimiwa Waziri atanisiaidaje sasa kuisaidia Halmashauri yangu ule mradi wa Haydom ukaisha na wananchi wakapata maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, japokuwa hilo ni kama swali la msingi, ila sasa linahusu maji, naona Mheshimiwa Mbunge ameona aulize hapo hapo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, ipo miradi mingi ambayo ukamilishaji wake umechukua muda mrefu na sababu mojawapo ni ama kulikuwa na matatizo ya mkandarasi au kulikuwa na matatizo ya vyanzo au kulikuwa na matatizo ya kutokulipwa. Sasa tulipoingia awamu hii, maana hii ni miaka saba, sisi tuna miaka miwili, tumeanza kwanza kufuatilia miradi mmoja baada ya mwininge na kuhakikisha kwanza Wakandarasi wanarudi. Miradi mingi wakandarasi walikuwa wameondoka kwenye utekelezaji ikiwa ni pamoja na huo mradi wake ambao umechukua miaka saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mkandarasi amerudi na sasa hivi tunawapa fedha kwa kazi ambazo wamefanya. Kwa hiyo, nitafuatilia huu mradi anaousema ili niweze kuona nini kinachoendelea na tuweze kumwambia Mheshimiwa Mbunge ni lini kazi ile ingeweza kukamilika? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi, sasa aulize swali lake.

Na. 60

### **Uhaba wa Maji Jimbo la Masasi**

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA** aliuliza:-

Katika Jimbo la Masasi, Kata za Marika, Mumbaka, Matawale, Sululu, Mwenge, Mtapika, Temeke na

Chanikanguo, kuna tatizo kubwa la maji wakati eneo la katikati ya mji linanufaika na maji ya mradi wa Mbwinji.

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha kwa ajili ya upanuzi wa mradi wa maji wa Mbwinji ili usambaze maji katika vijiji vya Jimbo la Masasi?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Jimbo la Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Safi wa Masasi, Nachingwea kutoka chanzo cha Mbwinji unahudumia wakazi wa Miji ya Masasi na Nachingwea pamoja na baadhi ya vijiji vya Halmashauri za Wilaya ya Masasi Nachingwea na Ruangwa. Jumla ya wakazi wapatao 188,250 wanahudumiwa na mradi huo uliojengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 31 na kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 24 Julai, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali imeendelea kuunganisha vijiji zaidi ili kuongeza upatikanaji wa maji kuititia mradi huo. Kwa sasa baadhi ya vijiji katika Kata za Marika, Mumbaka, Matawale, Sululu, Mwenge, Mtapika, Temeke na Chanikanguo, vimeanza kupata maji na vijiji vilivyobaki katika Kata hizo vitaendelea kuunganishwa kutoka kwenye mradi huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuendelea kuunganisha vijiji vilivyobaki na katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Serikali imetenga shilingi bilioni moja ambapo hadi sasa shilingi milioni 370 zimeshatolewa kwa ajili ya kuendelea kuunganisha vijiji vilivyobaki kwenye Mradi wa Masasi, Nachingwea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Kata nyingi katika Kata alizozitaja hakuna hata kijiji kimoja chenye maji ya bomba, na kwa sababu Serikali imetenga fedha katika mwaka uliopita wa bajeti, shilingi milioni 599 na fedha hizi bado hazijakwenda katika Halmashauri yangu wakati wananchi wameshachimba mifereji kwa ajili ya maandalizi.

Je, Serikali itapeleka lini fedha hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Halmashauri yangu imeandika barua ya kuomba uchimbaji wa visima katika vijiji kumi vya Halmashauri yangu vilivyopo pembezoni, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya uchimbaji wa visima hivi? Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Chuachua kwa namna alivyoweza kuwahamasisha wananchi wa Masasi kujitolea kuchimba mitaro ili ile Mamlaka ya *MWANAWASA* iweze kuunganisha. Nilifika pale na nikaona hiyo kazi, tukacheza na ngoma. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Chuachua na nataka huu mfano uigwe na Waheshimiwa Wabunge wengine, kwamba ni vizuri tukahamasisha wananchi pale inapowezekana, kujitolea kuchimba mitaro ili kazi iweze kwenda haraka na wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake kwamba ni lini fedha zitapelekwa? Tayari nimeshaidhinisha kupelekwa fedha, hasa kuanzia Masasi Mjini kwa ile kazi ambayo niliona inaendelea. Kwa hiyo, nimeshaidhinisha fedha, kwa hiyo, sasa

hivi ziko njiani, muda siyo mrefu watazipata ili waweze kuunganisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili kuhusu ombi la visima, hili naomba nilipokee kwa sababu ameliuliza kama swali la nyongeza, nilipokee, nitakwenda kuangalia tuone namna gani tutasaidia kuweza kuchimba visima hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Masala, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kazi iliyofanyika Masasi ya kuchimba mitaro, kazi hiyo iliyofanyika pia katika Wilaya ya Nachingwea katika Kata za Naipanga, Chiwindi, Rahaleo, Mkotokweana pamoja na Stesheni. Kupitia nguvu za Mbunge na wananchi tumechimba zaidi ya kilometra 15. Sasa fedha iliyoletwa ni chache na sasa hivi ni mwezi, mabomba yaliyoletwa kwa ajili ya mradi huu yameshindwa kukidhi mahitaji ya mradi mzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata jibu la Mheshimiwa Waziri, ili nguvukazi za wananchi zilizotumika zisipote, ni lini fedha hii ambayo imeombwa kwa ajili ya mradi huu italetwa ili tuweze kukamilisha kazi ambayo tumelanza? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa WAZIRI wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naye nimpongeze kama ameweza kuhamasisha wananchi kuchimba mtaro wa kilometra 15 ili iwe kazi rahisi kwetu sisi kuweka mabomba. Tayari mabomba mengi yameshapelekwa, yapo Masasi na Nachingwea kwa ajili ya kuyalaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la fedha, fedha tunazipeleka kulingana na namna tunavyopokea. Kwa hiyo,

fedha za Mfuko wa Maji zinazokuja kwa mwezi ni kama shilingi bilioni kumi. Kwa hiyo, hizi ndizo tunazogawana kuwapelekea kila Halmashauri, pale ambapo inaonekana kuna kazi inayօendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi ambayo imeanza haitaachwa, tutapeleka hiyo fedha mapema iwezekanavyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yaliyopo huko Masasi, yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo katika Mji wa Itigi wenye vijiji saba vya Kihanju, Songambele, Tambukareli, Majengo, Ziginari, Itigi Mjini na Mlowa, hakuna kabisa mtandao wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tulishaandika barua kwa Wizara kuomba wataalam wa Wizara waje watufanyie upembuzi yakinifu na Wizara ikatujibu kwamba haina wataalam kwa sasa na kwamba tushirikiane na Mkoa, na tukaandika barua ya kuomba kiasi kidogo tu, shilingi milioni 40 kwa ajili ya kutusaidia bajeti ili wataalam hawa wa Mkoa na wale wa Halmashauri waweze kufanya upembuzi yakinifu ili tuwapatie maji wananchi wa Itigi.

Je, ni lini sasa Serikali itaisaidia Halmashauri ya Itigi hizo hela kidogo tu ambazo zitafanya nasi tupate mchanganuo wa kujua ni nini tunahitaji ili Wizara iweze kutupa pesa za kujenga miundombinu ya maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kuhusu fedha za uendeshaji au kufanya usanifu wa kazi kwenye Halmashauri yake, katika hii bajeti ya shilingi bilioni 237 tulioitoa, kazi yake kubwa kwanza ni kujenga miundombinu kama ipo lakini pia fedha hizo zinatumika kwa usanifu, usimamizi na kadhalika; lakini pia na uendeshaji wa ofisi ni fedha hiyo hiyo. Kwa hiyo, katika bajeti ambayo Halmashauri yake ya Itigi imetengewa kwa mwaka 2017/2018 naomba watumie sehemu ya hiyo fedha ili waweze kufanya hiyo kazi ambayo Mheshimiwa Mbunge anaizungumzia. Kama wanaleta maombi, maana tutawapa hizo fedha, lakini tutakata kwenye *allocation* ambayo wametengewa kwa mwaka 2017/2018.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Ruge, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda nimuulize Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza. Tatizo la uhaba wa maji katika Wilaya ya Serengeti hasa vijiji, limekuwa ni kubwa na la muda mrefu na kuanzia mwaka 2007 mpaka sasa hivi Serikali bado inatekeleza mradi wa maji katika vijiji kumi, ila mpaka ninavyozungumza kuna miradi miwili katika vijiji vya Kenyana, Nyamitita na Kibanjabanja hajakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua, ni lini sasa miradi hii itakamilika ili wananchi wa maeneo husika waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Catherine amezungumzia baadhi ya miradi ambayo ipo kwenye Halmashauri yake na kuniuliza ni lini miradi ile itakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba itabidi nifuatilie niweze kujua, kwa sababu hili ni swalii la nyongeza, siwezi kuwa najua kila kijiji katika nchi nzima, mradii ule uko katika *status* gani? Kwa hiyo, naomba sana tuonane naye, anakaribishwa ofisini ili tuweze kuangalia. Nitampa *status* na taarifa kamili ni lini miradi ile itakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, swalii fupi.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo hili la maji lipo kwenye *categories* mbalimbali kwa nchi nzima, wapo watu ambao hawana kabisa miradi katika maeneo yao kwa sisi Wabunge hapa ndani Bungeni, lakini pia yapo maeneo ambayo miradi ipo lakini hajikamilika kutokana na sababu mbalimbali, lakini yapo maeneo katika nchi yetu ambayo maji yanapatikana lakini kumekuwa na manung'uniko ya chini chini ya wananchi kwamba jinsi bili zinavyotoka kunakuwa hakuna usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo haya yamekuwa yakisemwa kwa wananchi kwa muda mrefu na yamekuwa takribani kila Mbunge anaposimama hapa wengi wamekuwa wakigusia kuhusu tatizo la kutokuwa na usawa wakati wa kutoa bili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara badala ya kusema kwamba wananchi au sisi Wabunge twende kwenye bodi kutoa malalamiko au wananchi waende kule kwenye taasisi za kutoa huduma ili kwenda kupeleka malalamiko yetu.

Je, Wizara hii haioni sasa umefika wakati kuchukulia tatizo hili kwa ukubwa wake kama tatizo la kitaifa, kuunda timu maalum itakayopita kila maeneo na kuweza kujua kwamba maeneo haya yana matatizo haya tuweze kuyatatua vipi na eneo hili matatizo yake tuweze kutatua vipi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Mayenga ameuliza swali zaidi ya moja; anazungumzia habari ya matatizo ya upatikanaji wa maji, lakini pia anachanganya tena na masuala ya bili. Sasa ni vitu viwili tofauti. Masuala ya upatikanaji wa maji, Serikali inaendelea kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la matatizo ya bili nimeshalitolea majibu, labda nirudie kwa kuweka msisitizo. Ni kwamba Wizara inatambua yapo maeneo ya mtu mmoja mmoja kulalamikia bili, siyo kwamba kila mmoja analalamikia bili. Sasa nasema, kama ni *isolated cases*, hatuwezi kuchukulia kama ni tatizo la Kitaifa. Hili ni tatizo la mtu mmoja ambaye ana tatizo, amepewa bili ya miezi mitatu hajapata maji.

Sasa hili naomba tulifuatilie kwa maana ya kwa huyo mtu ambaye anatuletea ni *isolated case* tuishighulikie. Siyo jambo la kusema tulitolee mwongozo kama Taifa kwa maana ya kwamba tumeshakubaliana kwamba maji ili yawe endelevu, upatikanaji wake ni lazima tuchangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kulipa bili ni lazima ili tuwe na uhakika wa kuwa na maji. Sasa kama kuna matatizo mahali, tutayashughulikia kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 61

#### **Huduma ya Dawa za Kurefusha Maisha**

**MHE. LUCY S. MAGERELI** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Ripoti ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI ya Februari, 2017 fedha za wafadhili zinaendelea kupungua na baadhi yake kuwa na masharti yasiyoendana na mila na desturi za Kitanzania.

Je, Serikali imejipangaje kuendeleza huduma zilizokuwa zikitolewa na wafadhili, hususan dawa za kurefusha maisha?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie kwamba Wadau wa Maendeleo wameendelea kutoa msaada wa dawa za kurefusha maisha (*Antiretroviral Drugs - ARVs*) mbali na kwamba Serikali imeendelea kupinga maadili mbalimbali yasiyoendana na mila na desturi za Kitanzania kwa kutoa miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha tunajipanga vyema na upatikanaji, hususan wa dawa za kurefusha maisha (*ARVs*), Serikali kwa sasa imeanzisha Mfuko Maalum wa UKIMWI unaojulikana kama *AIDS Trust Fund (ATF)*. Mfuko huu utachangiwa na Serikali, mashirika, sekta binafsi pamoja na wahisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la mfuko huu ni kuchangia upatikanaji wa dawa za kurefusha maisha hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Magereli, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa swali langu lilirejea Taarifa ya Kamati ya Mambo ya UKIMWI iliyotolewa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Februari mwaka huu, nilitarajia majibu ya Mheshimiwa Waziri yawe *at least* na takwimu ambazo sasa zitaunga mkono hoja ya Taarifa ya Kamati au zitatengua ile hoja ya Taarifa ya Kamati kwamba fedha za wafadhili katika eneo hili zimepungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu, Mheshimiwa Naibu Waziri anisaidie kwamba hao wadau aliowataja ni wadau gani ambao wameendelea kutoa *support* katika eneo hili? Kwa sababu tunafahamu fedha za mambo ya UKIMWI zimekuwa zikichangiwa kwa asilimia kubwa sana na *PEFA* na *Global Fund* ambao kwa sehemu kubwa wame-*pull out*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijajua hao aliowazungumzia hapa Mheshimiwa Naibu Waziri ambao anasema wanachangia kwa kiasi kikubwa kinyume na Taarifa ya Kamati ni akina nani? Napenda kufahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kumekuwa na maendeleo kadhaa ya kitabibu na kimaabara ambayo yanaonesha majoribio yaliyofanikiwa katika upatikanaji wa chanjo na hata tiba ya Virusi vya UKIMWI. Je, Serikali ina maelezo gani kuhusu maendeleo haya na taarifa hizi ambazo zinatokana na vyombo mbalimbali? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwamba ni wadau gani? Kwa mujibu wa sheria ambayo inaanzisha Mfuko wa UKIMWI Tanzania, malengo makuu ya mfuko huu ni kukusanya pesa ambazo zitakwenda kuweka uendelevu wa pesa ambazo zitakuja kuwa zinatumika *sustainably* kwenye kununua dawa za UKIMWI kwa

kiwango cha asilimia 60, lakini pia kutoa huduma za kinga kwa asilimia 25, pia kwa asilimia 15 kusaidia kwenye mwitikio wa UKIMWI kwa maana ya kujenga mazingira mbalimbali wezeshi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mfuko huu una malengo ya kuwa endelevu na ulianzishwa kwa malengo kutokana na mabadiliko yaliyofanyika kwenye Sheria ya UKIMWI ambayo ilianzisha *TACAIDS* mwaka 2001 Sheria Namba 22 kwa ajili ya kutengeneza *sustainability* kwenye eneo la upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya *HIV/Aids*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mfuko huu bado ni mchanga sana na umezinduliwa mwaka 2016 tu mwezi Disemba na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano za Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan na kwa mwaka wa fedha uliopita tultenga kiwango cha shillingi billioni 5.5 na mwaka huu tumetenga shillingi bilioni tatu. Kwa hiyo, ndiyo tumeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wadau ni akina nani? Wadau wa kwanza ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia bajeti yake, lakini pia tunatarajia mfuko huu utakusanya vyanzo vingine vya fedha kutoka kwa wananchi kwa ujumla ambao watajitekeza kuchangia kutoka kwenye sekta binafsi, asasi za kiraia, asasi za hiari, lakini pia wadau wa maendeleo hawazuilliwi pia kuchangia kwenye mfuko huo. Malengo yetu ni kwamba tuweze kufikia angalau asilimia 30 ya kujitosheleza kwenye fedha za dawa za kupunguza makali katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, chanjo ya virusi vya UKIMWI bado inaendelea kufanyiwa utafiti duniani, jitihada bado zinaendelea. Nasi Tanzania ni washiriki katika tafiti mbalimbali ambazo zitapelekea kupatikana kwa chanjo kwa siku zijazo, lakini kwa sasa tuko katika hatua za awali sana za Kisayansi za kutafuta chanjo hiyo na bado hakujawa na mwangaza mkubwa sana kwamba labda katika kipindi cha miaka kadhaa tunaweza tukawa tumeefikia hatima ya kuwa na chanjo ya virusi vya UKIMWI.

Kwa hiyo, tuendelee kuvumilia wakati wanasayansi wakifanya kazi yao kwenye maabara zetu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nimesimama kwa sababu Mheshimiwa Mbunge Lucy Magereli anazungumzia upatikanaji wa dawa za *ARV*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kusema kwamba tunazo *ARV* ambazo kuanzia mwezi Oktoba, 2016 zinatolewa kwa kila Mtanzania atakayepima na kukutwa na maambukizi ya VVU.

Mheshimiwa Naibu pika, sasa kwa nini nimesimama? Kati ya watu wenye maambukizi ya VVU, wanawake wanaotumia *ARV* ni asilimia 73, wanaume ni asilimia 48 tu. Kwa hiyo, nitoe wito kwa wanaume wote Tanzania watumie dawa za *ARV* ili kwa pamoja tuweze kupunguza maambukizi ya VVU nchini. Acheni kujiona nyie mna misuli, ni wababe, dawa za *ARV* zipo, tumieni ili tuweze kupunguza maambukizi ya UKIMWI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa sababu kati ya maambukizi mapya ya vijana wetu wenye miaka 15 mpaka 24 kwa wavulana ni asilimia nane na wasichana ni zaidi ya asilimia 80. Maana yake hawa wanaume ndio wanarudi tena kwa watoto wadogo na hivyo kufanya kuwepo kwa maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nitumie fursa hii Waheshimiwa Wabunge wakawahamasishe wanaume watumie *ARV*, zipo bure, zinapatikana na mtu yeoyote akipima anapata bila shida. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa majibu ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa ili kuweza kulithibitishai Bunge lako kwamba mfuko huu ambaou ulianzishwa kwa Sheria Namba 6 ya mwaka 2015 na unasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, umeanza kufanya kazi nzuri sana pamoja na uchanga wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maagizo ya Kamati kama alivyosema Mbunge aliyeuliza swalii, yalikuwa na malengo ya kuhakikisha kwamba Serikali inasimamia mfuko huu na unaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Kamati inayohusika na masuala ya UKIMWI waliiagiza Serikali, kwa rasilimali ndogo iliyopatikana ni lazima sasa mfuko uanze kuhakikisha unatoa fedha kupeleka Wizara ya Afya ili kushughulika na dawa na kuongeza maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1) cha Sheria hiyo, mfuko unakaribia kutoa, umeshapitisha kwenye Bodi jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 1.45 kwa ajili ya kununua dawa za *septrine* na kwa ajili ya kujenga Kituo cha Upimaji Mererani na kujenga kituo kingine cha upimaji kwenye Visiwa ndani ya Ziwa Victoria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwathibitishie Wabunge kwamba Kamati ilifanya kazi nzuri na Serikali imepokea maagizo hayo na tayari mfuko wetu umeanza kuonesha kwamba tunaanza kujitegemea ndani ya Serikali yetu ingawa wafadhili bado wanaendelea kutusaidia. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 62

**Kufanya Mapinduzi Katika Sekta ya Kilimo**

**MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza:-

Pamoja na kwamba sekta ya kilimo ndiyo yenyeye kuajiri Watanzania walio wengi, lakini sekta hiyo imekuwa na maendeleo hafifu kutohana na watumishi wachache wenye ujuzi wa kutosha na ukosefu wa vitendea kazi kama vile pikipiki, zana za kufundishia na kadhalika.

Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kufanya mapinduzi ya kilimo kwa kuwa na wataalam wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa Sekta ya Kilimo ni muhimu na ndiyo yenyeye kuajiri Watanzania wengi, hivyo mapinduzi ya kilimo pamoja na mambo mengine yatachangiwa uwepo na wataalam wa kutosha wenye taaluma na ujuzi stahiki ili waweze kushauri matumizi ya teknolojia na kanuni bora za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ili kuleta mapinduzi ya kilimo ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya Maafisa Ugami wenye ujuzi ili kila Kata na kijiji kiwe na Afisa Ugani mmoja. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha na kuwezesha

Vituo vya Kilimo na Vituo vya Rasilimali za Kilimo za Kata kwa ajili ya kufundisha teknolojia mbalimbali za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwaka 2016/2017, Serikali imeajiri Maafisa Ugani 8,756 sawa na asilimia 43 ya mahitaji ya Maafisa Ugani 20,374 katika ngazi ya kijiji, Kata na Wilaya. Jumla ya wataalam wa kilimo 8,000 ngazi ya Astashahada na Stashahada waliohitimu mafunzo katika Vyuo vya Kilimo wameajiriwa katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Serikali inaendelea kusomesha vijana tarajali na kuwaajiri kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine ni pamoja na kuboresha huduma za ugani kwa kusambaza teknolojia za kilimo bora kwa wakulima kwa kutumia njia mbalimbali hususan shamba darasa, vipindi vya redio na luninga, mchapisho na Maonesho ya Kilimo - Nane Nane.

Aidha, Serikali itaendelea kutoa ushauri wa kitaalam na kuandaa miongozo na mafunzo ya huduma za ugani, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kazi za ugani na kuboresha usambazaji wa teknolojia za kilimo bora kwa wakulima nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Pamoja na maelezo hayo, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kabisa kwamba kumekuwa na dhana potofu kuwa kilimo kimekuwa kama *last resort*. Hata ukiongea na watoto wetu wa shule, ukiwaliza unataka kuwa nani? Mmoja atakwambia daktari, mwanasheria, *engineer* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka nipate maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ni mikakati gani sasa kama Wizara au *incentives* gani mmeziweka ili iwe kivutio kwa hawa Watanzania na vijana wetu ambao kuna tatizo kubwa la *unemployment?* Hilo ni la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika maelezo yangu ya mwanzo niliongelea suala la wataalam nashukuru kuwa Mheshimiwa Waziri ameli-*address* lakini kwenye ukosefu wa vitendea kazi, Watanzania wamekuwa wakiwalamu sana wataalam hasa hawa Maafisa Ugani kuwa wamekaa tu Maofisini, lakini ukiangalia tatizo kubwa ni ukosefu wa vitendea kazi. Sasa napenda nipate maelekezo, ni mkakati gani kama Wizara mmeweka kuhakikisha hawa wataalam wetu wanapata vitendea kazi kama vile pipipiki na zana za kufundishia ili tuweze kuleta mapinduzi ya hii Sekta ya Kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuweka mazingira ya kilimo kuvutia watu wengi zaidi hususan vijana, naomba nimahakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa kilimo kinavutia sana na ndiyo maana hata baadhi yenu Waheshimiwa Wabunge ni wakulima hodari. Kwa hiyo, kizuri kinajiuza, kilimo kinalipa, tayari kuna watu wengi wamenufaika na hivyo niwasihî tu vijana kwamba kilimo kina manufaa. Vilevile Serikali imeweka mazingira mazuri sana ya kuwavutia vijana na ndiyo maana tumeweka taratibu za wao kupata mitaji, tumeanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo, tuna Mfuko wa Pembejeo, lakini vilevile hata Benki za binafsi zinatoa mikopo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba kilimo kinavutia, kuna uwezeshaji, kwa hiyo, vijana wanakaribishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kuhusiana na wataalam, Maafisa Ugani kutokuwa na vitendea kazi. Hili limezungumzwa sana, lakini mara nyingi vilevile imekuwa ni ksingizio. Kinachohitajika kwa Afisa Ugani anapokuwepo kwenye eneo lake la kazi ni elimu ile aliyonayo ajaribu kuitumia kuwafikishia wananchi. Mara nyingi katika ngazi ya kijiji huwezi kulalamika kwamba kwa sababu sina pipipiki, basi siwezi kuwafikia wananchi. Watendaji wengine wa Serikali walioko katika ngazi hizo wanafanya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na ukweli kwamba kuna hitaji la kuhakikisha kwamba hivyo vitendea kazi viweze kupatikana lakini tunawasihi kwamba isiwe ni kisingizio. Lazima watumie elimu ambayo wanayo kwa sababu ni ajira yao ili kujaribu kuhakikisha kwamba wananchi wanapata elimu ya kilimo bora.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendela na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 63

**Serikali Kuwezesha *SIDO***

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA** aliuliza:-

*SIDO* pamoja na majukumu mengine inatoa huduma kwa viwanda vidogo na vya katika kutoa mikopo, mafunzo na vitendea kazi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuiwezesha *SIDO* kutimiza majukumu yake?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa *SIDO* katika ujenzi wa uchumi wa Taifa letu imekuwa na mipango na mikakati mbalimbali ya kuliwezesha Shirika hili kutimiza majukumu yake. Kupitia Bajeti Kuu ya Serikali, *SIDO* inatengewa fungu kwa ajili ya kujenga miundombinu ya ofisi ya maghala ya viwanda (*industrial sheds*). Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga jumla ya shillingi bilioni 7.04 kwa ajili ya kujenga miundombinu

tajwa hapo juu katika Mikoa ya Katavi, Manyara, Kagera, Geita na Simiyu. Nafurahi kutamka kuwa tayari shilingi bilioni tano kati ya bilioni saba zilizopangwa kufanikisha jukumu hilo hapo juu zimeshatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hutoa fedha za mitaji kwa *SIDO* kupitia Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali (*NEDF*). Mfuko huu uliainzishwa mwaka 1994 kwa mtaji wa shilingi milioni 800 na mpaka sasa Serikali imechangia shilingi bilioni 5.05 ambazo zimezungushwa na wajasiriamali na kufikia shilingi bilioni 62.8 kwa mwaka wa fedha 2017/2018; na kwa mwaka huu sasa tumetenga shilingi bilioni 7.14 kwa ajili ya mfuko huu; na mahususi tutaelekeza juhudini zetu katika uanzishaji wa viwanda vidogo sana na viwanda vidogo chini ya mkakati wa Wilaya Moja, Bidhaa Moja (*ODOP*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia ina mkakati wa kuwatafutia *SIDO* wabia wa nje ili waweze kuwasaidia kufikisha huduma kwa wananchi hasa wafanyakishara na wenye viwanda vidogo. *SIDO* inashirikina na Shirika la viwanda la India (*National Small Industry Corporation of India*) katika masuala ya kukuza teknolojia. Ushirikiano huo unahusisha uanzishwaji wa kiatamizi cha teknolojia za aina mbalimbali katika Mitaa ya Viwanda eneo la Vingunguti Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* imewezesha kuingia ubia na Shirika la maendeleo la Sweden na wamepatiwa shilingi bilioni 1.8 kuanzisha Kongano. Vilevile *SIDO* imewezeshwa kuingia Ubia na Shirika la Maendeleo ya Uchumi la Canada (*Economic Development Associates*) ambao unawezesha kutoa mafunzo ya kuimarishe na kuendesha biashara katika ukanda wa Mtwara na Lindi na ukanda wa Morogoro mpaka Arusha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiteto Koshuma, swali la nyongeza.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *SIDO* ndiyo mlezi wa viwanda vidogo vidogo

pamoja na vya kati ambapo tunatarajia viwanda hivi viweze kuelekea katika kuwa viwanda vikubwa na hivyo kuweza kuwezesha uchumi wa viwanda kuendelea hapa nchini Tanzania na Waziri amekiri kabisa kwamba Serikali inalitambua hilo na imekuwa ikitenga fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana na mimi kutenga fedha na kupeleka fedha ni kitu kingine. Kwa taarifa nilizonazo kabisa ni kwamba Serikali kwa mwaka 2015/2016 ilitenga shilingi milioni 500; mwaka 2016/2017 Serikali ilitenga shilingi bilioni 2.4; na kwa mwaka 2017/2018 kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, Serikali imetenga shilingi bilioni 7.14.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pamoja na kutenga fedha hizi zimekuwa haziendi. Kwa maana hiyo, tunategemea nini?

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kauli mbio ya viwanda ambayo tumeona Mheshimiwa Rais amekuwa akiisema kweli itaweza kutimia kwa mwenendo huu wa kutokupeleka fedha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, wanawake wa Mkoa wa Mwanza wamekuwa wakijishughulisha na shughuli za viwanda vidogo vidogo, lakini changamoto kubwa waliyokuanayo ni kukosekana kwa vifungashio ambavyo wanavipata kwa gharama za juu sana na hivyo kushindwa kuijendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua kwamba Serikali inawezaje kuwasaidia wanawake wa Mkoa wa Mwanza ili waweze kupata kiwanda cha vifungashio ili waweze kujikwamua kiuchumi? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikiri na ninakubaliana naye. Ujenzi wa uchumi wa viwanda endelevu unatokana

na viwanda vinayoitwa *LGI* (*Local Grown Industries*) siyo hizi *FDI*. Hawa wanatafuta *green pasture*, wataondoka na Serikali inalitambua hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 tulipaswa kupewa shilingi bilioni 2.4, hatukupewa. Tumeiomba Serikali tupewe shilingi bilioni 7.04; nina imani Serikali itatoa pesa hizo na ninazifuatilia. Napenda niishie hapo na Kamati yangu imefanya kazi na tusipotoa pesa hizo, hivi viwanda tunavyoita *FDI*, hao ni kware. Huwezi kulisha kware ukawaacha watoto wa kuku. Naomba niishie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vifungashio ni tatizo kwa wajasiriamali wadogo wote. *SIDO* tumeamua kuwekeza katika kiwanda cha vifungashio na hicho kitatoa vifungashio kwa akina mama wote na wajasiriamali wadogo. Nachukua firta hii kuwashimiza wajasiriamali wanaoweza kuwekeza kwenye biashara hii wawekeze katika vifungashio. Tunatumia pesa nyingi za kigeni kuagiza vifungashio kutoka nje ya nchi.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, sasa aulize swali lake.

Na. 64

#### **Matumizi ya Teknolojia ya Graphogemu-Kiswahili katika Kufundisha Katika Kufundishia**

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa (SEKOMU) kilichopo Lushoto kwa mafanikio makubwa kimeweza kutumia teknolojia rahisi inayoitwa *Grapho Game*, kwa kiswahili ni Grafo Gemu kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika darasa la kwanza

na la pili katika shule kadhaa zilizopo Wilaya ya Lushoto na Bagamoyo na pia SEKOMU kwa kutumia teknolojia hiyo imeweza watu wazima kujua kusoma na kuandika katika kijiji cha Kwemishai – Kibohelo – Lushoto.

(a) Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kuwatumia wataalam walioko SEKOMU akiwemo mtalaam aliyeshiriki kutayarisha maudhui katika teknolojia ambayo imeweka msisitizo katika mbinu za kufundishia kusoma ya kifoniki ambayo hujikita katika utambuzi wa sauti za herufi zinazounda maneno?

(b) Je, Serikali haioni ni jambo muhimu kabisa kwa kupitia mpango huu muhimu na maalum kama walivyofanya nchi ya Zambia na Finland kuidhinisha matumizi ya teknolojia hiyo iwe kama teknolojia suluhisho (*IT Solution*) kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa madarasa ya mwanzo ya elimu ya msingi wenye changamoto ya kujua kusoma na kuandika?

#### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Seriakli inatambua umuhim,u wa kuimarisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa wanafunzi wanaosoma madarasa ya chini hususan elimu ya awali, darasa la kwanza hadi darasa la nne na watu wazima wasiojua kusoma na kuandika kwa kuwa stadi hizo zinawawezesha kupata umahiri katika stadi za KKK.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itawasiliana na mtaalam wa *Grafo Gemu* (kiswahili) ili kufahamu jinsi teknolojia hiyo inavyofanya kazi. Wizara itakapo jiridhisha na ufanisi wa matumizi ya teknolojia hiyo, itafuata taratibu stahiki na kuidhinisha matumizi ya teknolojia hiyo shulenii.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, wakati Waziri anaendelea kufanya utafiti juu ya Grafo Gemu, je, Serikali ina mpango mkakati gani wa haraka wa kuweza kuwapatia baadhi ya vifaa ili wataalam wetu hao waendelee kuwasaidia watoto wetu pamoja na kwamba suala hili litakuwa ni suala la Kitaifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ni ya hapa kazi tu; je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongozana na mimi wakati Bunge likahirishwa ili akaone juhudzi za wataalam hawa watokao *SEKOMU* wanaofanya kazi kubwa kuwasaidia watoto wetu hasa mama yangu mtaalam anaitwa mama Gorosho? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimezungumza kwamba Wizara ingependa kujiridhisha namna gani teknolojia hiyo inavyofanya kazi na namna gani inavyoweza kuwanufaisha wanafunzi wengi zaidi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kawaida yetu sisi Waheshimiwa Mawaziri wengi tumekuwa tukiambiwa kutembelea maeneo na tunafanya hivyo. Kwa hiyo, nimwambie tu kwamba nitakuwa tayari kutembelea katika eneo la Mheshimiwa Mbunge ili kujiridhisha lakini vile vile kuona uwezekano wa kutoa vifaa ambavyo vitahitajika kama ambavyo ameomba. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake. (*Makof*)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mheshimiwa Pauline Phillip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 65

**Mapitio ya Sera ya Elimu Bure**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Serikali iliwahi kuliahidi katika Bunge hili kuwa inafanya mapitio ya Sera ya Elimu Bure na kwamba ingeleta Bungeni mambo yanayohitaji kuboreshwa:-

Je, ni lini mapitio hayo yatakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wangu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Phillip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliamua kuondoa malipo ya ada kwa elimu msingi inayojumuisha elimu ya awali pamoja na darasa la kwanza hadi kidato nne kama utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Ibara ya 3.1.5 na llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 Ibara ya 52(a). Lengo la Sera hii ni kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanapata fursa hiyo bila kikwazo chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa maamuzi hayo ya Serikali kwa ustawi wa wananchi na Serikali kwa ujumla mwezi wa Februari mwaka 2017 Wizara ilifanya ufuatiliaji kuhusu utekelezaji wa Sera hii ili kubainisha mafanikio na changamoto kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wake.

### **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itatumbia matokeo na mapendekezo ya ufuatilaji uliofanyika kutatua changamoto zilizojitokeza ili kuhakikisha lengo la Serikali la kutoa fursa kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule linafikiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwanza ni vizuri Serikali ikakiri kwamba imeshindwa katika Sera hii ya Elimu Bure na nitatoa mfano. Fedha wanazopeleka katika shule zetu asilimia 35 ni fedha kwa ajili ya utawala na chini ya utawala kuna mambo matano yafuatayo: Kuna *stationery*, maji, walinzi, umeme na dharura. Nitoe mfano katika sekondari moja ya Babati, sekondari ya Bagara – wanapeleka milioni moja na laki saba asilimia 35 ni 302, 4716.55. Katika 324,000 mlinzi analipwa 150,000, maji 200,000 acha *stationery*, acha dharura, kwa hali ya kawaida walinzi wameshaondoka katika shule zetu. Maji yamekatwa katika shule zetu za msingi na sekondari. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini hawataki kueleza ukweli kwamba wameshindwa kutekeleza sera hii kwa sababu shule zetu zimeachwa sasa na hakuna maji. Naomba majibu ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri katika majibu yake anasema kwamba tangu Februari 2017...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, tusaidie ufupisho kidogo maelezo ya la pili kwa sababu la kwanza umechukua muda mrefu sana.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijakupata.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**NAIBU SPIKA:** Fupisha maelezo ya swali lako la nyongeza la pili kwa sababu swali lako la nyongeza la kwanza limechukua muda zaidi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa wamefanya uchambuzi huu tangu Februari, 2017 mpaka sasa hawajarekebisha haya, ni kwa nini sasa wasiruhusu wazazi wachangie maji na walini katika shule zao kwa sababu sasa ukitaka kuchangia tu wanasema Serikali inapeleka fedha wakati Serikali haipeleki. Watoe mwongozo tuchangie kuliko watoto wetu wakose maji na walini waache shule zetu. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Serikali haijashindwa! Narudia tena kusema, Serikali haijashindwa! Kwa nini nasema Serikali haijashindwa? Nimeshatembelea mikoa mingi sasa hivi, nimeshatembelea shule nydingi sasa hivi, Kimsingi wanashukuru sana kwamba sasa kuna utaratibu wa wazi wa kupeleka fedha hizo kwenye shule. Wao wenyewe wanapanga, isipokuwa, lazima nikiri bado yapo matatizo machache yanayohitaji kurekebishwa. Tatizo mojawapo lilikuwa ni kutokuwa na ubora wa takwimu. Kuna baadhi ya shule zilikuwa hazijaweza kuleta takwimu zilizo sahihi na hapo ndipo tulipoweza kubaini hata wanafunzi hewa na hivyo tukaweza hata ku-save baadhi ya fedha takriban shilingi milioni 720 zilizokuwa zinaenda zikiwa hewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Rais na sisi kupitia Wizara hizi mbili tumekuwa tukisema kila wakati kwamba, wazazi wasijitoe katika kuendelea kusaidia elimu nchini. Pale panapoonekana kuna mahitaji ya msingi zipo taratibu zimeshatolewa mwongozo, Kamati za Shule kushirikiana na wazazi kuweza kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutatua.

### **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nadhani nimejibu yote kwa ujumla. Kwa hiyo, ninachomwomba tu Mheshimiwa kule kwenye jimbo lake aendelee kuhakikisha anashirikiana na Kamati za Shule lakini pia na uongozi kuona kwamba elimu hii tunaishughulikia wote kwa pamoja na hili sio suala la kusema nani afanye, nani asifanye! Mzazi anao wajibu wa kwanza katika kuhakikisha mwanafunzi wake anasoma vizuri. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati na Mdini, Mheshimiwa Abdallah Haji Ally Mbunge wa Kiwani sasa aulize swali lake.

Na. 66

### **Faida na Changamoto za Mfumo wa Vyama Vingi**

**MHE. ABDALLA HAJI ALI** aliuliza:-

Uzalishaji wa mafuta na gesi ni suala la Muungano na kwa kuzingatia ukweli kwamba visima vyta gesi vya songosongo na Mnazi *BayMkoani Lindi* na Mtwara vimekuwa vikizalisha gesi muda mrefu sasa:-

(a) Je, uzalishaji wa gesi kwa siku kwa visima hivyo ni mita za ujazo kiasi gani?

(b) Je, tangu uzalishaji ulipoanza mapato ya fedha yamekuwa kiasi gani kwa mwaka na yanatumikaje?

**NAIBU SPIKA:** Upande wa Serikali sijui ni nani anasimama, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI (K.n.y WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo.

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wastani jumla ya futi za ujazo milioni 145 za gesi asilia huzalishwa kwa siku katika visima vya uzalishaji gesi asilia vya Songsongo na Mnazi Bay ambako kiasi cha futi za ujazo milioni 90 huzalishwa kwenye visima vya Songsongo na kiasi cha futi za ujazo milioni 55 huzalishwa katika visima vya Mnazi Bay.

Mheshimiwa Naibu Spika, gesi asilia inayozalishwa hutumika kuzalisha umeme katika mitambo ya *SONGAS megawatt* 189; Kinyerezi, *megawatts* 150; Ubungo I *megawatts* 102; Ubungo II *megawatts* 129; Somangafungu *megawatts* 7.5; Tegeta *megawatts* 45; na Mtwara *megawatts* 18. Aidha, kiasi kingine cha gesi asilia hutumika kama chanzo cha nishati kwenye viwanda 42 vilivyounganishwa pamoja na matumizi madogo kwenye nyumba kwa ajili ya kupikia na kuendeshea magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha jumla ya shilingi bilioni 488 zimekusanywa kutoka kwenye mauzo ya gesi asilia kwa miaka sita tangu 2011 hadi 2016 sawa na wastani wa kiasi cha shilingi bilioni 81.3 kwa mwaka. Mapato haya huwasilishwa Hazina kwa mujibu wa taratibu husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Haji Ali swalii la nyongeza.

**MHE. ABDALLA HAJI ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa masikitiko tu kidogo kwamba hili suala tunasema ni la Muungano lakini katika majibu ya Naibu Waziri naona hakutaja upande wa pili hata neno moja, sijui kama tumo au hatumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swalii la kwanza; kwa kuwa Sheria ya Mafuta na Gesi ni ya Muungano na hivyo kila nchi inastahiki kupata gawio stahiki kutokana na mauzo ya gesi. Je, ni kiasi gani cha gawio kilichopelekwa kwa Hazina ya Zanzibar tangu mauzo haya ya gesi yafanyike?

### **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kitaalam tunaambi kwamba gesi inayozalishwa Tanzania ni gesi safi kabisa, yaani haihitaji gharama kubwa kufanyiwa mchakato kwa matumizi. Sasa tulitegema kwamba umeme unaotokana na uzalishaji kutokana na gesi hii ungekuwa rahisi kwa watumiaji lakini kila siku umeme unapanda bei. Ni kwa sababu gani? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI (K.n.y.)**  
**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba suala la gesi asilia ni suala la Muungano kwa mujibu wa Ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Nyongeza ya kwanza ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gawio la Zanzibar kutokana na mapato ya gesi ni suala la takwimu, ningeomba niweze kulifanyia kazi halafu niweze kumpatia Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili kwamba katika hali ya kawaida gesi inatakiwa iweze kuzalisha umeme ambao ni bei rahisi, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba huo ndiyo ukweli na toka tuanze kuzalisha umeme kwa kutumia gesi tumeweza kuokoa fedha nyingi sana. Kwa mwaka inakadirisha tunaokoa dola za Kimarekani bilioni 1.6 ambapo kama tungetumia umeme wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimweleze tu kwamba pamoa na bei ya umeme kuendelea kubadilika badilika lakini bado itabakia kwamba tokea tumeanza kutumia umeme wa gesi tumeweza kupunguza gharama kubwa sana za fedha tunazotumia katika kuzalisha umeme.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta matangazo tuliyonayo mezani...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wako...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaku nina uhakika hutaki kuanza kukumbushwa Kanuni sasa hivi kwa sababu hizo ni fujo.

Tutaanza na wageni walioko jukwaa la Spika, wageni wanne wa kwangu mimi kutoka Umoja wa Mabunge Duniani (*IPU*) Mheshimiwa Win Masiko, huyu ni Mbunge kutoka Bunge la Uganda, karibu sana na utupelekee salamu zetu kwa Mheshimiwa Spika huko mwanamama matata kabisa Mheshimiwa Kadaga. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni mwengine anaitwa Hilary Gbedemah kutoka Ghana, karibu sana. Tunaye pia Profesa Masheti Masingila kutoka Kenya. (*Makofi*)

Naona kuna wageni wengine pale lakini sijapata majina yao. Karibuni sana wageni mliokaa jukwaa la Spika, kwenye Bunge letu. (*Makofi*)

Tunaye mgeni mwengine ambaye amekaa hapo ni Mstahiki Meya wa Manispaa ya Moshi Mkoani Klimanjaro Mheshimiwa Raymond Robert Mboya, karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kundi la kwanza ni wageni 100 wa Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer ambaao ni wanafunzi 90 na Walimu 10 kutoka Mwalimu Anna *English Medium Pre and Primary School*, Mkoani Arusha. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 40 wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambaao ni wanafunzi wa Liwale *High School* na Walimu wao kutoka Mkoa wa Lindi. Karibuni sana na

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

nimepewa taarifa Waheshimiwa Wabunge kwamba hii shule ndiyo iliyoongoza kimkoa kwa matokeo mazuri Mkoani Lindi. (*Makof!*)

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambaa ni familia yake wakiongozwa na Nicolson na Maria. Karibuni sana, hawa wameongozana na wadogo zake ambaa wanaitwa Marwa na Jessica. (*Makof!*)

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi ambaa hawa ni wataalam wa kutafsiri Grafo Gemu ambayo ililiziba swali hapo kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili na hawa wanatoka Chuo cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa yaani *SEKOMU* Lushoto. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao pia wanafunzi ambaa wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 80 na Walimu watatu kutoka Bwawani *Secondary School* ya Mkoani Morogoro, sijui hawa watakuwa wamekaa sehemu gani. Pengine hawakupata nafasi ya kuingia. Karibuni sana wageni wetu.

Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo mengine. Tangazo lingine linatoka kwa Manager wa Bunge *Sports Club* Mheshimiwa John Kadutu. Mheshimiwa Kadutu anawatangazia Waheshimiwa Wabunge siku ya Jumamosi tarehe 9 Septemba, 2017 Bunge *Sports Club* ilipigwa mabao mawili kwa moja na timu inayotoka kwa Mheshimiwa Spika, Salasala *Vison Group* –jamani shangilieni timu ya Spika ilishinda. (*Makof!*)

Naona Waheshimiwa Wabunge mmezoea kushangilia timu ya Bunge *Sports Club*, safari hii timu ya Mheshimiwa Spika ilishinda na hapa Mheshimiwa Kadutu anajaribu kusema kwamba ni kwa sababu Mheshimiwa Spika aliomba. Mlifungwa tu Waheshimiwa, kubalini kushindwa! (*Makof!*)

Pia tarehe 10 Septemba, 2017 Bunge *Sports Club* ilirudi kwenye makali yake kwa kuwafunga bila huruma timu ya

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Muongano Veterans ya hapa Dodoma magoli matatu kwa bila. Nyota wa mchezo huo alikuwa Mheshimiwa Venance Mwamoto na huyu ni kocha wa timu. (*Makofu*)

Waheshimiwa Wabunge ninayo hapa taarifa ya Mheshimiwa Spika, anapenda kuwalishwa kuwa tarehe 8 Septemba, 2017 alipokea taarifa kutoka kwa Kaimu Katibu Mkuu wa CUF Mheshimiwa Magdalena Sakaya kuwa katika kikao chao cha tarehe 6 Septemba, 2017 walichagua viongozi wa Kambi ya Wabunge wa Chama hicho hapa Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma atakuwa Mwenyekiti; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed atakuwa Katibu; Mheshimiwa Maulid Said Mtulia atakuwa Mnadhimu na Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo atakuwa Mweka Hazina wao. (*Makofu*)

Hivyo, basi Mheshimiwa Spika, anawatangazia mabadiliko hayo ya uongozi wa Chama cha wananchi (*CUF*) hapa Bungeni na Mheshimiwa Spika ameahidi ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yao. (*Makofu*)

Waheshimiwa Wabunge ninalo pia tangazo kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa TWPG, Mheshimiwa Suzan Lyimo anatangaza kuwa na miwani ambayo iliachwa wakati wa *family planning seminar* ambayo ilikuwa siku ya ijumaa tarehe 8, Morena Hotel. Kwa hiyo, aliye poteza miwani ama aliyesahau miwani amwone Mheshimiwa Suzan Lyimo.

Pia yupo Mheshimiwa ambaye alisahau simu yake tarehe 9 kwenye semina ya kuhusu *CEDAW* ambayo ilifanyika pia Morena, naye aliyesahau simu hiyo amwone Mheshimiwa Susan Lyimo atapatiwa hiyo simu yake.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante, nimesimama kwa kanuni ya 68(7) naomba mwongozo wako kwa kuokoa muda sitoisoma. Naomba mwongozo wako kwa sababu kumekuwa na utaratibu kunaleta wageni kuwaona wanafunzi kuja kujifunza lakini wageni hawa mara nyingi wamekuwa wakikwama pale mapokezi na matokeo yake wanaingia ukumbini baada ya Spika kuingia. Pengine wanachelewa zaidi wanakuja mpaka kipindi cha katikati ya maswali. Sasa naomba mwongozo wako kwa utaratibu hii ile dhana ya wanafunzi hawa kuja kujifunza inakuwa bado haijakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimesimama kwa kanuni ya 68(7) nikirejea kwenye majibu ya Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Olenasha akijibu swalil la nyongeza kutoka swalil namba 62 alizungumza kwamba Serikali imeanzisha Benki ya Wakulima, mimi nashukuru na hilo ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako kuna tatizo linalojitokeza katika mabenki au taasisi za fedha hazikubali hatimiliki za vijiji ambazo wanazo wananchi wetu wa kule vijijini ambao ni wakulima akinamama, vijana na wazee. Sasa hizo hatimiliki za mila hazikubaliki lakini amewahamisisha hapa vijana wajunge katika shughuli za kilimo kwa kuwa Watanzania wengi wamenufaika. Sasa naomba mwongozo wako, watanufaika vipi hali ya kuwa hata hiyo mikopo yenyewe hatimiliki za kimila walizokuwa nazo hazikubaliki na taasisi za fedha? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM JAKU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa kanuni ya 68(7) nafikiri haina haja ya kutaka

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kuisoma ili kupoteza muda wako. Hoja zangu zilikuwa ni mbili. Kumetokea kitendo hapa ambacho kinaweza kutugombanisha na Rais wetu, hasa *back bencher* wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha alipokuwa akijibu swalii alisema tumuunge mkono Mheshimiwa Rais. Kinachoonekana kwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri mara nydingi huwa akijibu hapa hatumuungi mkono. Kwa maana hiyo sisi *back bencher* humu hatumuungi mkono, ni kitu cha kusikitisha sana na kinatugombanisha na wapiga kura wetu. Nahitaji mwongozo wako hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la kibinadamu zaidi na ubinadamu huo umeonesha wewe ulipotoa gari kumuhudumia Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki kumpeleka hospitali umeonesha ubinadamu mkubwa wa hali ya juu, gari ya familia yako nikupongeze kwa hilo. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa kuonyesha ubinadamu wao bila kujali itikadi ya vyama na huu ndio ubinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu, hili ni la kibinadamu zaidi ulifikiri na ubinadamu wenywewe umeanza kuonyesha wewe na hata sisi Wabunge katika posho zetu kukatwa. Ningombu tu ili kutaka kujua hali ya mgonjwa ukateua watu kama watatu au wanenye kwenda kuangalia hali ya Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu Mughwai ili kuridhia kibinadamu hili nafikiri halitotaka muda, hili ni la kibinadamu, halimo katika kanuni zetu ni ungwana zaidi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana na mimi nasimama kwa kanuni ya 68(7). Wakati Waziri wa Afya akijibu swalii hapo la Mheshimiwa Magereli, amerudia mara mbili kauli ambayo kiukweli sisi wanaume haijatuweka kwenye mazingira mazuri. Amezungumza naomba kunukuu kwamba "anawaomba wanawake wote wawalazimishe wanaume wao waende

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kunywa dawa za ARV's, sasa ni wanaume wote na wazima au wanaume wanaoumwa, nataka tu mwongozo wako. (Kicheko)

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante, napenda kutumia kanuni juu ya jambo lilitokoera leo na linalotokana na taarifa ambayo umetusomea hapa inayotokana na maagizo ya Spika, kwamba isomwe hapa. Katika taarifa hiyo, umeeleza kwamba kuna uongozi mpya wa Kambi ya Upinzani *CUF* ndani ya Bunge ambayo umetusomea orodha yake lakini sisi tunajua kwamba tuna uongozi rasmi wa Kambi ambaao tuliuchagua kwa kura na wakati huo tukiwa watu 42 tukapiga kura na uongozi huo haujaezuliwa kwa njia yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, na juzi tulichagua mwenyekiti wetu kwa sababu Bl. Riziki hayupo tukamchagua bwana Abdallah Mtalea kuwa Mwenyekiti na pia tukamchagua Mweka Hazina wetu mwingine na hatua iliyofuata ilikuwa ni kiliarifu Bunge. Mwongozo wangu nataka kujua hivi nani anayeamua uongozi wa chama, walio wengi au walio wachache? Je, tokea lini Bunge hili ndani yake kukawa na uongozi mbili bila ule mwingine kuondoka, kuijuzulu au kuvuliwa madaraka? Naomba mwongozo wako. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo kadhaa hapa. Wa kwanza ni mwongozo uliyombwa na Mheshimiwa Kuchauka ambaye ametoa maelezo kwamba, wako wageni ambaao huwa wanakwama sehemu za kuingilia magetini na hivyo kuchukua muda mrefu pale na kukuta humu Bungeni wakati mwingine wanaingia Mheshimiwa Spika, akiwa ameshaingia.

Kimsingi hili ni jambo ambalo linatakiwa kufanyiwa kazi kiutawala kuliko kutolewa mwongozo na kitu kwa sababu zile kanuni nadhani tutafika mahali mtu akitaka kusimama nayo aisome yeye mwenyewe kwanza, kwa sababu jambo unaloliombea mwongozo unataka kujua kama linaruhusiwa humu ndani au haliruhusiwi ndio unataka mwongozo wa Kiti.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Sasa jambo hilo haliko kwenye eneo hilo, kwa hiyo niseme na watu wa Katibu wako hapa mezani, watampelekea ujumbe wako Mheshimiwa Kuchauka lakini si jambo linalohitaji kutolewa mwongozo na kitu.

Nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Mbarouk Mussa akitoa maelezo kwamba wakati likijibiwa swalii la 62 Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi alitoa maelezo ya kuanzishwa kwa benki ya wakulima. Yeye anasema tatizo lipo kwamba benki zinakataa hati miliki za kimila sasa, hawa watu watanufaika vipi na mikopo kutoka kwenye hiyo benki.

Mambo mawili, la kwanza, Mheshimiwa Spika alishawahi kutoa maelekezo hapa ama mwongozo hapa kwamba namna maswali yalivyojibiwa, mtu anayeweza kuwa na hoja na swalii hilo ni yule aliyeyuliza swalii. Kwa hiyo, huo ni upande mmoja.

Upande wa pili kwamba jambo hili kwamba linaruhusiwa ama haliruhusiwi humu ndani mabenki siyo ambayo yako humu ndani. Kwa hiyo, kwa kuwa hilo jambo hatushughuliki nalo hapa ndani sitalitolea mwongozo, lakini naamini Waziri kwa namna ulivyoeleza amepata taarifa hiyo kwamba hati za kimila zinakataliwa na yeye ataona namna bora ya kushauriana na hiyo benki iliyo chini ya Wizara yake.

Mheshimiwa Jaku na yeye ametoa maelezo kuhusu majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwamba alipokuwa akitoa maelezo ya maswali yaliyoulizwa alikuwa akisisitiza kwamba tumuunge mkono Mheshimiwa Rais na juhudzi zake za kukusanya kodi na mambo mengine ambayo aliyeleza ambayo sitaki kuyarudia.

Kwa maelezo ya Mheshimiwa Jaku, anaona maelezo kama hayo ni kana kwamba humu ndani Mawaziri pekee ndio wanaomuunga mkono Mheshimiwa Rais, lakini wale wanaouliza maswali ambao Mheshimiwa Jaku anasema ni *back benchers* wao ni kana kwamba hawamuungi mkono Rais kwa kuuliza maswali.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Niseme hivi, hizi ni lugha za kawaida wala hazina lengo la kugombanisha na hata namna alivyolizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri sidhani kama alimaanisha kwamba haungwi mkono, alimaanisha kwamba twende pamoja katika mambo haya na kumwelewa majibu aliyokuwa akiyatoa hapa mbele. (*Makofi*)

Ametoa maelezo tena kwa namna nyingine kwamba, kiti kitoe mwongozo kufanya jambo la kibinadamu la kuteua Wabunge kwenda kumwona Mheshimiwa Tundu Lissu kule alikolazwa. Nimtaarifu tu Mheshimiwa Jaku pengine anaweza kuwa hana taarifa, lakini Mheshimiwa Lissu kule aliko yuko na Mheshimiwa Freeman Mbowe ambaye ni Mbunge, yuko pia na Mheshimiwa Msigwa naye ni Mbunge. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika anapata taarifa kutoka kwa hao walioko huko na kama ambavyo mlishtaaarifiwa kwa maelezo marefu sana aliyotoa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbowe anawasiliana naye, kwa hiyo, tusipate wasiwasi wowote.

Nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Musukuma, kuhusu msisitizo aliota Mheshimiwa Waziri wa Afya kwamba kina mama ambao wao kwa asilimia kubwa na ametaja nadhani zaidi ya 70 kwamba wao wanakunywa dawa, maana yake ni wale walioathirika ndio wanaokunywa dawa. Sasa akasema wale akinamama wawasadie waume zao ili na wao wanywe dawa.

Kwahiy, Mheshimiwa Musukuma usitie shaka, wale waliopima kama mama amepima na anatumia dawa ama wameenda wote wamepima wanapaswa kutumia dawa halafu mama anatumia yeye hatumii, huyu mama nina uhakika hataki kubaki mjane. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri alikuwa anasisitiza tu kwamba ili mama asibaki mjane basi amsaidie na aweze kunywa hizo dawa, lakini pengine Mheshimiwa Waziri kwa hizo takwimu ulizotoa sina hakika kama na humu Bungeni zinahusika, labda utusaidie hicho kipimo ili na sisi tupime humu halafu tuone namna bora ya kuweza kwenda nalo hilo, ili tuone takwimu zetu zinaenda vipi. (*Makofi*)

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Ally Saleh kuhusu taarifa niliyoisoma ya Mheshimiwa Spika, kuhusu uongozi wa Kambi ya *CUF*. Mheshimiwa Ally Saleh ametoa maelezo ambayo nisingependa kuyarudia lakini kimsingi anataka kujuu nani anaamua uongozi, ni wengi ama wachache. Waheshimiwa Wabunge Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunawajua viongozi wake, lakini pamoja na kwamba kuna Kambi Rasmi, vyama pia vinakuwa na uongozi wao.

Sasa uongozi wa Chama cha Wananchi (*CUF*) ndio wanaoulizia Mheshimiwa Ally Saleh na kwamba taarifa ya Mheshimiwa Spika imetaja viongozi ambao yeye anafahamu viongozi wengine ambao wamechaguliwa. Sasa kwa maelezo aliyotoa ni kwamba pengine kwamba taarifa za kikao hiki Chama cha *CUF* inavyoonekana kina makundi mawili, kundi moja limefanya uchaguzi bado halijamtaarifu Spika, kundi moja limefanya uchaguzi limemtaarifu Spika.

Mheshimiwa Ally Saleh naona unapunga mkono na maelezo uliyoyatoa mwenyewe, ukinitaka niitishe *hansard* nitaita. Umesema hivi, tumefanya kikao, tulikuwa katika mchakato wa kutaka kumweleza Mheshimiwa Spika, sasa hilo lina tofauti na hili ninaloeleza mimi hapa, kwa hiyo, tulia kidogo.

Sasa Waheshimiwa wabunge hii taarifa imesomwa kama ilivyoletwa hapa mezani. Mambo yaliyoko kwenye kambi mahususi ya Chama cha Wananchi (*CUF*), mimi naona ninyi mtakapofikia mahali ambapo mnataka kuzungumza na Spika na kuona uongozi ni upi mtafanya hivyo, lakini Bunge hili hatutaweza kuanza kujadili jambo hilo sasa hivi. (*Makofi*)

Kwa hivyo, niwaombe kama ambavyo taarifa hii imekuwa naamini hata hiyo nyngine Mheshimiwa Spika atakavyoamua italetwa hapa. Kwa hivyo, siwezi kulielezea jambo hilo kwamba linaruhusiwa ama haliruhusiwi hapa ndani kwa sababu chaguzi za ndani ya *CUF* hazijafanyika hapa ndani. (*Makofi*)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa tangazo lingine hapa na Mheshimiwa Maulid Mtulia anasema ana wageni wake hapa ambao wametokea Dar es Salaam wakiongozwa na Dkt. Jamal Adam Katundu, karibuni sana.

Kwa hiyo, baada ya hapo, tutaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA- KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAAZIMIO**

**Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba (*Intergovernmental Agreement – IGA*) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamuhuri ya Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (*East Africa Crude Oil Pipeline – EACOP*) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kuwepo hapa Bungeni leo tukiendelea kutekeleza majukumu yetu. Aidha, nakupongeza kwa namna ambavyo wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Spika, mnavyoliongoza na kuliendesha Bunge hili mkisaidiwa na Wenyeviti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda ni Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoundwa tarehe 30 Novemba, 1999 ambayo malengo yake ni pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya Nchi Wanachama kwenye maeneo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiteknolojia, utafiti, ulinzi na masuala ya kisheria.

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 101(1) ya mkataba kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inahamasisha Nchi Wanachama kushirikiana katika utafiti, uendelezaji na utumiaji wa rasilimali mbalimbali za nishati zilizomo katika ukanda wa Afrika Mashariki. Vilevile Ibara ya 101(2)(a) ya mkataba huo inasitiza kuhusu ushirikiano katika ujenzi wa mabomba ya usafirishaji wa mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Uganda kupitia kampuni za kimataifa za *TOTAL*, *TULLOW* na *CNOOC* iligundua kuwepo kwa mafuta ghafi takribani mapipa bilioni 6.5 katika eneo la Albetini nchini Uganda. Kufuatia ugunduzi huo Serikali ya Uganda ilianza kutafuta njia ya kusafirisha mafuta hayo kwa njia ya bomba (*Pipeline Route*) kutoka eneo la Kabale, Nchini Uganda kwenda kwenye Soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchambua njia ya Bomba Serikali ya Uganda ilainisha njia takribani tatu, ikiwemo ile ya kutoka Hoima Nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga, Nchini Tanzania; mchakato na majadiliano mbalimbali baina ya Serikali ya Uganda nan chi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwemo Tanzania, yalifanyika kutathmini njia bora ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 22 hadi 24 Aprili, 2016 Mawaziri wanaosimamia masuala ya Nishati kutoka Nchi za Uganda, Kenya na Tanzania walikutana Jijini Kampala kwa ajili ya kuhitimisha mazungumzo kuhusu njia itakayotumika kutekeleza mradi huo. Mkutano wa Mawaziri ulifuatiwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Uganda, Kenya, Rwanda, Tanzania na Sudan Kusini kuhusu ushoroba wa Kaskazini (*Nothern Corridor Intergration Projects*) uliofanyika tarehe 23 Aprili, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano huo Rais wa Jamhuri ya Uganda, Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, alitangaza rasmi kuwa njia ya kutoka Kabale, Uganda kupitia Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida,

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Dodoma, Manyara hadi Bandari ya Tanga, Tanzania, ndio njia iliyochaguliwa na Serikali ya Uganda katika ujenzi wa mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi yaliyogunduliwa Nchini Uganda kwenda kwenye soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hatua hiyo, tarehe 26 Mei, 2017, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda zilisaini Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (*The Inter-Governmental Agreement between the United Republic of Tanzania and the Republic of Uganda Concerning The Pipeline System of The East African Crude Oil Pipeline Project*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya Serikali ya Uganda kuchagua njia ya bomba la mafuta kupitia nchini Tanzania na kisha kusainiwa kwa mkataba huu isingefanikiwa kama sio juhudhi, umahiri na uongozi thabiti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Watanzania napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanikisha kutekelezwa kwa mradi huu mkubwa wa kimataifa. Aidha, nawapongeza Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalam wote walioshiriki kufanikisha hatua hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki utajumuisha ujenzi wa bomba la mafuta ghafi lenye urefu wa kilometra 1,445 ambapo kati ya hizo kilometra 1,149 zitakuwa upande wa Tanzania na kilometra 299 zitakuwa upande wa Uganda. Bomba hilo litakuwa na kipenyo cha sentimeta 24 na litakuwa na uwezo wa kusafirisha mapipa ya mafuta ghafi 216,000 kwa siku na litapita katika mikoa minane, wilaya 24 na vijiji vipatavyo 124 vya Tanzania Bara. Ujenzi wa bomba hilo unatarajiwa kugharimu takribani Dola za Kimarekani bilioni 3.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu umegawanyika katika Sehemu kuu Nne, ambapo Sehemu

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

ya Kwanza ambayo inahusisha Ibara ya kwanza (1), inaweka masharti ya kuhusu ufanuzi na tafsiri ya maneno yaliyotumika katika mkataba huo, utaratibu wa kuanza kutumika na kuridhiwa kwa mkataba pamoja na masharti mengine ya utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 1(2) (b), inazitaka kila nchi mwanachama kuanza mchakato wa kuridhia mkataba huu ndani ya siku 30 tangu kusainiwa kwa mkataba. Aidha, Ibara ya 1(3) inaweka masharti kuwa kila nchi mwanachama itatunga sheria wezesi ya mradi kwa ajili ya utekelezaji wa mkataba huu iwapo zitaona inafaa. Ibara ya 1(8) inaweka masharti kuwa, kila nchi mwanachama itaingia mkataba na kampuni ya mradi wa bomba (*Host Government Agreement – HGA*) kwa kuzingatia masharti ya mkataba huu na masharti mengine ambayo itaona yanafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Mkataba inaweka masharti kuhusu wajibu wa jumla (*General Obligations*) kwa nchi wanachama na inaaniz Ibara ya pili (2) hadi Ibara ya 15 kama ifuatavyo:-

(i) Ibara ya pili (2) inaweka masharti kuhusu ushirikiano baina ya nchi wanachama zitakazotekeleza mradi husika. Aidha, Ibara hii inaitaka kila nchi kuanzisha Kamati ya Mashauriano ambayo itakuwa ni chombo cha kubadilishana taarifa na kushauriana juu ya masuala ya mkataba huu pamoja na mradi wenyewe. Vilevile Ibara hii inaeleza namna nchi wanachama zitakavyoshirikiana pamoja na kampuni ya mradi kukagua mradi na kubadilishana taarifa kuhusu ukaguzi husika.

(ii) Ibara ya tatu (3) inaainisha masharti kuhusu Haki za Ardhi. Kwa mujibu wa Ibara hii kila nchi mwanachama itatoa ardhi kwa kampuni ya mradi wa bomba kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi husika. Aidha, Ibara hii inazitaka nchi wanachama kuzingatia Sheria za Nchi na za Kimataifa katika ulipaji wa fidia kwa wananchi na kuhakikisha wananchi na wadau wote wanaohusika katika ulipaji wa fidia wanashirikishwa. (*Makofi*)

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

(iii) Ibara ya nne (4) na tano (5) zinaweka masharti yanayoiruhusu Jamhuri ya Uganda kuitisha mafuta ghafi nchini Tanzania kwa kutambua kuwa, Jamhuri ya Uganda haina bahari (*Land Locked*) na kwa kuzingatia Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Sheria ya Bahari, mwaka 1982 (*The United Nations Convention The Law of The Sea*). Aidha, kila nchi mwanachama imepewa wajibu wa kuchukua hatua muhimu na kutoa vibali vinavyotakiwa. Ibara hiyo, imainisha masharti ya kuhusu kutoathiri shughuli za mradi (*Non Interruption of Project Activities*).

(iv) Ibara ya sita (6) inaainisha masharti kuhusu ulinzi na usalama. Kila nchi mwanachama imepewa jukumu na wajibu wa kuhakikisha kuwepo kwa ulinzi na usalama wa miundombinu ya mradi husika kwa kuzingatia sheria za nchi husika na misingi ya haki za binadamu.

(v) Ibara ya saba (7) inawecka masharti kuhusu masuala ya fedha za kigeni (*Foreign Exchange*) ambapo kila nchi mwanachama itatoa na kuongeza vibali vyta mradi kwa kampuni kuhusiana na fedha za kigeni na masuala muhimu ya shughuli za mradi.

(vi) Ibara ya nane (8) inaainisha masharti kuhusu uhuru wa uingizaji au uingiaji wa watu na uingizaji wa bidhaa na huduma (*Freedom of Movement of Person, Goods and Services*) baina ya nchi wanachama kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kwa kuzingatia sheria za nchi husika na mipango ya ushiriki wa wazawa na ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani (*National Content Plans*).

(vii) Ibara ya tisa (9) inaeleza kuhusu ushiriki wa wazawa na ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani (*National Content*). Ibara hii inazitaka nchi wanachama kwa kushirikiana na kampuni ya mradi wa bomba kuandaa mpango wa kuwawezesha wazawa na makampuni ya ndani kushiriki katika mradi (*National Content Plan*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huo utahakikisha kuwa mradi unatumia bidhaa na huduma mbalimbali

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

pamoja na rasilimali watu kutoka nchi husika. Aidha, kampuni ya mradi itatakiwa kutoa mafunzo ya kitaalam kuhusu uendeshaji wa bomba la kusafirisha mafuta na kuhamasisha ujuzi wa kiufundi, kuhamisha ujuzi wa kiufundi (*Transfer of Technology*) kwa wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mpango huo utapaswa kuonesha fursa zilizopo kwenye mradi kwa kuzingatia ratiba ya utekelezaji katika kipindi cha ujenzi na uendeshaji ili wazawa waweze kufahamu fursa mbalimbali zilizopo kwenye mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo bidhaa au huduma zinazohitajika hazipatikani katika nchi wanachama basi, kampuni ya mradi wa bomba itaruhusiwa kutumia mzabuni wa nje kwa kigezo kuwa mzabuni huyo anahuisha wazawa katika utekelezaji wa shughuli husika, ili kuwajengea uwezo.

(viii) Ibara ya 10 inaipatia kampuni ya mradi haki ya kumiliki mafuta ghafi katika mradi wa bomba (*Title and Ownership of Petroleum in the EACOP System*).

(ix) Ibara ya 11 inaainisha masharti kuhusu muundo, umiliki na uendeshaji wa mradi. Ibara hii pamoja na mambo mengine inaelekeza kuwa mradi wa bomba utaanishwa na kuendeshwa na sekta binafsi kupitia kampuni maalum ya mradi. Kampuni hiyo, inaundwa na wanahisa na kutoa fursa kwa Serikali zote mbili au taasisi zake kuwa na hisa katika kampuni hiyo. Aidha, kila mwanahisa atawajibika kugharamia hisa zake kwa mujibu wa mkataba wa wanahisa utakaointingiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara hii pia, inatoa fursa kwa Serikali ya Tanzania kufanya majadiliano na kampuni ya mradi wa bomba kuhusu uendeshaji wa Bandari ya Tanga katika eneo la Chongoleani.

(x) Ibara ya 12 inatoa fursa kwa nchi wanachama kutumia bomba hilo endapo kutakuwa na ugunduzi wa mafuta katika maeneo mengine. Vilevile Ibara hii inatoa fursa

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

kwa nchi jirani kutumia bomba hilo kusafirisha mafuta kwa kuzingatia vigezo vitakavyowekwa kwenye Mkataba wa HGA.

(xi) Ibara ya 13 inaweka masharti kuhusu vibali na leseni zitakavyotolewa na nchi wanachama katika utekelezaji wa mradi wa bomba.

(xii) Ibara ya 14 inaainisha masharti yanayozitaka nchi wanachama kutotaifisha uwekezaji au mali za mradi wa bomba (*Expropriation*). Hata hivyo, Ibara hiyo inatoa fursa kwa nchi wanachama kutaifisha mali za mradi wa bomba iwapo itakuwa ni kwa manufaa ya umma na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi husika.

(xiii) Ibara ya 15 inaweka masharti kuhusu masuala ya mazingira, Jamii, usalama kazini, viwango vya kiufundi na haki za wafanyakazi. Aidha, Ibara hii inazitaka nchi wanachama kushirikiana na kuhakikisha kwamba, kampuni ya mradi inaendesha shughuli zake kwa kuzingatia sheria za nchi husika pamoja na Sheria za Kimataifa zinazohusu masuala ya mazingira, usalama wa watu, uendeshaji wa mitambo na haki za wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Mkataba inahusisha Ibara ya 16 ambayo inaainisha masharti kuhusu mfumo wa kodi (*Fiscal Regime*). Ibara hii inaeleza kuwa, mfumo wa kodi katika mradi huu utakuwa kwa mujibu wa sheria za kodi za nchi mwanachama, kama ilivyoainishwa katika kiambatisho Na. 2 cha mkataba huu. Kiambatisho hicho kimeweka misingi ya uainishaji (*Harmonization*) wa masuala mbalimbali ya kikodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne, inaainisha masharti ya jumla ya mkataba (*Financial Provisions*) na inahusisha Ibara ya 17 hadi Ibara ya 26. Masharti hayo ni pamoja na:-

Uhai wa Mkataba (*State Succession*) Ibara ya 17; kushindwa kutekeleza mkataba kutokana na sababu

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

zisizozuilia yaani *force majeure*, Ibara ya 18; utatuzi wa migogoro, Ibara ya 19; sheria inayoongoza mkataba, Ibara ya 20; marekebisho ya mikataba na kupokea wanachama wapya (*Subsequent Modification and Accessionn*), Ibara ya 21; ukiukwaji wa masharti ya mkataba, Ibara ya 22; muda wa mkataba, Ibara ya 23; kusitisha mikataba ya utekelezaji wa mradi, Ibara ya 24; hifadhi, lugha na viambatisho vya mkataba (*Reservation, Language and Annexes*), Ibara ya 25; na uwasilishaji na usajili mkataba, Ibara ya 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Masharti ya Utatuzi wa Migogoro itakayojiteza wakati wa utekelezaji wa mkataba huu, Ibara ya 19 inaainisha kuwa mgogoro wowote utatatuliwa kwanza kwa njia za kidiplomasia na nchi wanachama kuitia Kamati ya mashauriano na kwamba, iwapo muafaka hautafikiwa mgogoro husika utafikishwa katika Baraza la Usuluhishi kwa mujibu wa Kanuni za Usuluhishi za Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza hilo litakaa sehemu ambayo nchi wanachama watakubaliana. Endapo nchi wanachama zitashindwa kukubaliana basi, baraza hilo litakaa London, Uingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda (*Inter-governmental Agreement between United Republic of Tanzania and Republic of Uganda Concerning The Pipelines System of The East Africa Crude Oil Pipeline Project (EACOP Project)*) kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda ni Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

**NA KWA KUWA**, Ibara ya 101(1) ya Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inahamasisha nchi wanachama kushirikiana katika utafiti, uendelezaji na utumiaji wa rasilimali mbalimbali za nishati zilizomo katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Ibara ya 101(2)(e) ya Mkataba huo inasisitiza ushirikiano katika ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji wa mafuta na gesi asilia;

**NA KWA KUWA**, jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda zimeanza kushirikiana katika ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania;

**NA KWA KUWA**, katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki kuhusu ushoroba wa Kaskazini (*13<sup>th</sup> Summit of The Northern Corridor Intergration Projects*) ullofanyika Kampala, Uganda tarehe 23 Aprili, 2016 pamoja na mambo mengine ilikubaliwa kuwa bomba la mafuta ghafi litajengwa kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania;

**NA KWA KUWA**, katika utekelezaji wa maamuzi ya mkutano huo tarehe 26 Mei, 2017 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda zilisaini Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (*Inter-governmental Agreement between the United Republic of Tanzania and the Republic of Uganda Concerning The Pipelines System of The East African Crude Oil Pipeline Project*);

**NA KWA KUWA**, Mkataba huo umetambua na kuzingatia Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Sheria ya Bahari wa 1982 (*The UN Convention on The Law of The Sea*) ambao unazipatia nchi zisizokuwa na bahari (*Land Locked*) haki ya kupitisha watu, mizigo, bidhaa na kutumia njia ya usafirishaji kupitia nchi zenyе bahari;

**NA KWA KUWA**, Ibara ya 1(2)(b) ya Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Afrika Mashariki inaelekeza kuwa Mkataba huo utaanza kutumika baada ya kuridhiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi wanachama;

**NA KWA KUWA**, kutokana na Mkataba huu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itanufaika kama ifuatavyo:-

(a) Kuongezeka kwa mapato ta Serikali kutokana na kodi za zuio na kodi ya mapato ya kampuni zitakazotozwa wakati wa ujenzi na uendeshaji wa mradi.

(b) Kuongezeka kwa mapato ya Serikali kwa takribani Dola za Kimarekani 12.2 kwa pipa la mafuta ghafi, litakalosafirishwa kuititia Bandari ya Tanga kulingana na kiwango cha hisa za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Kuongezeka kwa mapato ya Serikali kuititia Bandari ya Tanga wakati wa ujenzi na uendeshaji wa mradi.

(d) Kuimariika kwa huduma mbalimbali katika Bandari ya Tanga kutokana na shughuli za mradi na miundombinu itakayojengwa kwa ajili ya mradi huo ikiwemo barabara.

(e) Kuimariika kwa mahusiano ya kidiplomasia, ulinzi na usalama kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda pamoja na Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla.

(f) Kuchocha shughuli za kiuchumi na kibiashara kwa jamii katika maeneo ambapo bomba la mafuta ghafi litapita.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(g) Kuongezeka kwa fursa za ajira kwa Watanzania ambapo takribani watu 10,000 wataajiriwa wakati wa ujenzi na ajira zipatazo 1,000 wakati wa uendeshaji wa mradi.

(h) Kuongezeka kwa uwekezaji wa nje (*Foreign Direct Investment*) nchini.

(i) Kuchochea shughuli za utafutaji mafuta nchini, hususan katika maeneo ya Ziwa Eyasi na Ziwa Tanganyika.

(j) Kutumika kwa mkuza wa bomba kujenga miundombinu mingine, bomba la kusafirisha gesi asilia na kadhalika litakalowezesha kufunguka kwa ushoroba wa Kaskazini (*Nothern Corridor*) wa biashara, hususan katika Nchi za Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Sudani Kusini.

(k) Kuimarika kwa uwezo na uzoefu wa Watanzania kushiriki katika masuala ya majadiliano, ujenzi na uendeshaji wa miradi ya mabomba ya kusafirisha mafuta.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia yatokanayo na mkataba huu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Nane linaombwa kutafakari mapendekezo yaliyomo katika Azimio hili na Kuazimia Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (*Intergovernmental Agreement between the United Republic of Tanzania and the Republic of Uganda Concerning The Pipeline System of The East African Crude Oil Pipeline Project*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makof*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Deo Ngalawa kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA MAKAMU MWENYEKITI  
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda (*Inter-governmental Agreement Between the United Republic of Tanzania and the Republic of Uganda Concerning the Pipeline System of the East African Crude Oil Pipeline Project*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi la Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda (*Intergovernmental Agreement Between the United Republic of Tanzania and the Republic of Uganda Concerning the Pipeline System of the East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa fasili ya (9) ya Kanuni ya 6, ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya Kanuni ya 7, katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, inalo jukumu la kushughulikia Miswada

ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ilioyo chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Bunge, uliletu kwenye Kamati ya Nishati na Madini hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi la Bomba la Kusafirishia Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda (*Inter-governmental Agreement Between the United Republic Of Tanzania and the Republic Of Uganda Concerning The Pipeline System of the East African Crude Oil Pipeline Project*), ili Kamati iweze kuishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 4 Septemba, 2017, Kamati ilikutana katika Ukumbi wa Utawala Kuu, Chuo kikuu cha Dodoma (*UDOM*) na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekozo la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirishia Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipotekeleza jukumu lake kuhusiana na hoja hii, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(8) na 117(9) kuhusu utaratibu wa Kamati pamoja na kuwaalika wadau. Katika hatua hii, Kamati iliwaalika wadau kwa ajili ya kupata maoni yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda ambao Kamati ilikuwa nao katika kushughulikia hoja hii, wadau wengi hawakuweza kuwasilisha maoni yao na hata ambao waliweza kuwasilisha, waliwasilisha kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishukuru sana Taasisi ya Utawala wa Maliasili (*Natural Resources Governance Institute*) kwa maoni ya msingi iliyowasilisha kwenye Kamati ambayo yametoa mchango mkubwa sana katika kujadili Azimio hili. Nafurahi kutamka kuwa utaratibu huu wa kuwaalika wadau kutoa maoni yao kuhusu hoja inayoshughulikiwa na Kamati, ni wa msingi na ni muhimu kwa jamii ya kidemokrasia kama Tanzania. Aidha, ni utaratibu

unaolisaidia Bunge kuendelea kudhihirisha kwamba ni chombo halisi cha uwakilishi wa wananchi chenye jukumu la kukidhi matarajio yao wakati wa mchakato wa kuridhia mikataba ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati. Ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali muhimu katika uchambuzi wa hoja hii ya Serikali ambayo leo tunawasilisha taarifa yake. Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na:-

Kuangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria za nchi zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya mkataba unaopendekezwa, pamoja na kutafakari kuhusu kiwango cha manufaa au madhara yanayoweza kupatikana kwa nchi kuridhia au kutokuridhia mkataba huu kama ulivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo ya Serikali ambayo yaliwasilishwa na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Kamati ilipitia na kuchambua kikamilifu maudhui ya mkataba huu wa makubaliano baina ya pande mbili husika. Mantiki ya kufanya hivyo ni kuliwezesha Bunge kujiridhisha iwapo taratibu za msingi zimezingatiwa na kuelewa vyema jinsi ambavyo nafasi ya Tanzania katika diplomasia na uhusiano wa kimataifa itaendelea kudumishwa kutokana na hatua ya kuridhia au kutokuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la mkataba huu wa makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda, kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda. Ni katika Kikao cha Kumi na Tatu cha Jumuiya ya Afrika Mashariki, kilichofanyika Kampala - Uganda, tarehe 23 Aprili, 2016, Wakuu wa Nchi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda walikutana na kuanzisha mazungumzo

ambayo hatimaye yalizaa uamuzi wa kushirikiana katika ujenzi na uendeshaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza uamuzi huo, nchi hizi mbili zimeazimia kutekeleza uwekezaji na uendeshaji wa mradi huo kwa kuzingatia Sheria za Kimataifa katika utaalam, mazingira na maslahi ya kijamii, pamoja na kuhamasisha na kulinda uwekezaji ili kuleta ufanisi katika maendeleo, umiliki na utekelezaji wa muda mrefu wa mifumo ya nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo ya mtoa hoja, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu hali iliyofikiwa katika mkataba huu kwa kuangalia kama unayo nguvu ya kisheria na kubaini kuwa, kifungu cha 2(c) cha Sehemu B ambayo inahusu *Corporate Income Tax*, katika kiambatisho cha pili cha mkataba, kinahitaji kutazamwa kwa umakini kwani kinaweza kisiwe na maslahi kwa Taifa iwapo kampuni inayotekeleza mradi itakosa uaminifu na kutangaza kupata hasara kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hicho kinaruhusu hasara iliyobainika kuhusiana na utekelezaji wa mradi kabla, wakati au baada ya kipindi cha msamaha wa kodi kusogezwa mbele katika mwaka wa fedha unaofuata iwapo haikufanyiwa kazi katika mwaka wa fedha husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ina mashaka juu ya Ibara ya saba (7) ya mkataba huu ambayo inahusu fedha za kigeni (*foreign exchange*). Kwa mujibu wa kifungu hiki, kampuni itakayokuwa inatekeleza mradi inaruhusiwa kuhamisha fedha kwenda nje ya Uganda na Tanzania bila kizuizi na kubakiza fedha katika nchi hizo ambazo fedha itapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona kama Ibara hii inakinzana na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili [*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty)*]ya Mwaka 2017 ambayo inaruhusu

fedha zinazotokana na mgawo wa faida tu ndiyo ziwekwe nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa mkataba huu ambao ulisainiwa tarehe 26 Mei, 2017 Kampala, Uganda baada ya makubaliano baina ya nchi mbili za Tanzania na Uganda, unaenda sambamba na malengo yaliyobainishwa katika Ibara ya 101(1) ya Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, inayohamasisha nchi wanachama kushirikiana katika utafiti, uendelezaji na utumiaji wa rasilimali mbalimbali za nishati zilizomo katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Vilevile Ibara ya 101(2)(e) ya mkataba huo inasistiza kuhusu ushirikiano katika ujenzi wa mabomba ya usafirishaji wa mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kutambua kwamba Tanzania na Uganda ni mionganini mwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyooundwa tarehe 30 Novemba, 1999 ambayo mionganini mwa malengo ya kuanzishwa kwake ni kuimarishta ushirikiano kati ya wanachama kwenye maeneo ya kisiasa, Kiuchumi, kijamii, kiteknolojia, utafiti, ulinzi na masuala ya kisheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ilizingatia ushirikiano baina ya nchi hizi na faida za uwekezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi wakati wa kuifanyia kazi hoja iliyopo mbele ya Bunge hili kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inakuwa makini wakati wa utekelezaji wa mkataba huu kwa kuzingatia mustakabali wa manufaa ya Kiuchumi kwa Taifa kwa ujumla na kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo mradi huu utatekelezwa. Aidha, Serikali ihakikishe wananchi hao wanashirikishwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuhamasishwa kutumia fursa za kiuchumi zitakazojitokeza kutokana na utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa fidia ya ardhi kwa wananchi ambao watalazimika kuachia maeneo yao ili kupisha utekelezaji wa mradi. Aidha, malipo hayo yafanyike kikamilifu kwa wakati na kwa viwango stahiki ili kuepusha migogoro ambayo inaweza kujitokeza na kuathiri utekelezaji wa mradi kwa muda uliopangwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mionganini mwa mambo yanayoweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya uwekezaji ni kukosekana kwa mazingira ya usalama na utulivu katika maeneo ambayo miradi hiyo inatekelezwa, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yote ambayo mradi huu utatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara ya kwanza kwa nchi yetu kutekeleza mradi wa thamani kubwa na wa aina hii, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatoa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya umuhimu wa mradi huu kwa maendeleo ya Taifa letu hivyo wanapaswa kuuthamini na kushiriki katika kuulinda na kuutunza ili uweze kuwa na manufaa kwao na kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wajumbe wameonesha mashaka kuhusu kifungu cha 2(c) cha sehemu B ambayo inahusu *Corporate Income Tax*, katika Kiambatisho cha Pili cha Mkataba, kwani kinaweza kutumiwa na wawekezaji wasio waaminifu kuihujumu nchi yetu. Kifungu hicho kinaruhusu hasara iliyobainika katika utekelezaji wa mradi kabla, wakati au baada ya kipindi cha msamaha wa kodi kusogezwa mbele katika mwaka wa fedha unaofuata iwapo haikufanyiwa kazi katika mwaka wa fedha husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali iwe makini na kifungu hiki wakati wa utekelezaji wa mradi ili kampuni zitakazohusika kutekeleza mradi zisijaribu kukitumia kutangaza kupata hasara kila mwaka na hivyo kuikoseshwa Serikali mapato stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Ibara ya saba (7) ya mkataba huu inairuhusu kampuni itakayotekeleza mradi kusafirisha fedha nje ya Uganda na Tanzania na kuzihifadhi huko bila kizuizi chochote, Kamati inaishauri Serikali kuangalia kwa umakini Ibara hii ili kuepuka kukinzana na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili [*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty)*] ya Mwaka 2017 ambayo inazuia wawekezaji kusafirisha fedha kwenda nje ya nchi isipokuwa zile zinazotokana na mgawo wa faida iliyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudzi zake na umahiri aliouonesha katika kuhakikisha Tanzania inapata fursa ya mradi huu mkubwa wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), ambao utachangia kwa kiasi kikubwa kufungua milango ya kiuchumi kwa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, niwashukuru sana Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa uongozi wenu mahiri na miongozo ambayo imeiwezesha Kamati kushughulikia kikamilifu hoja uliyoleta kwenye Kamati hadi kufikia hatua hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Niwashukuru pia Wenyevit i wote wa Bunge kwa uratibu na usimamizi mzuri wa shughuli za Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt Medard Kalemani, Makatibu Wakuu pamoja na wataalam wote wa Wizara hii kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati wa kushughulikia Azimio hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati kabisa, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuandaa maoni juu ya Azimio hili

ambayo nimeyawalisha mbele ya Bunge hili Tukufu. Majina yao naomba yaingie moja kwa moja kwenye Kumbukumbu za Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bi. Mwanahamisi Munkunda na Bi. Felister Mgonja pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Kokuwaisa Gondo kwa kuratibu shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
NISHATI NA MADINI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA  
MKATABA WA KIMATAIFA WA MRADI WA UJENZI WA  
BOMBA LA KUSAFIRISHA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA  
MASHARIKI KATI YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO  
WA TANZANIA NA SERIKALI YA JAMHURI YA UGANDA  
(*INTERGOVERNMENTAL AGREEMENT BETWEEN THE UNITED  
REPUBLIC OF TANZANIA AND THE REPUBLIC OF UGANDA  
CONCERNING THE PIPELINE SYSTEM OF THE EAST AFRICAN  
CRUDE OIL PIPELINE (EACOP) PROJECT*) KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi la Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda (*Intergovernmental Agreement Between the United*

*Republic of Tanzania and the Republic of Uganda concerning the Pipeline System of the East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project).*

Kwa mujibu wa fasili ya (9) ya Kanuni ya 6, ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya Kanuni ya 7, katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, inalo jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

Aidha, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Bunge, ulileta kwenye Kamati ya Nishati na madini, Hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi la Bomba la Kusafirishia Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda (*Intergovernmental Agreement Between The United Republic Of Tanzania And The Republic Of Uganda Concerning The Pipeline System Of The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project*), ili Kamati iweze kuishughulikia.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 04 Septemba, 2017 Kamati ilikutana katika Ukumbi wa Utawala Kuu, Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi la Bomba la Kusafirishia Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda (*Intergovernmental Agreement Between The United Republic Of Tanzania and The Republic of Uganda Concerning The Pipeline System of The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project*).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipotekeleza jukumu lake kuhusiana na hoja hii, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (8) na 117 (9) kuhusu utaratibu wa Kamati pamoja na kuwaalika wadau. Katika hatua hii, Kamati iliwaalika wadau kwa ajili ya kupata maoni yao, hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda ambao Kamati ilikuwa nao katika kushughulikia

hoja hii, Wadau wengi hawakuweza kuwasilisha maoni yao, na hata ambao waliweza waliwasilisha kwa njia ya maandishi tu.

Kamati inaishukuru sana Taasisi ya Utawala wa Maliasili (Natural Resources Governance Institute - NRG) kwa maoni ya msingi iliyowasilisha kwenye Kamati ambayo yametoe mchango mkubwa sana katika kujadili Azimio hili. Nafurahi kutamka kuwa Utaratibu huu wa kuwaalika wadau kutoa maoni yao kuhusu hoja inayoshughulikiwa na Kamati, ni wa msingi na ni muhimu kwa Jamii ya Kidemokrasia kama Tanzania. Aidha, ni utaratibu unaolisaidia Bunge kuendelea kudhihirisha kwamba, ni chombo halisi cha uwakilishi wa wananchi chenye jukumu la kukidhi matarajio yao wakati wa mchakato wa kuridhia mikataba ya kimataifa.

## **1.1 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali muhimu katika uchambuzi wa hoja ya hii ya Serikali, ambayo leo tunawasilisha Taarifa yake. Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na kuangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Sheria za nchi zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya Mkataba unaopendekezwa, pamoja na kutafakari kuhusu kiwango cha manufaa au madhara yanayoweza kupatikana kwa nchi yetu kuridhia au kutokuridhia Mkataba huu kama ulivyo.

Pamoja na maelezo ya Serikali ambayo yaliwasilishwa na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Kamati ilipitia na kuchambua kikamilifu maudhui ya Mkataba huu wa makubaliano baina ya pande mbili husika. Mantiki ya kufanya hivyo ni kuliwezesha Bunge kujiridhisha iwapo taratibu za msingi zimezingatiwa na kuelewa vyema jinsi ambavyo nafasi ya Tanzania katika diplomasia na uhusiano wa kimataifa itaendelea kudumishwa kutokana na hatua ya kuridhia au kutokuridhia Mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika**, chimbuko la Mkataba huu wa makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda, kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Mradi wa Ujenzi la Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda (*Intergovernmental Agreement Between The United Republic of Tanzania and The Republic of Uganda Concerning The Pipeline System of The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project*), ni katika Kikao cha kumi na tatu cha Jumuiya ya Afrika Mashariki, kilichofanyika Kampala Uganda, tarehe 23 Aprili, 2016. Wakuu wa nchi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda walikutana na kuanzisha mazungumzo ambayo hatimaye yalizaa uamuzi wa kushirikiana katika ujenzi na uendeshaji wa mradi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi.

Katika kutekeleza uamuzi huo nchi hizi mbili zimeazimia kutekeleza uwekezaji na uendeshaji wa mradi huo kwa kuzingatia Sheria za Kimataifa katika utaalami, mazingira na maslahi ya kijamii, pamoja na kuhamasisha na kulinda uwekezaji, ili kuleta ufanisi katika maendeleo, umiliki na utekelezaji wa muda mrefu wa mifumo katika nchi zao.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo ya Mto hoja, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu hali iliyofikiwa katika Mkataba huu kwa kuangalia kama unayo nguvu ya kisheria na kubaini kuwa, kifungu cha 2(c) cha Sehemu B ambayo inahusu *Corporate Income Tax*, katika Kiambatisho cha Pili cha Mkataba, kinahitaji kutazamwa kwa umakini kwani kinaweza kisiwe na maslahi kwa taifa iwapo kampuni inayotekeliza mradi itakosa uaminifu na kutangaza kupata hasara kila mwaka.

Kifungu hicho kinaruhusu hasara iliyobainika kuhusiana na utekelezaji wa mradi kabla, wakati au baada ya kipindi cha msamaha wa kodi kusogezwa mbele katika mwaka wa fedha unaofuata iwapo haikufanyiwa kazi katika mwaka wa fedha husika.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati ina mashaka juu ya Ibara ya 7 ya Mkataba huu ambayo inahusu fedha za kigeni "foreign exchange". Kwa mujibu wa kifungu hiki kampuni itakayokuwa inatekeleza mradi inaruhusiwa kuhamisha fedha kwenda nje ya Uganda na Tanzania bila kizuizi na kubakiza fedha katika nchi hizo ambazo fedha itapelekwa. Kamati inaona kama ibara hii inakinzana na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili [The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty)] ya Mwaka 2017 ambayo inaruhusu fedha zinazotokana na mgawo wa faida tu ndiyo ziwekwe nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa Mkataba huu ambao ulisainiwa tarehe 26 Mei, 2017 Kampala, Uganda baada ya makubaliano baina ya nchi mbili za Tanzania na Uganda, unaenda sambamba na malengo yaliobalishwa katika Ibara ya 101 (1) ya Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, inayohamasisha nchi wanachama kushirikiana katika utafiti, uendelezaji na utumiaji wa rasilimali mbalimbali za Nishati zilizomo katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Vilevile Ibara ya 101 (2) (e) ya Mkataba huo inasisitiza kuhusu ushirikiano katika ujenzi wa mabomba ya usafirishaji wa mafuta na gesi asilia.

Aidha, kwa kutambua kwamba, Tanzania na Uganda ni mionganoni mwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliyoundwa tarehe 30 Novemba, 1999 ambayo mionganoni mwa malengo ya kuanzishwa kwake ni kuimarissha ushirikiano kati ya nchi wanachama kwenye maeneo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiteknolojia, utafiti, ulinzi na masuala ya kisheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ilizingatia ushirikiano baina ya nchi hizi na faida za uwekezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi wakati wa kuifanya kazi hoja iliyopo mbele ya Bunge hili kwa sasa.

## **1.2 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inakuwa makini wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu, kwa kuzingatia mustakabali wa manufaa ya kiuchumi kwa Taifa kwa ujumla na kwa Wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo Mradi huu utatekelezwa. Aidha, Serikali ihakikishe wananchi hao wanashirikishwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuhamasishwa kutumia fursa za kiuchumi zitakazojitokeza kutokana na utekelezaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa fidia ya ardhi kwa Wananchi ambao watalazimika kuachia maeneo yao ili kupisha utekelezaji wa mradi. Aidha, malipo hayo yafanyike kikamilifu kwa wakati na kwa viwango stahiki ili kuepusha migogoro ambayo inaweza kujitokeza na kuathiri utekelezaji wa mradi kwa muda uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa mionganii mwa mambo yanayoweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya uwekezaji ni kukosekana kwa mazingira ya usalama na utulivu katika maeneo ambayo miradi hiyo inatekelezwa, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yote ambayo mradi huu utatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa ni mara ya kwanza kwa nchi yetu kutekeleza mradi wa thamani kubwa na wa aina hii, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatoa elimu ya kutosha kwa Wananchi juu ya umuhimu wa mradi huu kwa maendeleo ya Taifa letu hivyo wanapaswa kuuthamini na kushiriki katika kuulinda na kuutunza ili uweze kuwa na manufaa kwao na kwa vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Wajumbe wameonesha mashaka kuhusu kifungu cha 2(c) cha Sehemu B ambayo inahusu *Corporate Income Tax*, katika Kiambatisho cha Pili cha Mkataba, kwani kinaweza kutumiwa na Wawekezaji wasio waaminifu kuihujumu nchi yetu. Kifungu hicho kinaruhusu hasara iliyobainika katika utekelezaji wa mradi kabla, wakati au baada ya kipindi cha msamaha wa

kodi kusogezwa mbele katika mwaka wa fedha unaofuata iwapo haikufanyiwa kazi katika mwaka wa fedha husika.

Kamati inaishauri Serikali iwe makini na kifungu hili wakati wa utekelezaji wa mradi ili kampuni zitakazohusika kutekeleza mradi zisijaribu kukitumia kutangaza kupata hasara kila mwaka, na hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Ibara ya 7 ya Mkataba huu inairuhusu Kampuni itakayotekeleza mradi kusafirisha fedha nje ya Uganda na Tanzania na kuzihifadhi huko bila kizuizi chochote, Kamati inaishauri Serikali kuangalia kwa umakini ibara hii ili kuepuka kukinzana na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili [The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty)] ya Mwaka 2017 ambayo inazuia wawekezaji wa kusafirisha fedha kwenda nje ya nchi isipokuwa zile zinazotokana na mgawo wa faida iliyopatikana.

## 2.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudzi zake na umahiri aliuonesha katika kuhakikisha Tanzania inapata fursa ya mradi huu mkubwa wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima Uganda hadi Tanga Tanzania, ambao utachangia kwa kiasi kikubwa kufungua milango ya kiuchimi kwa nchi yetu.

Kwa namna ya pekee, nakushukuru sana wewe binafsi kwa Uongozi wako mahiri na miongozo ambayo imewezesha Kamati kushughulikia kikamilifu hoja uliyoleta kwenye Kamati hadi kufikia hatua hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Niwashukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa uratibu na usimamizi mzuri wa shughuli za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru pia Naibu Waziri wa Nishati na Madini Mhe. Dkt Medard Kalemani (Mb), Makatibu

Wakuu pamoja na wataalam wote wa Wizara hii kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati wa kushughulikia Azimio hili.

Kwa moyo wa dhati kabisa, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuandaa maoni juu ya Azimio hili ambayo nimeyawalisha mbele ya Bunge hili Tukufu. Majina yao ni kama yanavyoonekana katika orodha hapa chini, na kwa ruhsa yako naomba yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

i.	Mhe. Doto Mashaka Biteko, Mb	-	Mwenyekiti
ii.	Mhe. Deogratius Ngalawa, Mb		M/Mwenyekiti
iii.	Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb		Mjumbe
iv.	Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb		"
v.	Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb		"
vi.	Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb		"
vii.	Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb		"
viii.	Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb		"
ix.	Mhe. Stella Ikupa Alex, Mb		"
x.	Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb		"
xi.	Mhe. Mauled Said Abdalah Mtulia, Mb		"
xii.	Mhe. Desderius John Mipata, Mb		"
xiii.	Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb		"
xiv.	Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb		"
xv.	Mhe. Joyce Bitta Sokombi, Mb		"
xvi.	Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb		"
xvii.	Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb		"
xviii.	Mhe. Zainabu Mussa Bakar, Mb		"
xix.	Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb		"
xx.	Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb		"
xxi.	Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb		"
xxii.	Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb		"
xxiii.	Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb		"
xxiv.	Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb		"
xxv.	Mhe. John Wegesa Heche, Mb		"
xxvi.	Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb		"

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bi Mwanahamisi Munkunda na Bi Felister Mgonja pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi Kokuwaisa Gondo kwa kuratibu shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Deogratius Ngalawa, (Mb)  
M/MWENYEKITI  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
NISHATI NA MADINI**  
7 Septemba, 2017

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitamwita Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Nishati na Madini.

**MHE. DEVOTA M. MINJA (K.n.y. MHE. JOHN J. MNYIKA - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe mezani maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba Bainaha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda Kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika ya Mashariki (*Inter-governmental Agreement Between the United Republic of Tanzania and the Republic of Uganda Concerning the Pipeline System of the East African Crude Oil Pipeline*). Yanatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(c) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kutoa pole na pongezi nyingi kwa Waheshimiwa Wabunge toka pande shindani na chama tawala kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi ambacho Bunge letu lilikuwa mapumzikoni lakini Wabunge mlikuwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa heshima kubwa nichukue fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano mkubwa wakati wa kutekeleza majukumu yao ya Kibunge ndani ya Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba bomba hili la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda hadi mwambao wa Bahari ya Hindi ilikuwa ni kazi iliyo husu zaidi ushawishi mpana, kwani kulikuwa na ushindani mkubwa kutoka kwa ndugu zetu wa nchi jirani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bomba hili la mafuta ghafi la Afrika ya Mashariki litakuwa na urefu wa kilometa 1,445. Kati ya kilometa hizo kwa upande wa Tanzania inazo kilomita 1,149 zilizo katika Mikoa nane na katika Wilaya 24 za Tanzania Bara na kilometa 296 zillizobakia zipo upande wa Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbinu za kushinda mradi mkubwa kama huu bila ya kuwepo kwa zabuni ni dhahiri lazima vivutio vikubwa viliwekwa mezani kama ambavyo maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanavyosomeka. Hoja ya msingi, je, vivutio hivyo vilivyotolewa ili kupata mradi huo vinawiana na manufaa yatakayopatikana kwa upande wa watu wetu? Ingekuwa ni vyema Bunge letu hasa ngazi ya Kamati ikapatiwa taarifa ya upembuzi yakinifu kwa mradi huu ili hapo baadaye tusijeanza kulaumiana sisi Wabunge ambaao tumebariki jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa utangulizi huo wa jumla, naomba sasa kuangalia baadhi ya vipengele vya mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya kwanza (1), kifungu cha nne (4) cha mkataba kinaeleza kuwa hakuna sheria ya ndani au ya kimataifa itakayokuwa juu ya mkataba huu. Katika mkutadha huo huo ukiangalia Ibara ya 19 inayohusu utatuzi wa migogoro kuhusiana na mkataba huu kwa pande husika, kifungu cha pili (2) kinatamka wazi kwamba

wasuluhishi watakutana London na hawatatoka mionganoni mwa pande hizi zilizofungiana mkataba huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuweka kumbukumbu sawa ni kwamba Bunge hili tarehe 4 Julai, 2017, lilipitisha Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili ya mwaka 2017. Katika sheria hiyo, Sehemu ya Tatu, kifungu cha 11 kinapiga marufuku mashauri yote yanayohusu utajiri wa rasilimali na maliasili zetu kufanyika nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa tafsiri ya maneno ya sheria hiyo ardhi ni sehemu ya rasilimali asili za nchi yetu na katika uwepo wa bomba la mafuta ardhi binafsi na za umma zitakumbwa na kadhia hiyo ya upishwaji wa bomba la mafuta. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, ni kwamba mkataba huo ambao Mheshimiwa Rais alisaini (*Instrument of Power*) tarehe 24 Mei, 2017 na kumuidhinisha Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria kusaini mkataba huu kwa niaba ya Serikali. Tarehe 26 Mei, 2017, Mheshimiwa Profesa Kabudi alisaini kwa niaba ya Serikali. Aidha, mwezi wa Sita, Serikali kupitia Mawaziri wa Katiba na Sheria ikaleta Miswada miwili iliyohusu umiliki wa rasilimali na maliasili za nchi vifungu tajwa kuhusu kuzuia mashauri kufanyika nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vifungu hivyo vimeelezea kwa kirefu. Hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani, ni kwa nini Bunge linaingizwa kwenye mtego kwa kutunga sheria zinazokinzana? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 2(3)(a) inasema kwamba, *any confidential information supplied by one state party to another shall not be further disclosed by the receiving state party without prior consent of the supplying state party.* Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kifungu hiki ni kifungu hatari sana kwani hata Bunge kama taasisi inayowakilisha wananchi haitakuwa na haki ya kuona taarifa hizo hadi pale kibali cha kufanya hivyo kitolewe na nchi, shirika au mkataba huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, mtazamo wetu, ni dhahiri mkataba huu unaweza kuwa kama ile mikataba ya uchimbaji wa madini illyosainiwa miaka zaidi ya kumi iliyopita ambayo makosa yake yanaonekana hivi sasa na baadhi ya watendaji waliwajibishwa wakiwemo Mawaziri. Mikataba ya madini na utafiti wa mafuta imekuwa ikifanywa kwa siri kwa kiasi kikubwa na kuwa watendaji wa taasisi moja ya Serikali walifikia hatua ya kuwekwa ndani na Kamati moja ila bado hawakuwa tayari kutoa mikataba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunatoa angalizo kuwa mkataba huu usiwe kama mikataba waliyokuwa wanaitumia wakoloni na wazee wetu wa makabila mbalimbali ili kuchukua rasilimali zilizokuwepo kwa njia ya udanganyifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tatu (3) ya mkataba inayohusu haki ya kumiliki ardhi inasema kwamba kila nchi mwanachama itachukua hatua stahiki kuhakikisha kwamba utwaaji wa ardhi na umilikishwaji wa ardhi hiyo kwa kampuni ya mradi utalindwa na nchi wanachama lakini kwa kadhia nzima ya utwaaji huo wa ardhi ni lazima uwe kwenye mazingira ambayo ni kwa manufaa ya kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaeleza kuwa, ardhi ni rasilimali inayopanda thamani kila kukicha na hivyo mauzo ya ardhi za vijiji kwa wananchi ni lazima yafanywe kwa kuangalia thamani ya soko na si vinginevyo. Kinyume cha hapo hujuma kwa mradi inaweza kutokea kutokana na wamiliki kutokuridhika na hivyo kutokutoa ushirikiano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya nne (4) inatoa uhuru wa kusafirisha mafuta ya Tanzania na kutoa haki zote kwa nchi ya Uganda hadi bandarini, kwa maana nyingine ni kuwa Bandari ya Chongoleani, Tanga ni mali ya Uganda na pia haki hiyo ambayo Tanzania tumeitoa kwa Uganda inaenda pia kwa wamiliki wa meli zitakazokuja kununua mafuta. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu ni kwa

jinsi gani Mamlaka ya Bandari itajihusisha au itahusika na biashara hii ya kutoa huduma za meli za mafuta zitakazokuwa zinatia nanga katika bandari hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 inahusu umiliki wa mafuta yaliyomo kwenye bomba. Kambi Rasmi ya Upinzani inashindwa kuelewa ni kwa nini vifungu vya Ibara hiyo vinaeleza kuwa hakuna mshirika atakayekuwa na haki ya kudai mafuta na mali yake bali ni yule atakayefanya utaratibu wa kibiashara na mmiliki wa meli kwa kushirikiana na makampuni ya pamoja yaliyoundwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya pamoja ambayo inapewa mamlaka makubwa katika biashara hii ya bomba, mkataba haukusema kuwa itasajiliwa wapi katika mataifa haya wanachama. Kambi Rasmi ya Upinzani ina wasiwasi kwamba kampuni hii inaweza kusainiwa au kusajiliwa *offshore* kwenye nchi ambazo hazikuhusiana kabisa na ulipaji wa kodi za nchi maarufu kama uchakachuaji na utunzaji wa fedha chafu kama baadhi ya makampuni yaliyoingizwa hapa nchini na kuchukua rasilimali zetu kama ile ya Meremeta ilivyokuwa na mwisho wa siku kubaki kulaumiana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufanuzi wa kina kuhusu umiliki wa mafuta hayo yanayotoka Uganda na kusafirishwa nje kuitia bandari mpya itakayojengwa katika Kijiji cha Chongoleani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona lingekuwa ni jambo la busara kwa Bunge hili kutokuridhia Azimio hili hadi pale mikataba itakapopitiwa vizuri na kujiridhisha kuhusiana na vifungu ambavyo tunaona vinaathiri Watanzania moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA BAINA YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA SERIKALI YA JAMHURI YA UGANDA KUHUSU MRADI WA UJENZI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA YA MASHARIKI (INTERGOVERNMENTAL AGREEMENT BETWEEN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA AND THE REPUBLIC OF UGANDA CONCERNING THE PIPELINE SYSTEM OF THE EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE (EACOP) Project) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

"Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6) (c ) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016"

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii kutoa pole na pongezi nyingi kwa Waheshimiwa wabunge toka upande shindani na chama tawala kwa kazi kubwa mliyoifanya katika kipindi ambacho Bunge letu ilikuwa mapumzikoni lakini wabunge mlikuwa kazini.

**Mheshimiwa Spika**, Pia kwa heshima kubwa nichukue fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano mkubwa wakati wa kutekeleza majukumu yetu ya kibunge ndani ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, ni kweli kwamba Bomba hili la kusafirishia mafuta ghafi kutoka Uganda hadi mwambao wa Bahari ya Hindi ilikuwa ni kazi iliyohusu zaidi ushawishi mpana, kwani kulikuwa na ushindani mkubwa kutoka kwa ndugu zetu wa nchi jirani.

**Mheshimiwa Spika**, bomba hili la mafuta Ghafi la Afrika ya Mashariki litakuwa na urefu wa kilometra 1,445; katika kilometra hizo kwa upande wa Tanzania inazo kilomita 1,149 zilizo katika mikoa 8 na katika wilaya 24 za Tanzania Bara na kilometra 296 zilizobakia zipo upande wa Uganda.

**Mheshimiwa Spika**, mbinu za kushinda mradi mkubwa kama huu bila ya kuwepo kwa zabuni ni dhahiri lazima vivutio (incentives) vikubwa viliwekwa mezani kama ambavyo maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanavyosomeka.

Hoja ya msingi je vivutio hivyo viliviyotolewa ili kupata mradii huo vinawiana na manufaa yatakayopatikana kwa upande wetu? Ingekuwa ni vyema Bunge letu hasa ngazi ya kamati ikapatiwa taarifa ya upembuzi yakinifu kwa mradii huu ili hapo baadae tusijeanza kulaumiana sisi wabunge ambao tumebariki jambo hili.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa utangulizi huo wa jumla, naomba sasa kuangalia baadhi ya vipengele vyatubaki. Mkatiba huu.

**Mheshimiwa Spika**, ibara ya 1 kifungu cha 4 cha mkataba kinaeleza kuwa hakuna sheria ya ndani au ya kimataifa itakayokuwa juu ya mkataba huu. Katika mkutadha huo huo ukiangalia Ibara ya 19 inayohusu utatuzi wa migogoro kuhusiana na mkataba huu kwa pande husika, kifungu cha 2 kinatamka wazi kwamba wasuluuhishi watakutana London na hawatatoka miongoni mwa pande hizi zilizofungiana mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuweka Kumbukumbu sawa ni kwamba Bunge hili tarehe 04/07/2017 lilipitisha sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na maliasili ya mwaka 2017 **(The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) ACT,2017)**. Katika sheria hiyo sehemu ya III kifungu cha 11 kinapiga marufuku mashauri yote yanayohusu utajiri wa rasilimali na maliasili zetu ni marufuku kufanyika nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa tafsiri ya maneno ya sheria hiyo ardhi ni sehemu ya rasilimali asili za nchi yetu, na katika uwepo wa bomba la mafuta ardhi binafsi na za umma zitakumbwa na kadhia hiyo ya upishwaji wa bomba la mafuta.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mantiki hiyo ni kwamba Mkataba huu ambao Mheshimiwa Rais alisaini "instrument of Power" tarehe 24/ 05/2017 akimuidhinisha Prof. Paramagamba John Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria kusaini Mkataba huu kwa niaba ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 26/05/2017 Mheshimiwa Prof. Kabudi alisaini kwa niaba ya Serikali.

Aidha, Mwezi wa sita, Serikali kupitia kwa Waziri wa Katiba na sheria ikaleta miswada miwili inayohusu umiliki wa rasilimali na Maliasili za nchi na vifungu tajwa kuhusu kuzuia mashauri kufanyika nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vifungu hivyo vimeelezea kwa kirefu. Hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni kwa nini Bunge linaingizwa kwenye mtego wa kutunga sheria zinazokinzana?

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 2 kifungu cha 3 (a) kinachosema kwamba;

*"Any confidential information supplied by one state Party to another shall not be further disclosed by the receiving state Party without the prior consent of the supplying State Party"*

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kifungu hiki ni kifungu hatari sana kwani hata Bunge kama taasisi inayowakilisha wananchi haitakuwa na haki ya kuona taarifa hizo hadi pale kibali cha kufanya hivyo kitolewe na nchi mshirika wa Mkataba huu. Hivyo basi kwa mtazamo wetu ni dhahiri mkataba huu unaweza kuwa kama ile Mikataba ya Uchimbaji wa Madini iliyo sainiwa miaka zaidi ya kumi iliyopita ambayo makosa yake yanaonekana sasa na baadhi ma baadhi ya watendaji kuwajibishwa wakiwemo Mawaziri. Mikataba ya Madini na utafiti wa mafuta imekuwa ikifanywa kwa siri kwa kiasi kikubwa kuna watendaji wa taasisi moja ya Serikali walifikia kuwekwa ndani na Kamati moja ila bado hawakuwa tayari kutoa mikataba. Aidha, tunatoa angalizo kuwa mkataba huu usiwa kuwa kama mikataba waliyokuwa wanaitumia wakoloni kwa wazee wetu wa makabila mbalimbali ili kuchukua rasilimali zilizokuwepo kwa njia ya udanganyifu.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 3 ya Mkataba inayohusu Haki ya kumilki Ardhi, inasema kwamba kila nchi mwanachama itachukua hatua stahiki kuhakikisha kwamba

utwaaji wa ardhi na umilikishwaji wa ardhi hiyo kwa Kampuni ya mradi utalindwa na nchi mwanachama, katika kadhia nzima ya utwaaji huo wa ardhi na ni lazima uwe kwenye mazingira ambayo ni kwa manufaa kwa Kampuni.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaelewa kuwa ardhi ni rasilimali inayopanda thamani kila kukicha, hivyo mauzo ya ardhi za vijiji au wananchi ni lazima yafanywe kwa kuangalia thamani ya soko na sio vinginevyo. Kinyume cha hapo hujuma kwa mradi inaweza kutokea kutokana na wamiliki kutokuridhika na hivyo kutokutoa ushirikiano.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 4 inayotoa uhuru wa kusafirisha mafuta kwa Tanzania kutoa haki zote kwa nchi ya Uganda hadi Bandarini, kwa maana nytingine ni kuwa Bandari ya Chongoleani-Tanga ni mali ya Uganda na pia haki hiyo ambayo Tanzania tumeitoa kwa Uganda inaenda pia kwa Wamiliki wa Meli zitakazokuja kununua mafuta.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu ni kwa jinsi gani Mamlaka ya Bandari itajihusisha/ itahusika na biashara hii ya kutoa huduma kwa meli za mafuta zitakazokuwa zinatia nanga katika Bandari hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 10 inayohusu umiliki wa mafuta yaliyomo kwenye Bomba. Kambi Rasmi inashindwa kuelewa kwani vifungu vya Ibara hiyo vinaeleza kuwa hakuna mshirika atakayekuwa na haki ya kudai kuwa mafuta ni mali yake, bali ni Yule atakaye fanya utaratibu wa kibiasara na mmiliki wa meli kwa kushirikiana na kampuni ya pamoja iliyoundwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya pamoja ambayo inapewa mamlaka makubwa katika biashara hii ya Bomba, mkataba haukusema kuwa itasajiliwa wapi katika mataifa haya wananchama. Kambi Rasmi ya Upinzani inawasiwasi kwamba Kampuni hii inaweza kusajiliwa "off shore" kwenye nchi ambazo hazihusiana na ulipaji wa kodi na nchi maarufu kwa uchukuaaji na utunzaji wa fedha chafu, kama ambavyo

baadhi ya makampuni yaliyoingizwa hapa nchi na kuchukua rasilimali zetu kama ile ya meremeta ilivyokuwa na mwisho wa siku tukabaki kulaumiana tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufanuzi wa kina kuhusu umiliki wa mafuta hayo yanayotoka Uganda na kusafirishwa nje kuititia bandari mpya itakayojengwa katika kijiji cha Chongoleani.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona lingekuwa ni jambo la busara kwa Bunge hili kutokuridhia azimio hili hadi pale mkataba utakapopitiwa vizuri na kujiridhisha kuhusiana na vifungu ambavyo tunaona vinaathari kwa watanzania moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasillisha.

.....  
**Devota M. Minja (Mb)**  
**K.n.y Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya**  
**Upinzani-Wizara ya Nishati na Madini.**  
11.09.2017

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumeshamsikiliza Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja, Kamati na pia Msemaji wa Upinzani.

Ninayo majina hapa ya walioomba kuchangia, kwa hiyo tutaanza na uchangiaji halafu mtoa hoja atapewa fursa ya kuhitimisha. Tutaanza na Mheshimiwa Mussa Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kuunga mkono hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani. (*Makofii*)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kusema hayo, nami nina yangu machache ya kuzungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya njema na kuweza kukutana katika Kikao chetu hiki cha Bunge na hatimaye kuipitia taarifa hii ya *Intergovernment Agreement Between the United Republic of Tanzania and the Republic of Uganda Concerning the Pipeline System of the East African Crude Oil Pipeline Project*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nami nina yangu ya kushauri. Kwanza, nishukuru kwamba mradi huu umekuja kwenye Jimbo letu la Tanga ambayo itakuwa ndiyo *last destination*. Vilevile niwashauri wale ambao mradi huu utapita katika maeneo yao, katika mikoa nane, wilaya 24 na vijiji takribani mia moja na ushehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwanza tushirikishe wananchi wetu katika suala hili lakini vilevile na Serikali nayo itoe maandalizi maalum kwa sababu wananchi wengi huu mradi wamekuwa wakiusikia juujiu, lakini hapa nishukuru kwamba Kamati yetu ya Nishati na Madini imelifanyia kazi vizuri na imetoa baadhi ya tahadhari na hata Kambi Rasmi ya Upinzani katika baadhi ya maeneo ambayo nikipata nafasi nikayataja huko mbele, imetoa tahadhari, lakini makubwa zaidi ninayoona ni haya yafuatayo.

Kwanza, Serikali iwe makini katika kila hatua kuepuka tabia ya kusaini mikataba ambayo baadaye inakuja kuonekana kuwa mikataba mibovu kama ilivyosemwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu malipo ya fidia, yazingatie bei ya soko la ardhi iliyopo sasa na pasiwe na visingizio. Kwa mfano katika eneo la Chongoleani wananchi kule wamelipwa eka moja kwa thamani ya shilingi milioni mbili na baadhi walikuwa wakitaka ufanuzi zaidi kujua kwa nini wanalipwa pesa hiyo kwa sababu wapo watu ambao walikuwa wamenunua, ule ni Ukanda wa Pwani

kabisa, wapo watu waliokuwa wamenunua eka moja kwa zaidi ya hata milioni 10, lakini baada ya kutaka ufanuzi tukaenda kwa Mkuu wa Mkoo wakaitwa wataalam wa ardhi wao wakasema tu moja kwa moja kwamba bei ya milioni mbili iliwekwa kabla hapajawekwa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo kwa kweli lileta taabu kidogo kwa sababu binafsi kwa maoni yangu niliwahi kuwaeleza kwamba lazima mjue wakulima hawa maeneo yao ambayo yalikuwa ndiyo chanzo chao cha mapato yanachukuliwa. Zao kubwa katika maeneo ya Chongoleani ni minazi, mihogo, midimu, milimao, michungwa na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nikueleze tu, ndimu katika maeneo ya Chongoleani imekuwa na faida kubwa sana kwa sababu mdimu mmoja unaweza kutoa visalfeti viwili na kila kiroba cha ndimu kikifkishwa katika soko la Dar es Salaam ni sawasawa na Sh.40,000. Kwa hiyo, mti mmoja wa mdimu unaweza kutoa katika zao la awamu moja Sh.80,000 ya Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilliomba Serikali kwamba kwa kuwa wananchi wale maeneo yao yanachukuliwa basi watafutiwe maeneo mbadala. Vilevile pia kama tunavyojua kwamba kuna thamani ya ardhi na thamani ya mimea, kwa hiyo, yote hayo nilitaka Serikali iyazingatie. Sasa nawashauri Waheshimiwa Wabunge wengine ambapo mradi huu utapita wawe makini na hilo ili tusije tukawarudisha wananchi wetu katika lindi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tujue kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda tunaamua kuchukua maeneo yale ya wananchi, basi lazima wananchi wale tuwatafutie maeneo mbadala kwa ajili ya shughuli zao za kilimo. Kwa mfano, katika eneo la Chongoleani lipo shamba la mkonge linalomilikiwa na Kampuni ya *Amboni Limited* ambayo sasa hivi imebadilisha jina inaitwa *Cotel Company Limited*. Shamba lile limekuwa haliendelezwi, kwa hiyo,

naiomba Serikali hususan Mheshimiwa Rais alifutie hati shamba lile la Amboni ambalo liko eneo moja linaitwa Mwanyungu na wananchi wale ambao maeneo yao yamechukuliwa wapewe maeneo ya Mwanyungu sasa katika shamba la mkonge ili waendelee na shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu wengi wamekuwa wakilalamika kwamba maeneo yamechukuliwa lakini fedha waliyolipwa haikidhi kwenda kununua mashamba au ardhi maeneo mengine. Wale ambao nyumba zao zimepitiwa na mradi pamoja na kwamba ni nyumba za tope lakini kwa fedha waliyopewa labda mtu anaweza akawa ana eka nne amepata labda shilingi milioni nane na fidia ya mimea labda amepata shilingi milioni nne, shilingi milioni 12 leo huwezi ukajenga nyumba yenye hadhi na ya kisasa, kwa sababu lengo letu ni kwamba wananchi wetu waishi katika maisha bora na nyumba ambazo zina huduma zote za kibinadamu. Kwa hiyo, mimi niombe tu kwamba Serikali iwe makini katika kufidia wananchi wetu lakini pia kuwapatia maeneo mbadala ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusiana na suala zima la *first priority* kwa wale wakazi ambao wanapitiwa na mradi. Kwa mfano, zimetajwa ajira hapa takribani 10,000 ambazo zitajitokeza katika mradi, lakini kutakuwa na zile ajira ambazo ni *permanent* takribani 1,000. Sasa hatukuchanganuliwa hapa katika hizi ajira 1,000 labda zitagawanyika *vipi ki-percentage*, kwamba katika 1,000 asilimia kadhaa itatoka Uganda, asilimia kadhaa itatoka Tanzania. Tuwe makini hapa, tusije tukakuta zile ajira 1,000 zote zinatoka kwa wananchi wa Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tena viongozi wa ngazi mbalimbali ambao wanapitiwa na maeneo ya mradi kuanzia Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, hata Wenyeleviti wa Vijiji na Vitongoji wawe wanashirikishwa kwa karibu katika zoezi zima la mradi huu. Kwa sababu lengo ni mradi huu uwe na manufaa kwa Watanzania isije ikawa tena mradi umekwishaanza panaanza manung'uniko ya hapa na pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nashukuru katika Jimbo langu nimeshiriki kwa asilimia kadhaa au kwa asilimia takribani 70 katika haya masuala yote ya mradi, ndiyo maana umeona pia hata Tanga hapakutokea manung' uniko mengi kuhusiana na mradi huu. Kwa hiyo, naishauri Serikali kule ambapo mradi huu utapita wananchi, Viongozi wa Vijiji, Mitaa, Madiwani, Waheshimiwa Wabunge washiriki kikamilifu. Waelewe *in and out* katika kila kinachoendelea katika mradi huu ili baadaye tusije tukaja tukabeba lawama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile pia nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge, mtakaposhiriki kikamilifu katika mradi huu tukawatetea wananchi wetu itakuja kuwa ni sababu mojawapo ya wewe kurudi tena humu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk, naona una imani nzuri sana ya kurudi humu ndani. (*Makofii/Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Nkamia.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Sina budi kuanza kwa kusema naunga mkono hoja tena kwa furaha kubwa sana. Ungekuwa unaruhusu kidedea humu tungesema neema, neema, neema imefunguliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imepata bahati nzuri, bahati kubwa kwamba hayawi hayawi yanakuwa, hatimaye makubaliano haya au mkataba huu ukawa umesainiwa na sasa hivi unaendelea kuwa mkataba unaitwa *treaty*. Kwa hiyo, naomba kwanza niseme kama Watanzania tujue tofauti ya mkataba huu na ile mikataba ya madini, mikataba ya madini, *those are contracts*, ile ni mikataba ya makampuni, lakini hii ni *treaty* maana yake makubaliano kati ya Serikali na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba kabisa kusema tuisipotoshe Watanzania kwa sababu tunataka kutoa mawazo mbadala. Katika suala hili tuungane kama Taifa na kama Bunge, kwanza kumpongeza Rais wetu kwamba hapa ameingiza goli, hapa utake usitake goli limeingia na hongera sana, tunashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili mimi nimelifuatilia kwa muda mrefu na najua kwamba ilichukua muda. Haikuwa kitu rahisi kwa mtu kufanya maamuzi kutoa zile *concessions* kama tulivyoona pale Chongoleani kwa wale tuliokwenda kuwawakilisha. Katika hili nawashukuru sana kwamba na ninyi mlihakikisha kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Kamati mbalimbali tulishiriki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niungane kabisa na Taarifa ya Kamati kama ilivyotolewa. Niwapongeze sana kwa kufanyia kazi mkataba huu. Nimesikiliza sana mapendekezo na mimi nakubaliana nayo. Sasa nasimama hapa kuongezea tu yale ya wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, mimi bomba hili linapita katika kata sita za Jimbo langu. Bomba hili linapotoka Ngenge linaingia Burungula, likitoka Burungula linakwenda Mubunda, likitoka Mubunda linapiga kona liko Karambi, likitoka Karambi linaingia Kimwani, likitoka Kimwani linaingia Nyakabango likipinda likitafuta Chato. Kwa hiyo, jamani ni mambo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa niaba ya wananchi na naunganana na Waheshimiwa Wabunge wengine walionitangulia waliosema kwamba sisi kazi yetu ni nini, kazi yetu kwanza ni kuuelewa mkataba huu na kuusifu na kujua kwamba katika mkataba wa nchi kwa nchi ni *give and take*, huwezi kusema kwamba utachukua kila kitu uweze kuleta bomba Tanzania, au siyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, bomba hili lilikuwa na njia tatu na mnajua kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli

alikazana sana kulitoa Kenya kulileta huku, si kazi ndogo, naomba kabisa Bunge hili tumpigie makofi. Katika kulileta, katika mikataba, dhana ya *treaty*, dhana ya mikataba lazima uwe na *concessions*, sasa tuko katika kipindi ambacho tunaangalia mikataba yetu, hatutaki kuingia katika mikataba mibovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba mibovu inatokana na usiri, sasa tuko hapa tunajadili jambo na Kamati imeshaona mkataba unavyokwenda, sasa kuboresha, lakini watakapokuja wanaweza kuja wakasema tunapata nini. Mimi nilikuwepo Chongeleani, Tanga na Mheshimiwa Rais alisema faida tutakozipata kwa hesabu ya haraka, mapipa 216,000 kwa siku na bei inaweza ikayumba lakini kwa bei ya chini tulioambiwa zilikuwa ni dola 12 kwa pipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kila siku tuna uwezo wa kupata dola 2,592,000, hapo utasema kwamba Dkt. Magufuli hakucheza jamani? Alicheza, kwa sababu mafuta haya sio ya kwetu, mafuta ni ya Waganda lakini na sisi tumeingia pale kwa sababu tumepata ushoroba, kwa hiyo tulinde amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuhimiza kwa wananchi wangu, tungependa amani. Sisi kazi yetu lazima tuwe na ulinzi shirikishi, ulinzi wa kitaalam lakini pia ulinzi shirikishi. Kulinda bomba hili litakuwa nijukumu la Watanzania wote. Tumelipata kwa sababu ya utulivu ambao kwa kweli wahenga waliufanya kazi na sisi tunaendeleza. Kwa hiyo, ulinzi ndicho kitu kikubwa ambacho nakiona hapa lakini pia na fursa na ajira ambazo Mheshimiwa Waziri ameshasema katika hotuba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika suala la ulinzi naomba sasa tusiibue migogoro ya ardhi. Naposimama hapa kule kwangu kuna watu wanapima ardhi katika hizi kata nilizozitaja ambapo bomba linapita na mimi kama Mbunge wa eneo wala sina taarifa yoyote. Kwa hiyo, naomba jamani hapa Serikali, Mheshimiwa Waziri, msituchanganye na

Mheshimiwa Waziri wa Mifugo naomba utusimamie. Suala hili, Waheshimiwa Mawaziri, mimi ntakuwa mkweli, nikiona mnasusua mimi nakimbia naenda kwa Waziri Mkuu, naamini watatusaidia huko ngazi za juu kama ikibidi lakini tusifike huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabisa katika upimaji wa ranchi, watu wanaosema wanapima ranchi katika maeneo ambapo bomba linapita wanatuchanganya. Wananchi sasa hivi kuna tataruki kubwa sana, wananchi wanalia kabisa *nbagila bati twafa twafa*. Sasa kilio kule twafa, twafa, wakati tunasubiri bomba, sasa bomba likija upimaji wa bomba utakwendaje? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamezungumzia fidia, fidia ni muhimu na wanaochanganya mambo ya ardhi, ile ardhi itatwaliwa kwa fidia kwa mujibu wa sheria inakuwa sasa bomba litapita katika ardhi ushoroba itakuwa ni mali ya Serikali, haitakuwa tena mali ya watu binafsi. Huwezi kupitisha bomba la Serikali katika ardhi ya watu binafsi, itatwaliwa ile ardhi lakini mimi mwenyewe kama nilivyosema, tutasimamia haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa hili na wewe utuwekee nguvu, hao watu ambao wako kule Muleba wanawachanganya wananchi, naomba Serikali, Mheshimiwa Waziri ananisikia, naomba watusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipofika Biharamulo alisema kwamba suala la mifugo ni ufugaji wa kisasa sasa, mambo ya kurandaranda na mifugo hakuna tena. Kwa hiyo, tunakwenda kupima ardhi lakini kwa taratibu. Huwezi kupima ardhi za vijiji bila kuzihawilisha kwanza. Mimi ninavyojuu mchakato wa kuhawilisha ardhi mpaka Rais anatoa *notice* ya miezi mitatu, sasa hiyo *notice* ya kwenda kuipima Muleba imetoka lini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili pia niiwasilishe, na suala lenyewe ni tete tena linavuruga bomba la mafuta, maana yake ni kwamba linakwenda kuvuruga amani tunayoizungumzia. Naomba barua hii ambayo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, pia kwa Mheshimiwa Mwijage yeye mdomo wake hawezi akasema zaidi hapa labda lakini mimi nalitaja wazi wazi hapa. Wananchi wa Muleba hawawezi kutuelewa mimi na Mwijage hatutaeleweka na Wabunge wengine hapa kutoka Mkoa wa Kagera tusipozungumza suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili pia litavuruga amani, linapandikiza mgogoro wa ardhi, sisi hatukubali na tunaomba Serikali itusaidie, naamini watendaji wamekurupuka, wamekwenda kule bila kufuata utaratibu naomba mtusaidie na naomba barua hii niiwasilishe kwako na iwe sehemu ya *Hansard*. Kusema kwamba huwezi kwenda kupima kata sita, kata kumi. Hata na kule Kaskazini pia wameathirika hata sisi wawakilishi wa wananchi hatuna habari, wananchi wanatupigia simu katika taharuki kubwa sana. Wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa Biharamulo alifafanua...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tibaijuka malizia maelezo yako dakika moja.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kimsingi ni siku ya furaha, ni wale wanaotaka kutuharibia hao ndio tujadiliane nao lakini nadhani hili ni jambo jema limekuja Tanzania, vijana changamkeni, jifunze mgambo, mkalinde bomba la mafuta. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Nkamia tutamalizia na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote

nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai mimi na sote tuliomo humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kabisa niishukuru na kuipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufulsi kwa kufanikisha mradi huu wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ni muhimu sana kwetu, na wote tunafahamu kwamba kulikuwa na kama mashindano hivi kati ya nchi hizi za Afrika Mashariki kuhusu bomba lipite hili wapi, lakini baada ya Serikali ya Tanzania kufanikiwa na mradi huu kuzinduliwa kule Tanga kwa kweli imekuwa ni faraja kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Chemba bomba hili linapita si chini ya kilometra 170 kutoka mpakani na Kiteto hadi mpakani na Singida. Linapita Mrijo, Chandama, Songolo, Goima, Paranga, Farqwa, Kwamtoro, Ovada hadi Kinyamshindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, wananchi ni vizuri wakaelezwa mapema ili wasiendeleze baadhi ya maeneo yao kwamba bomba hili litapita wapi. Lakini pia itakuwa vyema sana kwa wale ambao wataguswa na eneo lao kuchukuliwa wakalipwa fidia yao stahiki kwa kipindi muafaka, litakuwa limewasaidia sana. Pia ni mradi mzuri kwasababu ukiangalia kwa siku, Mama Tibajuka alikuwa anajaribu kupiga hesabu pale na mimi nimejaribu kupiga hesabu hapa kwamba kwa siku Tanzania tunapata dola 2,708,325, *it's a huge amount of money*na hii hela itatusaidia sana.

Sasa mimi ombi langu ni kwamba ni vizuri Waheshimiwa Wabunge pamoja na Madiwani wa maeneo husika. Kwa sababu nimeanza kuona kuna tatizo moja dogo tu na ningeomba kuishauri Serikali; kwamba wanawashirikisha sana Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Hawa ni watendaji wa Serikali, lakini wanaoulizwa

maswali ni Wabunge na Madiwani. Mbunge ukienda mahali wananchi wanakuuliza hebu tuambie bomba likipita hapa sisi tutafaidika nini? Mbunge unashindwa kutoa majibu kwasababu aliyeqwenda kuhudhuria hivi vikao vingi vingi hivi ni Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa na nashukuru sana baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambako bomba hili linapita walishirikishwa kule Tanga.

Ningetoa rai kwamba sasa tunapokwenda kwenye *process* hii ya ku-*finalize* hili suala Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani wa maeneo husika ni vizuri wakashirikishwa. Seriakli msi-*ignore* sisi ni wawakilishi wa wananchi tu lakini sisi ndiyo *responsible* kwenye maswali ya wananchi. Kwa nia njema tu, tushirikisheni ili na sisi twende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kiwango hiki cha fedha tutakachokipata ni kikubwa kidogo. Maeneo mengi bomba hili litakapopita vijiji vingi havina maji, na ndiyo maana mimi na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Dodoma, Manyara na hata Tanga bomba lilikopita ndiko ilikopimwa barabara ya lami kutoka Handeni - Kiberashi - Kibaya - Mrijo, Chemba - Donsee - Farqwa - Porobanguma - Kwamtoro mpaka Singida. Kwa hiyo nadhani ni wakati muafaka saa Seriakli ijenge ile barabara kwa kiwango cha lami ili hata usimamizi na usalama wa bomba hili uwe mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya nakushuru sana na ninaipongeza sana Serikali na naunga mkono. Jambo hili ni jambo jema sana kwentu, ni jambo jema kwa Watanzania wote tuungane ili tufike pale Mheshimiwa Rais wetu anataka tufike pamoja na chama chetu, chama tawala. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vedustus Manyinyi, halafu Mheshimiwa Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia

katika hoja iliyopo mbele yetu inayohusiana na bomba la mafuta kutoka Uganda mpaka Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kila jambo huwa linakuwa na mapingamizi, lakini tuseme tu kweli kwamba kwa kazi hii aliyoifanya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba bomba hili tunaweza kupewa huu mradi ni kazi ambayo anastahili kupongezwa sana, kwasababu kwanza ni mradi ambao umechukua muda mfupi sana, lakini wote tunafahamu ni kwa kiasi gani wenzetu wa Kenya walivyokuwa wanautaka mradi huu kwa udi na uvumba, lakini imekuwa bahati nzuri tuimeweza kuupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako manufaa ya wazi wazi ambayo yatatokana na mradi huu maana hili bomba litakapo jengwa maana yake ni kwamba hata barabara katika maeneo hayo yote zitapita na watu wetu ambao wako katika maeneo hayo watafaidika zaidi katika biashara zao mbalimbali, watafaidika na ajira ambazo zitatokana na mradi huu. Hii ikiwa ni pamoja na Serikali itaendelea kupata kodi katika mradi huu, lakini na ile tozo ya upitishaji wa mafuta kwa sababu lile bomba linalopita katika nchi yetu, kwamba *tuta-charge* kile kitu kinaitwa *throughput* ambayo kwetu sisi vilevile tutafadika nayo mbali na kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu kwamba katika hili bomba linalopita kama ingwezekana, maana nimeambiwa kwamba bomba hili tunalijenga sisi, Serikali ya Uganda pamoja na Kampuni za mafuta ikiwemo Total. Basi kama tungeweza ni vizuri na sisi nasi kama Serikali tungeongeza nguvu zaidi au mtaji mkubwa ilio kwenye lile gawiwo tutakalokuwa tunapata basi tuweze kupata kiasi kikubwa zaidi kuliko ambacho tunachoweza kupata kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, jambo lingine ambalo limenifurahisha ni pale ambapo Serikai ili amua kuweka nafasi kubwa ambayo itapitisha bomba la gesi,

ikiwezekana na miundombinu mingine labda bomba la mafuta ghafi lakini ikiwezekana na bomba la gesi

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme, kama inawezekana hebu Serikali ione uwezekano wa kupitisha bomba la mafuta kutoka Tanga litakalokwenda sambamba mpaka kule Uganda. Hilo bomba kama endepo litakuwepo vilevile litakuwa na manufaa makubwa. Kwanza, kama ni gharama za fidia tutakuwa tumeshalipa kwa hiyo tayari eneo tutakuwa nalo. Hata hivyo leo itoshe tu kusema kwamba wenzetu majirani mafuta yanafika Mombasa lakini wanaweza kuuza Uganda, Rwanda, Burundi na hata DRC kushinda sisi siyo kwa sababu nyingine, ni kwa sababu wana bomba la mafuta linalotoka Mombasa mpaka Kisumu; Mombasa mpaka Eldoret.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu na sisi nafasi hii tumeipata, ukweli wa ni kwamba ukiweka bomba kutoka Tanga la mafuta likaenda mpaka Uganda maana yake sisi tutakuwa tumeshaminya zaidi ya kilometa 400, tutakuwa tuna kilometa 400 chini ya wao. Kwa hiyo tafsiri yake ni kwamba gaharama za mafuta kufika kwenye hizo nchi zitakuwa ni ndogo kwahiyo vilevile tutaendelea kufaidika zaidi kuliko wao kwa hiyo, hiyo kwetu itakuwa *competitive advantage* kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitahadharishe tu juu faida ambayo tunayo lakini hatuiangalii sana, kwamba sambamba na hili bomba la mafuta gahfi tulilonalo tunayo miradi kama hii. Kwa mfano liko bomba hili la TAZAMA ambalo linatoka Dar es salaam mpaka kwa wenzetu kule Zambia pale Kapirimposhi na Ndola.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili bomba hatulitumii sana, ni bomba la mafuta ghafi pamoja na mafuta masafi, lakini cha ajabu ni kwamba tunaacha kutumia lile bomba lakini malori mengi yanapitisha mafuta kupeleka huko na mtokeo yake ni kwamba kwanza yanaendelea kuharibu barabara lakini na gharama za uendeshaji nazo zinakuwa kubwa. Kwa hiyo, ni vizuri tukaangalia namna tunavyoweza

kutumia hii miundombinu ambayo kwangu mimi ninaamini kabisa kwamba tukiitumia vizuri inaweza ikatuletea faida zaidi; ukilinganisha kwamba kwa Tanzania kijigrafia tumekaa vizuri, kwamba inatupa nafasi nzuri zaidi ya kufanya biashara na wenzetu wanaotuzunguka kuliko wenztu ambao wako pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo bada ya kusema hayo, na mimi naunagana na wenzangu kwa kuipongeza Serikali kwa kazi hii ambayo wameifanya kwa haraka, lakini niseme tu kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria uje uhitimishe hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuonesha kupitia michango yao mbalimbali hapa, kwa kweli mshikamano na Serikali katika suala hili kimsingi simuoni hata mmoja ambaye anaona kwamba huu mradi hauna tija kwetu. Wote wanaunga mkono, na ni maeneo machache tu ambayo Waheshimiwa Wabunge wanataka kufanyike *fine tuning* (marekebisho ya uboreshaji) na kuipa Serikali tahadhari hapa na pale, hayo tunayapokea. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni saba, sita kwa kuongea na mmoja kwa maandishi; na hoja kubwa ambayo nimeiona katika michango yote hapa, pengine nianze na Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini; ni kuwa mkataba huu ukuuangalia kwa umakini unakinzana na Sheria yetu ya mamlaka ya nchi kuhusiana na umiliki wa Rasilimali na maliasili na unaiona hoja hiyo hiyo ikitolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba niiiongelee kwa kifupi hoja hiyo. Naomba nianze kusisitiza kwamba Sheria yetu hii ya Maliasili na Rasilimali tulioipitisha, ya *sovereignty* inahu maliasili zetu. Katika mkataba huu na

mradi huu, tunachokiongelea hapa ni mafuta ya Uganda. Sisi ni wasafirishaji, sisi tuna lori lakini mikungu ya ndizi iliyoko ndani tunayoitoa Kyela kuileta Dar es Salaam si yetu ndiyo maana naona maudhui ya sasa hayaoani na yale ya Sheria ya *permanent sovereignty*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwa mfano juzi hapa tumepitisha Sheria hapa ya Azimio la Bonde la Mto Songwe lilletwa tena hilo suala. Sasa hizi ni *shared resources*, sasa wakati tunakuta nchi mbili zenyе *sovereignty* zimekaa pamoja, lakini sisi sheria yetu ndiyo ikachukua *pre-dominants* na ikawa na *over-riding effect* kupita sheria zao wenyewe pia wenzetu upande wa pili hilo katika sheria za kimataifa sijawahi kuliona. Mnakaa chini mnajadiliana na mkataba huu ni zao la makubaliano kati ya nchi mbili zenyе *sovereignty*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunafaidika na kodi, kwa ajira pamoja biashara kadhaa zitakazojiteza. Mimi pengine niungane na Profesa Tibaijuka hapa amesisitiza pia. Hebu tuone tofauti kati ya mkataba, tuna mikataba ya madini na Serikali, ni tofauti na mikataba kati ya Serikali na Serikali ambazo ni international *treaties* ipo tofauti kubwa naomba tuisichanganye. Mimi nakushukuru sana Profesa Tibaijuka kwahuo mchango wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumepokea hoja nzuri tu kutoka kwa Kambi Rasmi ya Upinzani lakini kuhusu kifungu cha pili kiko katika ukurasa wa tatu wa hotuba ya Kambi ya Upinzani; kwamba kifungu hiki kinazuia taarifa na kwamba inafanana kabisa na mikataba inayoingiwa kisirisiri na mpaka hata Bunge hili linanyimwa hizo taarifa. Nilitaka tu kusema kuwa kifungu hiki hakizui utoaji wa taarifa, bali kinaweka utaratibu bora tu wa kutoa taarifa hiyo kwa kuitaarifu nchi iliyotoa taarifa nayo iweze kutoa taarifa yake, ni heshima tu. Ni sawa na kusema leo hii sisi Wabunge tuna haki ya kuwa na mikataba, lakini huendi tu wewe mwenyewe moja kwa moja kwenda kuchukua, unapitia kwa Spika. Sasa huo utaratibu wa kupitia kwa Spika ikaonekana ni kizuizi hilo itakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema tu kwamba, haya tu ni makubaliano kati ya nchi na nchi, ni utaratibu tu kama ule ambao tumejiwekea hapa hata wa mikataba, hebu pata ridhaa basi ya nchi mwenzako. Mwenzano amekupa taarifa sasa wewe unaisambaza tu maan taarifa inahitajika na Bunge. Mimi nina uhakika kwa ushirikiano tulionao, Uganda si nchi ya kigeni, si nchi iliyo nje ya bara hili, ni majirani zetu, wote tuko chini ya *East African Community* mimi nina uhakika mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile si kweli kuwa tumetoa uhuru mkubwa mno kwa Uganda kiasi cha kwamba tumewapa hata umilikiwa wa Chongoleani ya Tanga, habana. Tulichofanya sisi ni kuipa Uganda haki ambazo zinasimamiwa na sheria za kimataifa. Uganda ni *land locked state* na *land locked state* zote duniani zina haki zao sawa hasa ukisoma Sheria yetu hili *UN Convention on the Law of the Sea*, wana haki ya kupewa treatment ya kuitisha mizigo yao, kuwapa haki sawa, wasijisikie kwamba wanapoteza kwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wameongea wote wanaoguswa na bomba, nimefurahi sana. Mheshimiwa Mussa Mbarouk anasema tuwe waangalifu na fidia ya ardhi kwa wananchi wetu. Mimi nafikiri hili ni wazo zuri, tumelipokea na tunaomba sasa Serikali haina mikono mingi, sisi wawakilishi wa wananchi bomba litapita kwenye maeneo yetu, sisi tuwe mstari wa mbele kutetea haki za wananchi wetu hasa upande wa ardhi. Serikali itaweza kuchukua hatua tukisikia wawakilishi wa wananchi mko mstari wa mbele na kusema hapana, hapa kunaonekana kuna hitilafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna hoja ya kuwapa *priority* aliyotoa Mheshimiwa Mbarouk, kwamba tutoe *priority* ya ajira kwa wale wanaopitiwa na mradi, hiyo ni sahihi kabisa, hili ni suala la utekelezaji. Hata hivyo naomba nisisitize kwamba mradi huu tumesema unatekelezwa na *private sector* ambayo inahitaji *efficiency*, inahitaji kukimbilia fursa. Huwezi tu umekaa chini ya mwembe sasa wewe kwa sababu unapita kwako basi ubembelezwe ili ukafanye kazi

pale. Tuchangamkie fursa na Waheshimiwa Wabunge tuwe mstari wa mbele kuchangamkia fursa kwa niaba ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kwa kweli nakushukuru sana kwa michango yako. Mimi nafikiri...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) nataka kuongeza muda wa nusu saa ili tumalizie hoja hii ya Mheshimiwa Waziri hapa. Kwa hivyo nitawahoji maana fasili hii inaitaka niwahoji.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Sawa, ili kumbukumbu zikae sawa sawa, Wabunge wamehojiwa kuongeza nusu saa na wamekubali. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa ongezeko hili la muda ingawa sijawatendea haki wale wa mwanzo nilikuwa nakimbia kwa sababu najua muda ulikuwa umekwisha. Hata hivyo, naomba tu nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, ameongelea suala la ulinzi. Kwa kweli suala la ulinzi ni kitu muhimu sana kwetu wote Watanzania. Bomba hili ambalo linalopita nchini kwetu lina faida, lina tija kwa Taifa na kama alivyosema, ni wajibu wetu mkubwa Watanzania wote kuhakikisha usalama wa hili bomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nkamia naye vilevile kama ilivyo kwa Mbarouk, kama ilivyo kwa Profesa Tibaijuka, wote wamepitiwa na hili bomba na Mheshimiwa Nkamia amesitisiza kuhusu ulipwaji wa fidia stahili na kwa muda muafaka. Mimi nafikiri hili ni suala la muhimu, tunalipokea kama Serikali, ni masuala haya ya utekelezaji ambayo lazima angalizo tulichukue. Lakini vilevile kuna kitu

kimoja ambacho ningependa nikiongelee kidogo, ameongelea kuhusu suala la kiwango cha pesa tutakachopata kila siku, amesema ni kikubwa sana. Naja tunafaidika, lakini tusije tuka-exaggerate kiasi cha kupata tukafika mahali ambapo sasa kesho asubuhi tukadaiwa kila mtu anunuliwe bajaj.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha pesa tutakachopata, tukisoma vizuri maelezo niliyoyatoa ni kwamba kila pipa *lita-generate* dola 12.2; sawa, kwa siku kutakuwa na mapipa 216,000 lakini pesa hiyo si kwamba yote inakuja Tanzania, kisome vizuri kile kifungu, tukisoma vizuri kile kifungu ni pesa inatosha kwa sababu hapa tunaongelea *economies of scale*, hatimaye tunapata pesa ya kutosha; lakini si kwa kiasi ambacho kilioneshwa na Mheshimiwa Nkamia kwamba hiyo yote sasa inakuja kwetu hapana! Itakwenda *in proportion* na hisa zetu. Naomba tuisome vizuri hiyo *provision*, itakwenda *in proportion* na hisa. Pamoja na angalizo hilo bado pesa ni nzuri, tunafaidika *at the end of the day*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi ambaye kwa kweli ni kama amerudia tu hoja za wenzako zote. Hata hivyo nisisitize kitu kimoja; kwamba mradi huu haujadondoka kwetu kama zawadi au kama embe dodo tu umekaa chini ya mti likadondoka, tumeupigania kama Taifa. Ndiyo maana tumemshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyofanya ya kidiplomasia kuweza kushawishi nchi jirani kwamba njia bora kuitisha bomba hilo ni Tanzania na faida ni kubwa sana, na ndiyo maana hata ukiisoma hotuba ya upinzani hilo imekubali kabisa kwamba kwa kweli huu mradi una tija kubwa kwa Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito tu kwa Watanzania kwamba lazima maeneo ambayo mradi unapita na vilevile Mkoa wa Tanga wenyewe ambapo ndiyo hatma ya hilo bomba kuishia naomba jamani tuzichangamkie fursa tele ambazo zinajitokeza. Nilipokuwa

Tanga kwenye mkutano wa biashara tulikuwa na Mheshimiwa Mbarouk, nilitoa taarifa kwamba tayari kuna watu (*agents*) wapo Tanga na Dar es Salaam wakishawishi makampuni yatakayokuwa *based* Tanga pale kwamba aah! Sehemu nzuri kukaa ni jirani tu hapa, kuna mahoteli mazuri mnakuja kwa gari asubuhi au kwa helikopta. Sasa hiyo Watanzania tumeshajifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu tulikuwa tunachoronga kule Songsongo, watu walikuwa wanakuja na ndege asubuhi kulala. Ni fursa sasa kujenga mahoteli ya kutosha, fursa sasa kujenga miundombinu ya maisha ya kila siku kwa sababu watakaokuwepo Tanga wana watoto watahitaji kwenda shule, wana familia zitahitaji hospitali, wana familia zitahitaji hospitali, maduka ya dawa mazuri na huduma mbalimbali. Ndiyo maana nasema, la msingi kabisa hapa si Serikali tena, ni sisi Watanzania kuchangamka fursa zilizopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa Waheshimiwa Wabunge, nitawahoji.

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)  
(Hoja liliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba (Inter-governmental  
Agreement – IGA) baina ya Serikali ya Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamuhuri ya  
Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la  
Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki  
(East Africa Crude Oil Pipeline – EACOP)  
kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga  
(Tanzania) liliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda, kwa hiyo Azimio hili limeridhiwa na Bunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa ngazi ya Kamati kwa niaba yetu sisi sote, lakini pia kwa michango yenu hapa ndani ambayo imempa fursa Mheshimiwa Waziri kutoa ufanuzi kwa yale ambayo yalikuwa pengine hatukuya elewa vizuri.

Pia nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa kuhakikisha jambo hili linaenda kwa haraka kama ambavyo Mheshimiwa Rais angependa liende. Mmefanya vyema kutuletea Wabunge ili tuweze kujua ni mambo gani yanaendelea kuhusu bomba hili, na tumepata fursa sasa ya kuipitia na mwisho kupitisha azimio la kuridhia mkataba huu.

Kwa hiyo, tuwatakie kila la kheri katika utekelezaji, na sisi tunaamini kwa sababu kuna changamoto nydingi sana katika Wizara ya Nishati na Madini, kila wakati huwa kuna jambo.

Sasa tunaomba Serikali katika mkataba huu tuje tuyasikie mazuri tu wakati mnatoa taarifa kupitia Kamati, Kamati itakapokuwa inatueleza hapa kuhusu utekelezaji basi mambo yawe yameenda vizuri kama ambavyo leo mmepeata fursa ya kutueleza hapa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha shughuli za Bunge niwatake wale ambaao Kamati zao zinaendelea na kazi kwenda mchana huu kwenye hizo Kamati ili mkapate kukamilisha kazi ambazo kesho tunatakiwa kuzitazama hapa Bungeni.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, siku ya Jumanne saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.10 Mchana Bunge lilsitishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 12 Septemba, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*